# Uraia na Maadili

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la Saba




Taasisi ya Elimu Tanzania

29/10/2020 15:07

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Uraia na Maadili

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la Saba


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 374

Jina la Chapisho: Uraia na Maadili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Saba

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978 - 9987 - 09 - 142 - 3

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 08 Julai 2020 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Darasa la Saba katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2019.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

FOR ONLINE USE ONLY

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2020

Toleo la Kwanza 2020
Chapa ya Pili 2021

ISBN - 978 - 9987 - 09 - 142 - 3

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P 35094
Dar es Salaam - Tanzania

Simu: +255 735 041 170/+255 735 041 168
Barua pepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 2 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

**Shukurani** ........................................................................................v
**Utangulizi** .......................................................................................vi

**Sura ya Kwanza**
Kuwapenda wenzetu katika jamii ............................................... 1

**Sura ya Pili**
Kupenda na kujivunia shule yako ............................................... 13

**Sura ya Tatu**
Kuipenda na kujivunia nchi yako ............................................... 24

**Sura ya Nne**
Kujijali na kuwajali wenzetu ..................................................... 35

**Sura ya Tano**
Kujenga uhusiano mzuri na watu wengine ................................. 49

**Sura ya Sita**
Kulinda rasilimali kwa masilahi ya nchi....................................... 57

**Sura ya Saba**
Kutekeleza majukumu katika jamii ............................................. 64

**Sura ya Nane**
Kutii sheria na kanuni ............................................................... 73

**Sura ya Tisa**
Kujenga tabia ya uvumilivu........................................................ 82

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 3 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sura ya Kumi**
Jinsi ya kufikia malengo ........ 94

**Sura ya Kumi na Moja**
Kuchanganua mambo kiyakinifu ........ 104

**Sura ya Kumi na Mbili**
Kuaminika katika jamii ........ 110

**Sura ya Kumi na Tatu**
Kusimamia haki za binadamu ........ 119

**Sura ya Kumi na Nne**
Kujenga urafiki na mataifa mengine ........ 129

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 4 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi wa kitabu hiki cha mwanafunzi.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao:

**Waandishi:** Dkt. Jerome S. Machange, Mwl. Godlove E. Siara, Mwl. Allen Y. Mufuruki, Mwl. John W. Ngowi, Mwl. Edna M. Mathew, Mwl. Castor A. Lyuma, Mwl. Beatus B. Mapunda na Bw. Fikiri S. Salla (Elimu ya zimamoto na uokoaji).

**Wahariri:** Dkt. Evaristi M. Cornelli, Bw. Chediel R. Nyirenda, Mwl. Benedict A. Ndelele na Bi. Gertrude Joseph (Lugha-BAKITA).

**Msanifu:** Bw. Christian D. Mtavangu

**Wachoraji:** Bw. Fikiri A. Msimbe na Alama Art and Media Production Limited

**Mratibu:** Dkt. Jerome S. Machange

Pia, TET inatoa shukurani kwa walimu wote walioshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki cha mwanafunzi. Vilevile, TET inatoa shukurani za pekee kwa shirika la "Global Partnership for Education (GPE)" kupitia mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) uitwao "Literacy and Numeracy Education Support (LANES II)" kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya uandishi na uchapaji wa kitabu hiki.

Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kwa karibu zoezi zima la uandishi na uchapaji wa kitabu hiki.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kitabu hiki ni cha tano katika mfululizo wa vitabu vitano vya somo la Uraia na Maadili kuanzia Darasa la Tatu hadi la Saba, kilichoandaliwa mahususi kwako mwanafunzi wa Darasa la Saba. Kitabu hiki kimeandaliwa kulingana na Muhtasari wa Somo la Uraia na Maadili wa mwaka 2019 uliotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kitabu hiki kimezingatia mwenendo na matarajio ya nchi yetu ya Tanzania katika kukujengea wewe mwanafunzi uwezo wa kuheshimu na kuithamini jamii yako, kuwa mwajibikaji na mstahimilivu. Maudhui yaliyomo katika kitabu hiki ni mwendelezo wa yale yaliyomo katika kitabu cha Uraia na Maadili Darasa la Sita. Inatarajiwa kuwa, maudhui haya yatakujengea uwezo wa kuwa na tabia ya uadilifu, kupenda, na kudumisha amani katika nchi na kuweza kuishi vizuri na watu wa asili tofauti katika jamii. Kitabu hiki kina sura kumi na nne na kila sura imeundwa na vipengele kadhaa. Aidha, maudhui ya sura za kitabu hiki yamewasilishwa kwa njia ya habari na vielelezo au picha. Kila sura ina mazoezi na kazi za kufanya zinazozingatia kujenga nyanja za maarifa (utambuzi), vitendo (stadi) na mwelekeo (maono). Hivyo basi unapaswa kufanya kazi zote zilizopo kwenye kitabu hiki pamoja na kazi zingine utakazopewa na mwalimu.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 6 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

## Kuwapenda wenzetu katika jamii

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza dhana ya familia, mahitaji ya wanafamilia na vitendo vya kusaidia wanafamilia wenye mahitaji maalumu. Pia, ulijifunza namna ya kuthamini mchango wa wanafamilia katika maendeleo ya familia, kuonesha vitendo vya heshima katika familia na kutenda vitendo vya kuwalinda wanafamilia dhidi ya vikundi hatarishi. Katika sura hii, utajifunza jinsi ya kuelimisha jamii kutoa misaada kwa wahitaji na njia za kuhamasisha jamii kutoa misaada. Vilevile, utajifunza kuhudumia na kufariji wahitaji. Maarifa na ujuzi utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kushirikiana na wanajamii wengine katika kuwapenda na kuwasaidia wahitaji.*



**Fikiri**

1. Msaada uliowahi kutoa kwa kundi lolote la wahitaji.
2. Sababu zilizofanya kutoa msaada huo.

### Kuelimisha jamii namna ya kutoa misaada kwa wahitaji

Wahitaji ni watu waliopungukiwa na mahitaji muhimu kama vile, chakula, malazi, fedha, mavazi au afya njema. Ni muhimu kushiriki katika kuelimisha na kuhamasisha jamii kutoa misaada kwa watu wenye uhitaji. Yafuatayo ni mambo muhimu ya kuzingatia ili kuelimisha na kuhamasisha jamii kutoa misaada kwa wahitaji:

(a) Kubaini makundi mbalimbali ya wahitaji katika jamii tunamoishi;
(b) Kufahamu aina mbalimbali za misaada kwa wahitaji wa kila kundi;
(c) Kubaini njia za kuhamasisha jamii kutoa misaada kwa wahitaji;
(d) Kuelewa namna ya kuwahudumia na kuwafariji wahitaji katika jamii;
(e) Kubaini aina za huduma na faraja tunazoweza kuwapatia wahitaji;



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 1 30/07/2021 20:42


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(f) Kufahamu umuhimu wa kuwahudumia na kuwafariji wahitaji katika jamii; na
(g) Kupanga mikakati ya kuwatambua watu wenye uhitaji.

### Kubaini makundi mbalimbali ya wahitaji katika jamii

Wahitaji katika jamii ni pamoja na watoto yatima, watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, watu wenye ulemavu, na wazee. Kundi jingine la watu wenye uhitaji ni waathirika wa majanga mbalimbali katika jamii, kwa mfano, baa la njaa, janga la moto, mafuriko, magonjwa ya mlipuko, na tetemeko la ardhi.

Angalia Kielelezo namba 1 na 2, kisha jibu maswali yanayofuata.




**Kielelezo namba 1:** *Utoaji wa misaada kwa wazee wenye uhitaji*



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 2 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 2:** *Utoaji wa msaada kwa waathirika wa mafuriko*

### Zoezi la 1

1. Vitendo vinavyooneshwa kwenye Kielelezo namba 1 na 2 vinakufundisha nini?
2. Taja makundi ya wahitaji yaliyopo katika mazingira unayoishi.
3. Ni faida gani utapata ukiwasaidia wahitaji katika jamii unamoishi?
4. Eleza namna utakavyomsaidia mwanafunzi mwenzako mwenye uhitaji.

### Kazi ya kufanya namba 1

Jadiliana na wanafunzi wenzako njia mbalimbali za kuwasaidia wahitaji waliokumbwa na janga la mafuriko. Kisha, andika majibu uliyopata katika daftari lako la mazoezi na wasilisha kwa mwalimu.



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 3 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Aina za misaada kwa wahitaji

Misaada inayofaa kutolewa kwa wahitaji ni ya aina mbalimbali kutegemeana na uhitaji wa wahusika. Baadhi ya misaada hiyo ni chakula, mavazi, malazi, huduma za afya, na vifaa mbalimbali kama vile; vifaa vya michezo, usafiri, na huduma ya kwanza. Pia, ipo misaada ya ushauri na unasihi, ya kisheria, ya fedha, na ya malezi.

Misaada hii hutolewa pale uhitaji unapotokea katika jamii. Kwa mfano, wakati wa baa la njaa au mafuriko, watu huchangia chakula, dawa, mavazi, na malazi kwa wahitaji. Pia, wanafunzi waliokumbwa na majanga wanaweza kuwa na uhitaji wa vifaa vya shule kama vile, sare za shule, madaftari, na vifaa vya michezo kama; mipira, viatu, sare za michezo na vifaa vya riadha. Vilevile, wahitaji wanaweza kupatiwa ushauri na unasihi ili waweze kuhimili changamoto wanazokutana nazo shuleni na katika mazingira wanamoishi. Aidha, msaada wa kisheria ni muhimu ili kutoa haki kwa wanajamii wanaopeleka mashitaka au kushitakiwa mahakamani. Kwa mfano, msaada wa kisheria unahitajika kwa watoto yatima wanaonyanyaswa, kuporwa mali za wazazi wao, kufanyishwa kazi ngumu na kukosa huduma za afya au elimu bora. Ushauri wa kisheria kwa kawaida hutolewa na wataalamu wa sheria. Wataalamu hawa hutoa mchango wao kwa kusaidia kufungua kesi na kuwatetea bila gharama.

### Zoezi la 2

1. Fafanua mahitaji ya makundi mbalimbali ya wahitaji.
2. Ni changamoto zipi zenye kuhitaji ushauri na unasihi unapokuwa shuleni?
3. Msaada wa kisheria una umuhimu gani kwa wahitaji?
4. Eleza msaada ambao umeshawahi kuutoa kwa wahitaji katika jamii yako.

### Kazi ya kufanya namba 2



Jadiliana na wanafunzi wenzako namna ya kuwasaidia wanafunzi wenye uhitaji wa sare za shule, madaftari na kalamu katika darasa lako. Kisha, andika majibu katika daftari lako la mazoezi na wasilisha kwa mwalimu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Njia za kuhamasisha jamii kutoa misaada kwa wahitaji

Watu au taasisi mbalimbali za kijamii hufanya jitihada za kusaidia kupunguza changamoto zinazowakabili wahitaji. Zipo njia mbalimbali zinazoweza kutumika kuhamasisha wanajamii kushiriki katika kutoa misaada kwa wahitaji. Baadhi ya njia hizo ni pamoja na:

(a) **Kutumia vyombo vya habari:** Vyombo mbalimbali vya habari vinaweza kutumika kuhamasisha wanajamii kushiriki katika utoaji wa misaada kwa wahitaji mbalimbali. Vyombo vya habari ni pamoja na televisheni, magazeti, na redio ambavyo vinaweza kufikisha taarifa au ujumbe kwa watu wengi zaidi na kwa urahisi. Kwa mfano, kupitia televisheni, watu wanaoshiriki kutoa misaada wanaweza wakaoneshwa na kusikika. Jambo hili litasaidia kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa kushiriki kutoa misaada kwa wahitaji. Redio inaweza kutumika kutoa matangazo mbalimbali yanayohamasisha juu ya kusaidia kundi fulani linalohitaji msaada. Vilevile, redio na televisheni huweza kutumika kuibua wahitaji na kuhamasisha jamii kuwasaidia kwa njia mbalimbali.

(b) **Kutumia mitandao ya kijamii:** Mitandao ya kijamii ni njia ya mawasiliano inayowezesha kundi la watu kupeana taarifa. Taarifa hizo huibua mijadala mbalimbali. Kwa kutumia mitandao ya kijamii, wahitaji wanaweza kuchangiwa mawazo au michango mingine ya hali na mali. Baadhi ya mitandao ya kijamii ni "Facebook", "WhatsApp", "Instagram", na "Twitter". Mitandao ya kijamii inaweza kutumika kuhabarisha jamii juu ya ushiriki wa watu au kundi fulani katika kutoa misaada kwa wenye uhitaji. Pia, mijadala huweza kuendeshwa kuhusu umuhimu wa kusaidia wahitaji. Vilevile, mitandao ya kijamii hutumika kuhamasisha watu kushiriki katika kuwahudumia watu wenye uhitaji. Vikundi au taasisi mbalimbali zinaweza kushiriki kwenye harakati za kuisaidia jamii. Kwa njia hii, washiriki wengine kwenye mitandao ya kijamii wanaweza wakahamasika na kutoa misaada.

(c) **Midahalo na makongamano:** Hizi ni njia zinazoweza kutumika kuelimisha na kuhamasisha jamii kushiriki katika kuwasaidia watu wenye uhitaji. Katika midahalo na makongamano, mada kuhusu watu wenye uhitaji zinaweza kuwasilishwa na kujadiliwa ikiwa ni pamoja na kupendekeza namna ya kusaidia wahitaji. Mambo yanayohusu watu wenye uhitaji kama wazee, walemavu, yatima, wajane na wanaoishi katika mazingira magumu na hatarishi huweza kupewa kipaumbele ili kuijengea jamii moyo wa kuwasaidia na kubadili hali zao.

(d) **Mabango na vipeperushi:** Mabango na vipeperushi vinaweza kutumiwa

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ili kufikisha ujumbe kwa jamii juu ya umuhimu wa kuwasaidia watu wenye uhitaji. Ujumbe katika mabango na vipeperushi huweza kudumu kwa muda mrefu, hivyo, kuhamasisha jamii hatua kwa hatua.

(e) **Kutembelea nyumba kwa nyumba:** Matembezi ya nyumba kwa nyumba ni njia mojawapo ya kufikisha ujumbe kwa wanajamii. Pia, njia hii hutumiwa na wanaharakati wa masuala ya haki za binadamu katika kusaidia wanajamii kuelewa haki zao. Matembezi ya nyumba kwa nyumba huweza kuwa na malengo matatu tofauti. Kwanza, kubaini wenye uhitaji. Pili, kukusanya misaada kisha kugawa kwa wenye uhitaji na tatu, kuhamasisha watu kujitolea kusaidia wenye uhitaji.

(f) **Semina na mikutano ya hadhara:** Ili kufikisha ujumbe kwa jamii juu ya umuhimu wa kuwasaidia wenye uhitaji, viongozi wa Serikali na taasisi zake hutumia njia hii kutoa maelekezo na hamasa kwa wananchi na jumuiya zinazowazunguka.

(g) **Majadiliano ya vikundirika:** Watu wa rika moja huwekwa pamoja na kufanya majadiliano jinsi ya kuhamasisha na kuwasaidia wenye uhitaji. Njia hii ni nzuri kwani watu wa rika moja ni rahisi kujadiliana bila vikwazo kutokana na kuwa katika umri mmoja na maono yanayokaribiana.

(h) **Matumizi ya sanaa:** Sanaa za maonesho ni nyenzo muhimu ya kufikisha ujumbe kwa jamii kuhusu umuhimu wa kushiriki katika kutoa misaada kwa watu wenye uhitaji. Matumizi ya sanaa kama vile nyimbo, maigizo na majigambo, hubeba ujumbe uliokusudiwa kuwafikia walengwa kwa haraka kwa kuwa kazi za sanaa huvutia.

(i) **Vikundi vya kujitolea katika shule:** Shule inaweza kuwa na vikundi vya kujitolea. Kazi ya vikundi hivi ni kuhamasisha wanafunzi wengine kujitolea na kusaidia watu wenye uhitaji.

### Zoezi la 3

1. Unafikiri ni kwanini vyombo vya habari ni muhimu katika kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuwasaidia watu wenye uhitaji?
2. Kwa kutumia mifano minne, elezea namna vyombo vya habari vilivyokusaidia kupata taarifa juu ya watu wenye uhitaji na namna ulivyohamasika kuwasaidia.
3. Kwanini majadiliano ya vikundirika yana ufanisi zaidi katika kuhamasisha ushiriki wa vijana katika harakati za kuwasaidia wenye uhitaji?



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 6 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Ukiwa kiongozi mtarajiwa, andika insha ukielezea mipango uliyonayo ya kuwahamasisha vijana kushiriki katika shughuli za kuwasaidia wenye uhitaji katika jamii yako.

**Kazi ya kufanya namba 3**

Andaa bango zuri lenye ujumbe maridhawa wa kuhamasisha wanafunzi wenzako kushiriki katika harambee ya kuwachangia vifaa wanafunzi wenye uhitaji shuleni kwako. Wasilisha darasani na toa maelezo kuhusu ujumbe ulioko katika bango.

### Kuwahudumia na kuwafariji wahitaji katika jamii

Huduma na faraja ni vitu muhimu sana kwa watu wenye uhitaji. Hii ni kwa sababu watu wenye uhitaji huwa wanakabiliwa na changamoto mbalimbali za maisha. Vitendo vya kuwasaidia wahitaji huenda sanjari na huruma, faraja na upendo kwa mtoa huduma. Wahitaji huhitaji kufarijiwa ili kuwasaidia kufurahia maisha kama watu wengine. Mtu hufarijika au kupata utulivu baada ya kupewa maneno mazuri ya faraja na ya kutia moyo ili aweze kukabiliana na hali aliyonayo.

Baadhi ya huduma na faraja zinazoweza kutolewa kwa wahitaji ni kama ifuatavyo:

(a) **Huduma ya kisheria:** Hii ni huduma anayopewa mhitaji wa mambo yanayohusu sheria kama vile; kubambikwa kesi, kudhulumiwa mirathi, na unyanyasaji wa kijinsia. Huduma hii humsaidia aliyeonewa kupata haki na kufarijika. Kwa kawaida, huduma za kisheria hutolewa na watu au taasisi yenye wataalamu wa sheria. Huduma ya kisheria inapotolewa bila malipo hujulikana kama “msaada wa kisheria”.

(b) **Makazi:** Huduma hii hutolewa kwa wahanga wa majanga yanayoharibu makazi. Kwa mfano, watu ambao nyumba zao zimebomolewa na mafuriko kipindi cha mvua, kuungua moto au paa kuezuliwa na upepo, hupewa hifadhi ya makazi ili kuwasitiri kwa muda. Aidha, wanaweza kupewa viwanja na vifaa vya ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa makazi mapya.

(c) **Huduma muhimu za kiafya:** Wahitaji hupewa huduma hii ili kukabiliana na matatizo ya kiafya yanayowakumba. Misaada ya kiafya inaweza kuwa vifaatiba, dawa, huduma za matibabu au elimu ya afya.

(d) **Ushauri:** Huduma hii hutolewa kwa mtu mwenye jambo linalomtatiza

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 7 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

na linalohitaji ufumbuzi wa haraka ili aweze kuendelea na mipango yake au ndoto zake. Ndoto au mipango inaweza kuwa inayohusu elimu, afya, kazi, biashara au kilimo. Pia, ushauri huu unaweza kuwa ni wa namna ya kuhimili changamoto za maisha kama vile, kufiwa na wazazi, watoto, kupata magonjwa ya kudumu au wazazi kufukuzwa kazi. Ushauri unaotolewa kwa watu wenye hali hizi huitwa unasihi.

## Umuhimu wa kuwahudumia na kuwafariji wahitaji katika jamii

Utoaji wa huduma na faraja una faida nyingi ikiwa ni pamoja na:

(a) **Kujenga upendo:** Huduma anayopatiwa mhitaji husaidia kujenga upendo. Kwa mfano, mtu aliyepata ajali ya gari, moto, mafuriko na majanga mengine, hujenga upendo mkubwa kati yake na wale waliomsaidia. Upendo huu hutokana na ile hali ya kuona kwamba wanajamii wengine wanajali na kujitolea kumsaidia bila malipo.

(b) **Kujenga umoja na mshikamano:** Kushirikiana kwa pamoja katika kuwasaidia watu wenye uhitaji hujenga na kudumisha umoja na mshikamano kwa wanajamii. Ushirikiano huwaweka watu pamoja ili kutatua changamoto zinazowakabili.

(c) **Kulinda haki za binadamu:** Vitendo vya kuwahudumia wahitaji huwajengea wanajamii utayari na utashi wa kulinda haki za binadamu. Kwa mfano, haki ya kuishi hulindwa na wanajamii kwa kuwapatia wahitaji huduma mbalimbali kama vile; malazi, mavazi, chakula, na matibabu ili kujikimu kimaisha.

(d) **Kudumisha udugu:** Kuwahudumia na kuwafariji wahitaji, hujenga udugu katika jamii. Wanajamii wanapotoa misaada ya kijamii hujenga tabia ya upendo, ushirikiano na kujali wenzao, hivyo kuwafanya waishi kama ndugu.

(e) **Kuthamini utu:** Kutoa msaada na kuwafariji watu wenye uhitaji ni kitendo cha kuthamini utu wao. Mfano wa vitendo vya kujali utu ni kumsaidia mwanafunzi asiyeona kwa kumshika mkono anapokwenda maliwato au sehemu hatarishi kama vile kuvuka barabara na sehemu nyinginezo.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 8 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

1. Ni aina gani za huduma na faraja zinazohitajika katika jamii unamoishi?
2. Taja faida tano  za kutoa huduma na faraja kwa watu wenye uhitaji.
3. Matendo gani ya utu unayoyafanya kwa wanafunzi wenzako?
4. Eleza kwa ufupi umuhimu wa kutoa huduma kwa upendo.

### Kazi ya kufanya namba 4

Kwa kushirikiana na wenzako katika kikundi, chambueni makundi ya wahitaji yasiyopungua matano yanayohitaji huduma na faraja shuleni kwenu, kijijini au mtaani. Kisha, watembelee au buni mbinu mtakazotumia kuwapa huduma na faraja na wasilisha darasani kwa majadiliano.

## Mikakati ya kuwatambua watu wenye uhitaji

Ili kuweza kuwapatia misaada na faraja watu wenye uhitaji, ni muhimu kubaini mahali walipo na mahitaji yao. Mikakati ya kuwatambua watu wenye uhitaji husaidia kuwajua na kuwapa misaada stahiki. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na:

(a) **Mikutano ya hadhara:** Kuwapo kwa mikutano ya hadhara katika vijiji na mitaa husaidia kutambua wahitaji katika jamii. Mikutano huwapa wanajamii fursa ya kuibua changamoto zinazowakabili; kwa mfano, watoto waliopo katika mazingira hatarishi, wajane waliodhulumiwa mirathi, na wanajamii wanaokabiliwa na changamoto mbalimbali za maisha.

(b) **Makongamano na mihadhara ya kidini:** Mikusanyiko ya kidini huhudhuriwa na watu wenye mahitaji mbalimbali. Ushirikiano wa viongozi wa dini na wanajamii katika mihadhara na makongamano husaidia kuwatambua wahitaji waliopo katika jamii na kuwapa misaada. Kwa mfano, makanisani au misikitini, vipo vikundi mbalimbali vinavyoweza kushiriki kubainisha wahitaji.

(c) **Vyombo vya habari:** Vyombo vya habari hutambua na kutangaza changamoto za watu mbalimbali wenye uhitaji. Vilevile, wanajamii hutumia vyombo vya habari kutoa taarifa za watu wenye uhitaji. Mifano ya vyombo vya habari ni televisheni, redio na magazeti. Kupitia vyombo

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 9 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

vya habari, watu wenye uhitaji hutambulika na jamii kisha kupatiwa misaada.

(d) **Kushirikiana na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali:** Ushirikiano na taasisi hizi ni muhimu kwa kuwa taasisi hizi hujihusisha na shughuli mbalimbali katika jamii. Mikakati ya kuwatambua watu wenye uhitaji katika jamii huweza kufanywa kupitia taasisi kama vile shule, zahanati au ofisi za Serikali za mitaa na taasisi za kidini. Taasisi hizi huwa na taarifa mbalimbali ikiwa ni pamoja na taarifa za wahitaji, hivyo ni rahisi kuwatambua wanajamii wenye uhitaji.

(e) **Mitandao ya kijamii:** Hii ni njia inayotumiwa na wanajamii kutoa na kupokea taarifa mbalimbali. Hivyo, inaweza kutumika kwa urahisi kuwatambua watu wenye uhitaji. Kwa mfano, kupitia mitandao ya kijamii kama vile “Twitter”, “Instagram”, na “WhatsApp” watu wenye uhitaji wanaweza kubainishwa na watu kujitokeza kuwasaidia.

**Zoezi la 5**

1. Je, kuna umuhimu gani kwa wahitaji kutambuliwa katika jamii?
2. Taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali zina mchango gani kwa watu wenye uhitaji?
3. Eleza kwa kifupi jinsi Serikali ya mtaa au kijiji inavyoweza kuwatambua watu wenye uhitaji katika jamii unamoishi.
4. Eleza namna ambavyo mitandao ya kijamii inaweza kutumika kuwatambua watu wenye uhitaji katika jamii unamoishi.

**Kazi ya kufanya namba 5**



Kwa kushirikiana na wanafunzi wenzako kwenye kikundi, andaa igizo fupi kuhusu taasisi ya Serikali au binafsi ikitoa msaada wa chakula kwa watu waliopatwa na janga la mafuriko. Onesha igizo hilo wakati wa kipindi darasani.

**Zoezi la 6**

A: Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi.

1. Watu waliokumbwa na majanga ya moto na mafuriko ni miongoni mwa wahitaji.__________

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Televisheni huchangia wahitaji wasipate msaada kwa haraka.______

3. Vyakula, malazi, huduma za afya na faraja ni baadhi ya mahitaji kwa wahitaji.__________

4. Msaada wa kisheria ni muhimu kwa wahitaji katika jamii._________

5. Nyimbo, redio na mitandao ya kijamii husaidia kufikisha ujumbe kwa jamii ili kutoa msaada kwa watu wenye uhitaji.__________

6. Faraja ni kitendo cha kuwaliwaza watu au mtu aliyepatwa na matatizo.__________

**B**: Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake kwenye kisanduku.

7. Huduma za kisheria kwa wahitaji huweza kupatikana sehemu gani?
   (a) asasi binafsi za utetezi wa haki za binadamu, mahakamani na magereza
   (b) kwa mwanasheria, mahakamani, na asasi binafsi za utetezi wa haki za binadamu
   (c) shuleni, vituo vya polisi na vituo vya afya
   (d) mahakamani, ofisi za vijiji na magereza

8. Nini umuhimu wa kuwahudumia na kuwafariji wahitaji katika jamii?
   (a) kujenga upendo na kuthamini utu
   (b) kudumisha udugu na kujitangaza
   (c) kulinda haki za binadamu na haki za kisiasa
   (d) kukuza utegemezi kwa wahitaji

9. Ni njia zipi zinazoweza kutumika kwa haraka kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutoa misaada kwa wahitaji?
   (a) televisheni, redio na mitandao ya kijamii
   (b) semina, mikutano ya hadhara na makongamano
   (c) mikutano ya hadhara, semina na vipeperushi
   (d) redio, mikutano ya hadhara na mitandao ya kijamii



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 11 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C:** Oanisha kipengele kutoka **Sehemu A** na maneno yaliyopo **Sehemu B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.

| Sehemu A | Jibu | Sehemu B |
|---|---|---|
| 10. Misaada kwa wahitaji | | (a) wahitaji katika jamii |
| 11. Mabango na vipeperushi | | (b) wavuti ambapo watu hujumuishwa pamoja na kutumiana ujumbe au kuwa na mijadala kupitia simu za mkononi au kompyuta |
| 12. Watoto yatima na wazee | | (c) ubinadamu, upendo na huruma |
| 13. Utu | | (d) vyakula, mavazi, huduma za afya, vifaa mbalimbali na makazi |
| 14. Mitandao ya kijamii | | (e) njia ya kutoa elimu kwa wahitaji |

## Msamiati

Baa — balaa linalomfika mtu, aghalabu husababisha hasara au maafa

Uhitaji — ukosefu wa mahitaji ya msingi ya binadamu

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 12 30/07/2021 20:42


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili

## Kupenda na kujivunia shule yako

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza kubaini ujumbe uliomo katika kaulimbiu na wimbo wa shule yako. Vilevile, ulijifunza mambo yanayoiletea sifa shule yako na njia zinazoweza kutumika kuitangaza shule yako. Aidha, ulijifunza kuipenda nchi yako kwa kubaini njia mbalimbali za kuitangaza nchi yetu ya Tanzania. Katika sura hii, utajifunza namna ya kushiriki katika shughuli za maendeleo ya shule yako. Pia, utajifunza jinsi ya kushiriki katika kuandaa na kutekeleza mpangokazi wa kujitolea kwa ajili ya maendeleo ya shule yako. Maarifa na ujuzi utakaopata katika sura hii utakuwezesha kushiriki katika juhudi za kuleta maendeleo katika shule yako.*



**Fikiri**

Shughuli ambazo umewahi kushiriki zenye lengo la kuleta maendeleo ya shule yako.

### Kushiriki katika kuleta maendeleo ya shule yako

Kila mtu anatakiwa kushiriki katika kuleta maendeleo kwenye jamii yake. Shule ni sehemu ya jamii, hivyo ni muhimu mwanafunzi kushiriki katika kuleta maendeleo ya shule yake. Mwanafunzi anaweza kushiriki kuleta maendeleo katika shule yake kwa kufanya yafuatayo:

(a) Kulinda mali za shule kama vile vitabu, madarasa, vyoo na ofisi za walimu; samani na vifaa vya kufanyia usafi kama vile, majembe, mafyekeo, mapipa ya kuhifadhi takataka na fagio;

(b) Kushiriki kufanya usafi wa mazingira ya shule;

(c) Kushiriki shughuli za ujenzi wa miundombinu ya shule, kwa mfano, kusomba matofali na mchanga na kusafisha eneo au sehemu jengo linapojengwa;

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Kushiriki kutoa maoni na mapendekezo kwa uongozi wa shule juu ya mambo yanayoweza kuisaidia shule kitaaluma na kijamii; na

(e) Kusoma kwa bidii na kufaulu vizuri mitihani ya ndani na nje ya shule kwa lengo la kuitangaza shule.

### Vitu vinavyohitajika kwa ajili ya maendeleo ya shule

Yapo mahitaji muhimu ambayo yanatakiwa yawepo ili kuiwezesha shule kufanya vizuri na kupata sifa katika jamii na Taifa kwa ujumla. Mahitaji haya huiwezesha shule kufanikisha utoaji wa elimu bora kwa wanafunzi wake. Baadhi ya mahitaji ya shule ni pamoja na chakula, vifaa, maji, umeme, ardhi na fedha.

**Chakula:** Shule inahitaji chakula ili kuwafanya wanafunzi na walimu kuwa na siha njema. Aina za vyakula vinavyohitajika ni kama vile mchele, unga, mafuta, sukari, maharage, nyama, matunda na mboga za majani. Vyakula hivi vikipatikana utendaji kazi wa walimu na wanafunzi huimarika.

**Vifaa:** Shule inahitaji vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia kama vile vitabu, chaki, manila na karatasi kwa ajili ya kuchapishia mitihani na nyaraka nyingine. Pia, huhitaji vifaa vya kufanyia usafi kama vile fagio, fyekeo, majembe, mapanga na mapipa ya kuhifadhi takataka. Vilevile, vifaa vya michezo vinavyohitajika ni mipira ya kuchezea, nyavu za magoli na nguo za michezo. Aidha, shule inahitaji baadhi ya vifaatiba na inaweza kuhitaji vifaa vya malazi.

**Maji:** Shule inahitaji maji safi na salama kwa afya ya walimu na wanafunzi na shughuli nyingine za maendeleo. Maji yanahitajika kwa ajili ya kunywa, kupikia, kumwagilia maua, bustani na miti. Pia, maji yanahitajika kwa ajili ya shughuli za ujenzi, na kufanya usafi kama vile kusafishia vyoo, madarasa, kufua nguo na kuoga.

**Umeme:** Shule inahitaji umeme kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Umeme unahitajika kusaidia wanafunzi wakati wa kujifunza hasa nyakati za usiku. Aidha, umeme unahitajika kuendesha mashine za kuchapisha na kurudufu nyaraka mbalimbali kama mitihani na kuimarisha shughuli za ulinzi wa shule na mali zake. Umeme husaidia shule kutimiza lengo lake la kutoa elimu bora kwa wanafunzi. Mathalan, somo la Sayansi na Teknolojia litafundishwa na kueleweka vizuri kukiwa na huduma ya umeme.



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 14 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Ardhi:** Shule inahitaji ardhi ya kutosha kuwezesha shughuli mbalimbali kufanyika. Ardhi husaidia kupatikana sehemu za kujenga miundombinu kama madarasa, ofisi za walimu, vyoo, maktaba na viwanja vya michezo mbalimbali. Pia, ardhi husaidia wanafunzi kupata eneo la kulima mazao mbalimbali kwa ajili ya kujipatia chakula chao wenyewe. Hivyo, kuwapo kwa ardhi ya kutosha huchochea maendeleo ya shule.

**Fedha:** Shule inahitaji fedha ili iweze kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo. Kwa mfano, shule inahitaji fedha ili iweze kuchapisha mitihani, kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kujenga, na kukarabati miundombinu kama vile madarasa na vyoo. Pia fedha huhitajika kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa shule kwa ujumla.

Mahitaji yaliyotajwa hapo juu yanaweza kupatikana kwa njia mbalimbali. Baadhi ya njia hizo ni ruzuku kutoka Serikalini, michango ya wazazi au walezi, wanajumuiya pamoja na misaada kutoka kwa wadau wa maendeleo.

**Zoezi la 1**

1. Taja shughuli ulizowahi kushiriki katika kuleta maendeleo ya shule yako.
2. Eleza umuhimu wa kushiriki katika maendeleo ya shule yako.
3. Orodhesha njia tatu za kushiriki katika kuleta maendeleo ya shule yako tofauti na ulizozisoma.
4. Fafanua kwa mifano vitu vitano vinavyohitajika kwa maendeleo ya shule yako.
5. Ainisha vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya maendeleo ya shule yako.

FOR ONLINE USE ONLY

### Njia za kupata misaada ya kusaidia maendeleo ya shule

Uongozi wa shule unaweza kubuni njia mbalimbali za kutafuta misaada kutoka kwa wadau wa elimu. Jambo muhimu la kuzingatia katika kutafuta misaada au michango kutoka kwa wadau ni kufuata sheria, kanuni na taratibu. Zifuatazo ni baadhi ya njia zinazoweza kutumiwa na shule kupata misaada:



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 15 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) **Kadi za michango kwa wadau wa elimu:** Uongozi wa shule unaweza kuandaa kadi za michango na kuzitumia kuomba misaada kwa wadau mbalimbali wa elimu. Wadau wa shule ni pamoja na wazazi, viongozi wa Serikali katika ngazi za mitaa na Serikali kuu, taasisi binafsi, mashirika, wakulima na wafanyabiashara walioko jirani na shule. Wadau wengine muhimu kwa shule ni wale watu waliosoma zamani katika shule hiyo. Jambo la kuzingatia ni kwamba lazima Mwalimu Mkuu apate idhini ya kutafuta michango na misaada kutoka kwa viongozi wake.

(b) **Harambee:** Uongozi wa shule unaweza kuandaa harambee kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, ofisi au vyoo. Uongozi wa shule unaweza kualika viongozi wa Serikali, wafanyabiashara na viongozi wa dini ili washiriki kwenye harambee. Kupitia harambee hiyo, wageni waalikwa wanaweza kutoa misaada yao kwa njia ya fedha taslimu au vifaa kama mabati, nondo na saruji.

(c) **Mnada:** Shule inaweza kuandaa mnada wa vitu mbalimbali ambavyo vitauzwa kwa watu. Kwa mfano, shule inaweza kufanya mnada wa mazao kutokana na shughuli za kilimo shuleni. Mazao kama mahindi, maharage na mifugo kama kuku, bata, ng'ombe, mbuzi na kondoo vinaweza kuuzwa kwa mnada na kuipatia shule fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kila siku.

(d) **Chakula cha hisani:** Uongozi wa shule unaweza kukaribisha watu wenye nyadhifa mbalimbali kwenye jamii kama viongozi wa Serikali, asasi zisizo za kiserikali, wafanyabiashara, wakulima na wafugaji kwa chakula cha hisani. Baada ya kula chakula hicho, wageni hao hualikwa kuchangia fedha na mali kwa ajili ya kukamilisha jambo fulani. Kwa mfano, kukusanya fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za walimu au ununuzi wa samani za shule.

(e) **Wadau wa maendeleo ya elimu:** Uongozi wa shule unaweza kuwashawishi wadau wa maendeleo ya elimu au asasi zisizo za kiserikali ndani na nje ya nchi kutoa misaada mbalimbali kwa shule. Wadau wanaweza kutoa fedha, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, vitendea kazi kama vile tarakilishi, fotokopia na vifaa vya ujenzi. Baadhi ya shule nchini zimekuwa zikifadhiliwa na balozi za nchi mbalimbali kama Kanada, Swideni, Marekani, Uingereza pamoja na mashirika ya kitaifa na kimataifa.

(f) **Kuhamasisha watu kujitolea nguvukazi:** Uongozi wa shule au mwanafunzi kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa wanaweza kuandaa

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 16 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mkakati wa kuhamasisha wananchi kujitolea nguvukazi katika kufanya shughuli mbalimbali za shule. Wananchi wanaweza kuhamasika kujenga madarasa, maktaba, maabara, ofisi na vyoo kwa kujitolea nguvukazi.

**(g) Michango ya hiari:** Uongozi wa shule unaweza kukaribisha watu binafsi kutoa michango ya hiari ili kuisadia shule kumudu uendeshaji wa shughuli za maendeleo. Michango hii ya hiari inaweza kuwa fedha taslimu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, chakula, malazi, vifaa vya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule.

### Zoezi la 2

1. Orodhesha njia tano za kupata au kukusanya misaada kwa ajili ya maendeleo ya shule yako.
2. Taja misaada mitano inayoweza kutolewa na wadau mbalimbali wa elimu kwa shule yako.
3. Eleza kwa ufupi jinsi unavyoweza kushiriki kutoa misaada kwa shule yako.
4. Eleza maana ya chakula cha hisani.

### Kazi ya kufanya namba 1



Kwa kushirikiana na wanafunzi wenzako kwenye kikundi chunguza mazingira ya shule yako, kisha bainisha mambo matatu ambayo yanahitaji misaada. Buni njia zinazoweza kutumika kupata fedha kwa ajili ya kukamilisha mahitaji hayo.Wasilisha majibu yenu mbele ya darasa.

## Mpangokazi wa kujitolea ili kuiletea shule maendeleo

Mpangokazi wa kujitolea ni andiko lenye utaratibu maalumu wa jinsi ya kuratibu shughuli mbalimbali zinazofanyika bila malipo au kulazimishwa. Ili kuwapo ufanisi katika kazi za kujitolea, inashauriwa mwanafunzi awe na mpangokazi wa kujitolea kwa ajili ya maendeleo ya shule yake. Mpangokazi huu waweza kuwa wa muda mfupi, yaani mwezi mmoja hadi mwaka mmoja au muda mrefu wa miaka miwili na kuendelea.

Mpangokazi wa kujitolea unahusisha vipengele mbalimbali kama ifuatavyo:

**(a) Malengo:** Hili ni tamko la dhamira au dhumuni la kutekeleza jambo



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 17 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

fulani shuleni. Katika kipengele hiki, mwanafunzi atabainisha lengo analotaka kufikia. Kwa mfano, lengo linaweza kuwa; kuboresha mazingira ya shule kwa kupanda miti au kuwasaidia wanafunzi wenzake kufaulu vizuri mitihani.

(b) **Muda:** Hiki ni kipengele kinachoonesha wakati utakaotumika kufikia lengo lililokusudiwa katika kazi ya kujitolea. Muda unaweza kuwa saa, siku, wiki, mwezi au mwaka. Kwa mfano, unaweza kukadiria muda utakaotumia kuwasaidia wanafunzi wenzako ili wote mfaulu Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba.

(c) **Mahitaji:** Kipengele hiki hubainisha watu, vitu au vifaa vitakavyotumika kutekeleza lengo ulilojiwekea. Kwa mfano, kama unataka kutembelea wagonjwa waliolazwa hospitali, itabidi kuainisha vitu au vifaa utakavyohitaji kuwapelekea wagonjwa. Kuainisha mahitaji kutasaidia kubuni mkakati wa kupata watu au vitu vitakavyotumika kufikia lengo lililokusudiwa.

(d) **Utekelezaji:** Kipengele hiki huonesha namna utakavyotekeleza kwa vitendo shughuli za kujitolea. Kipengele hiki ni muhimu kwa kuwa hubainisha mkakati wa utekelezaji wa shughuli za kujitolea shuleni. Kwa mfano, ili kuboresha mazingira ya shule yako kwa kujitolea, utahitajika kubainisha kazi au shughuli utakazozifanya ndani ya muda fulani ili kufikia kusudio la kuwa na mazingira bora shuleni.

(e) **Tathmini:** Katika kipengele hiki mwanafunzi hupima ni kwa kiwango gani malengo yamefikiwa kulingana na rasilimali na muda uliopangwa. Tathmini huonesha mafanikio na upungufu na sababu zilizosababisha kutotekelezwa kwa kipengele fulani. Kwa mfano, kama ulipanga kuwasaidia wanafunzi wenzako kufaulu vizuri mitihani shuleni, utapima iwapo lengo limefikiwa ndani ya muda uliopangwa. Kumbuka, kuna tathmini endelevu, ambayo hufanyika wakati utekelezaji unaendelea, na tathmini tamati, ambayo hufanyika mwishoni.

Jedwali lifuatalo linaonesha sehemu za mpangokazi wa kujitolea.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Jedwali: Mpangokazi wa kuwasaidia wanafunzi kufaulu vizuri mitihani yao shuleni

| Na. | Malengo | Muda | Mahitaji | Utekelezaji | Tathmini |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kuinua ufaulu wa wanafunzi Darasa la Saba | Kufikia mwezi Mei mimi na wanafunzi wenzangu tufaulu na kupata alama A au B katika mitihani yote | a. Vitabu vya kiada<br>b. Vitabu vya rejea<br>c. Mitihani ya marudio ya miaka iliyopita<br>d. Muda wa ziada wa kujisomea<br>e. Vikundi shirikishi vya kujisomea | a. Kuomba au kuazima vitabu vya kiada au rejea<br>b. Wanafunzi kufanya majaribio kila wiki<br>c. Wanafunzi kufanya marudio ya mitihani ya miaka 10 iliyopita<br>d. Kusoma kwa bidii vitabu vya kiada na vya rejea | Je, wanafunzi niliowasaidia wamepata alama gani katika mtihani wa muhula? |

### Hatua za kuandaa mpangokazi wa kujitolea

Ili kuleta maendeleo shuleni kwa shughuli za kujitolea ni muhimu kuzingatia mambo yafuatayo:

(a) **Uchambuzi wa mahitaji:** Katika hatua hii, mwanafunzi huchambua mahitaji muhimu ili kufikia lengo alilokusudia. Kwa mfano, ili uweze kuwasaidia wanafunzi wenzako kufaulu vizuri mitihani, lazima uainishe mahitaji muhimu ya kuwawezesha wanafunzi kujifunza vizuri. Mahitaji muhimu yanaweza kuwa ni pamoja na vitabu, muda wa kutosha wa kujisomea, na mahali pa kusomea.

(b) **Ukusanyaji wa taarifa:** Mwanafunzi ili uweze kufikia lengo ulilokusudia utawajibika kukusanya taarifa mbalimbali kutoka kwa wanafunzi wenzako,

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 19 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

walimu na wafanyakazi wengine kuhusu namna ya kukabiliana na tatizo fulani shuleni. Kwa mfano, kama lengo lako ni kuwasaidia wenzako kufaulu mitihani, unaweza kukusanya taarifa zinazohusu wanafunzi wenye kuhitaji kusaidiwa na wale wenye uwezo ili uwashirikishe katika kufikia lengo lako.

(c) **Uandaaji wa rasimu ya mpangokazi:** Katika hatua hii, mwanafunzi huandaa andiko au mapendekezo ambayo yanaweza kurekebishwa au kukubaliwa na wanafunzi wenzake na watu wengine. Hatua hii hurasimisha mpangokazi wa kujitolea na hivyo kuwezesha kuanza matayarisho ya utekelezaji. Aghalabu, matayarisho ya utekelezaji yatahusisha wanafunzi, walimu na viranja watakaokuwa wamechaguliwa kushiriki kusaidia utekelezaji wa kazi za kujitolea zilizopangwa.

## Umuhimu wa mpangokazi

Mpangokazi husaidia kubainisha rasilimali zinazohitajika ili kutimiza lengo fulani. Kupitia mpangokazi, mwanafunzi huweza kuwa na ufanisi katika kutekeleza mikakati aliyojiwekea ili kufikia lengo lake. Ufanisi huongezeka kwani kila jambo huwa limebainishwa vyema.

Pia, mpangokazi husaidia kuratibu kazi zilizopangwa kufanyika kwa wakati na kwa ustadi wa hali ya juu. Hubainisha ni nani na kwa muda gani atahusika katika kazi fulani. Kwa mfano, kama lengo lilikuwa kulima mbogamboga shuleni, mpangokazi utaonesha watu watakaohusika kumsaidia mwanafunzi anayejitolea kulima bustani ya mbogamboga ikiwa ni pamoja na watakaohusika kumpatia vifaa kama majembe, mbolea na mbegu.

Vilevile, mpangokazi hurahisisha kufikia malengo yaliyowekwa kwa muda uliopangwa na kwa gharama nafuu. Aidha, kupitia mpangokazi, mwanafunzi atabaini kazi au shughuli za kutekeleza kulingana na vipaumbele vilivyowekwa. Mpangokazi husaidia kubaini ni jambo gani linapaswa kutekelezwa kabla ya jingine. Hali kadhalika, kupitia mpangokazi ni rahisi kutathmini mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa shughuli na malengo yaliyokusudiwa.

### Zoezi la 3

1. Nini maana ya mpangokazi wa kujitolea?



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 20 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Kwa kutumia mifano, fafanua vipengele vitano vya mpangokazi.
3. Eleza faida za kuwa na mpangokazi wa kujitolea shuleni.
4. Fafanua hatua tatu za kuandaa mpangokazi wa kujitolea.

### Kazi ya kufanya namba 2



Kwa kushirikiana na wanafunzi wenzako katika kikundi, andaa mpangokazi wa kujitolea wa miezi minne. Wasilisha darasani mpangokazi mlioandaa kwa majadiliano zaidi.

### Zoezi la 4

**A.** Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi.

1. Kuandaa mpangokazi wa kujitolea ni kupoteza muda. ________
2. Mwanafunzi anaweza kushiriki kuandaa na kutekeleza mpangokazi wa kujitolea. _________
3. Si muhimu kuainisha mpangilio wa matumizi ya rasilimali katika mpangokazi wa kujitolea.________
4. Vyakula, vifaa, maji, umeme na ardhi ni misaada inayoweza kuleta maendeleo shuleni. ________
5. Harambee haiwezi kuisaidia shule kupata au kukusanya misaada. _________

**B:** Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake kwenye kisanduku.

6. Kipi kati ya vitendo vifuatavyo ni kitendo cha kulinda mali za shule?
   (a) kutoa taarifa kwa uongozi wa shule pindi unapoona uharibifu wa mali za shule
   (b) kutupa takataka ovyo kwenye mazingira ya shule

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) kuacha umeme na maji kutumika wakati havihitajiki
(d) kutomtaja mwanafunzi mwenzako aliyevunja meza darasani

7. Lipi kati ya yafuatayo si msaada kwa shule?
   (a) vinywaji kama soda na pombe
   (b) chakula na sare za shule
   (c) vifaa vya kufundishia na kujifunzia
   (d) utoaji elimu shuleni

8. Ipi kati ya sentensi zifuatazo si kweli kuhusu faida za kuwa na mpangokazi?
   (a) husaidia kuwa na mpangilio mzuri wa matumizi ya rasilimali
   (b) hufanya suala la ufuatiliaji na tathmini kuwa gumu sana
   (c) huongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu
   (d) husaidia kuratibu kazi

9. Uchambuzi wa mahitaji kama hatua ya kuandaa mpangokazi huhusisha kuandaa kitu gani?
   (a) nyaraka za mpangokazi
   (b) sura za mpangokazi
   (c) tathmini ya malengo ya taasisi
   (d) kubainisha na kuandaa rasilimali zinazohitajika

10. Ni jinsi gani mpangokazi wa kujitolea husaidia kugawa majukumu shuleni?
   (a) kila mmoja hutambua na kutekeleza majukumu yake kutokana na mpangokazi
   (b) kila mtu kutekeleza mambo yake binafsi
   (c) kila mmoja kutekeleza kila jukumu lililo ndani ya mpangokazi kwa muda wake mwenyewe
   (d) kila mmoja ataamua ni kwa namna gani atatimiza majukumu bila kupangiwa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C:** Oanisha kipengele kutoka **Sehemu A** na maneno yaliyopo **Sehemu B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.

| Sehemu A | Jibu | Sehemu B |
|---|---|---|
| 11. Kuandaa na kutekeleza mpangokazi wa kujitolea | | (a) njia nyingine kwa wanafunzi kushiriki katika maendeleo ya shule yake |
| 12. Kushiriki kutoa mapendekezo kwa uongozi wa shule | | (b) kupima ili kubaini ni namna gani malengo yamefikiwa |
| 13. Misaada kwa shule | | (c) njia mojawapo ya wanafunzi kushiriki katika kuleta maendeleo ya shule |
| 14. Wafadhili | | (d) njia mojawapo ya kuchelewesha maendeleo ya shule |
| 15. Tathmini | | (e) taasisi au watu wanaosaidia taasisi na watu wenye uhitaji |
| | | (f) kutoa kompyuta kwa shule |
| | | (g) kubeza jamii na shule yako |

## Msamiati

Hisani — tabia ya kupenda kumtendea mema mtu

Mnada — tukio la kuuza na kununua vitu kwa kushindanisha bei

Rasimu — andiko la mwanzo kabisa la jambo fulani kabla ya kufanyiwa marekebisho na kukubaliwa kuwa rasmi

Siha — hali ya kuwa na afya bora



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 23 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu

## Kuipenda na kujivunia nchi yako

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza ujumbe uliomo katika kaulimbiu na wimbo wa shule, matendo yanayoiletea sifa shule na njia za kuitangaza shule yako. Pia, ulijifunza kuipenda, kuitangaza na kubaini njia mbalimbali za kuitangaza nchi yako. Katika sura hii, utajifunza jinsi ya kushiriki katika kuhamasisha na kudumisha amani katika jamii yako. Aidha, utaweza kushiriki katika vitendo vya kulinda uhuru na umoja wa Taifa letu la Tanzania na kutenda vitendo vya kuthamini utu katika jamii. Maarifa na ujuzi utakaopata utakuwezesha kuwa mzalendo kwa nchi yako.*



**Fikiri**

Hali inavyokuwa katika nchi isiyokuwa na amani.

### Kudumisha amani katika jamii

Amani ni hali ya utulivu na usalama, isiyokuwa na ghasia, fujo au vita. Amani katika jamii huweka misingi imara ya kulinda usalama wa raia na mali zao na kudumisha utulivu kwa kuepuka ghasia, fujo au vita. Ili kudumisha amani, wananchi hawana budi kutii sheria, kulinda mipaka ya nchi, kuheshimu haki za binadamu, kukemea vitendo viovu, na kujenga uhusiano mwema na watu na mataifa mengine.

Kutii sheria ni kuheshimu kanuni na taratibu zilizowekwa na mamlaka zinazohusika bila kulazimishwa. Utii wa sheria husaidia kudumisha amani kwa sababu unaondoa migogoro na misuguano miongoni mwa wananchi au kati ya wananchi na Serikali. Hivyo, sheria zimewekwa ili kuongoza matendo ya watu katika maisha yao ya kila siku.

Ulinzi wa mipaka ya nchi yetu ni jukumu la kila mwananchi kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama. Kila mwananchi analo jukumu la kutoa taarifa



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 24 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kwa vyombo vya dola endapo ataona vitendo vinavyohatarisha usalama wa mipaka ya nchi. Baadhi ya vitendo hivyo ni pamoja na utoroshaji wa rasilimali za nchi kupitia mipaka ya nchi, uingizaji wa raia wa nchi zingine bila kufuata utaratibu, na biashara za magendo mipakani.

Amani katika jamii inaweza kudumishwa kwa kuheshimu haki za msingi za binadamu kama vile, haki ya kuishi na kupata mahitaji muhimu kama chakula, malazi, mavazi, elimu, ulinzi na usalama wa mtu na mali zake. Pia, haki nyingine za msingi ni kushiriki katika mambo ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

Vilevile, amani na usalama wa nchi yetu unaweza kudumishwa kwa kuhakikisha kuwa kuna uhusiano mwema kati ya nchi yetu na mataifa mengine. Uhusiano mwema na nchi jirani huanza kwa wananchi wanaoishi mpakani mwa nchi zinazohusika kutii sheria na taratibu za kila nchi. Uhusiano mwema na nchi nyingine huwezesha kuepuka migogoro, ugomvi na vita. Hali hii itawezesha nchi yetu kudumisha amani na usalama.

Katika kila jamii kuna watu ambao huwa na mwelekeo hasi katika kudumisha amani. Kwa mfano, kuwapo kwa watu wachache wanaovunja sheria kama vile, kufanya vitendo vya wizi na ubadhirifu. Hivyo, jamii haina budi kukemea mwenendo huu mbaya ili usiathiri amani na usalama wa jamii na nchi kwa ujumla.

## Njia za kuhamasisha jamii kudumisha amani

Amani ni moja ya tunu adhimu za Taifa letu. Kuna njia mbalimbali za kuhamasisha jamii kudumisha amani ikiwa ni pamoja na kutumia kazi za sanaa, michezo, mitandao ya kijamii, siku ya amani, mahubiri na mihadhara ya dini. Kwa kutumia njia hizi, ujumbe kuhusu umuhimu wa amani na madhara ya kutokuwa na amani huwafikia watu kwa urahisi.

Ngonjera, mashairi na michezo ya kuigiza hutumiwa katika kuelimisha umma kupitia matamasha mbalimbali hasa wakati wa sikukuu za kitaifa kama vile, tarehe 9 Disemba, ambayo ni Sikukuu ya Uhuru; tarehe 26 Aprili, ambayo ni Sikukuu ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar; au tarehe 12, Januari ambayo ni Sikukuu ya Mapinduzi ya Zanzibar, tarehe 1 Mei, ambayo ni Sikukuu ya Wafanyakazi; na tarehe 8 Agosti, ambayo ni Sikukuu ya Wakulima. Sikukuu hizi zinaweza kutumika kama majukwaa ya

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 25 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuhamasisha jamii kulinda amani kupitia vyombo vya habari kama vile redio, televisheni, na magazeti.

Pia, michezo mbalimbali kama mpira wa miguu, mpira wa kikapu, mpira wa wavu, na mpira wa pete na riadha ni mbinu bora za kuhamasisha jamii kudumisha amani ya nchi yetu. Michezo hii hujenga uhusiano mwema na kukuza urafiki miongoni mwa watu na pia kati ya jamii moja na nyingine.

Matumizi bora ya mitandao ya kijamii kama "Facebook", "WhatsApp", "Instagram" na "Twitter" ni njia nyingine ya kutoa elimu ya kudumisha amani. Njia hizi huwezesha jamii kushirikiana na hata kujadiliana namna ya kudumisha amani katika jamii. Aidha, njia hizi husaidia kusambaza habari kwa haraka na hivyo huweza kusaidia kuepusha uvunjifu wa amani katika jamii.

Pia, nchi yetu inaweza kutumia tarehe 21 Septemba, siku ambayo imetangazwa na Umoja wa Mataifa kuwa siku ya amani duniani ili kuelimisha na kuhamasisha jamii kudumisha amani nchini. Katika siku hii, masuala mbalimbali kuhusu udumishaji wa amani yanaweza kuwasilishwa na kujadiliwa kupitia mikutano, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Hali kadhalika, madhehebu ya dini yana fursa kubwa katika kudumisha amani ya nchi kwa kutumia mahubiri na mawaidha kwa waumini wao. Waumini huhubiriwa umuhimu wa amani kama msingi mkuu unaowawezesha kuabudu kwa uhuru na utulivu. Kwa kutumia mahubiri na mawaidha, upendo na amani huimarika miongoni mwa wanajamii.

### Umuhimu wa kudumisha amani katika jamii

Amani ina umuhimu mkubwa katika ustawi wa jamii. Jamii yenye amani huwa na nafasi ya kushiriki vizuri katika shughuli za uzalishaji mali. Shughuli hizi za uzalishaji mali huongeza kipato na kuondoa umaskini kwa wananchi. Kwa hiyo amani ni msingi wa maendeleo ya kiuchumi.

Amani inapotawala katika jamii huwapa wanajamii fursa ya kutumia rasilimali wanazomiliki kwa manufaa ya wote. Mahali penye amani watu huweza kujenga makazi ya kudumu, kusomesha watoto na kujitafutia kipato kwa njia mbalimbali. Jamii yenye amani hujenga umoja na mshikamano. Amani huifanya jamii kushirikiana na kusaidiana katika masuala mbalimbali ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 26 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Angalia Kielelezo namba 1, kisha jibu maswali yanayofuata.




**Kielelezo namba 1:** *Vitendo vya kuhamasisha amani katika jamii*

## Zoezi la 1

1. Kwa kutumia Kielelezo namba 1, eleza kwa kifupi uhusiano uliopo kati ya amani na nchi ya uchumi wa viwanda.
2. Kwa kutumia Kielelezo namba 1 fafanua ujumbe unaosema "usawa wa jinsia na amani".
3. Je, umejifunza nini katika Kielelezo namba 1?

### Kazi ya kufanya namba 1

Fanya uchunguzi katika jamii inayokuzunguka, kisha bainisha mbinu wanazotumia kulinda amani. Wasilisha darasani kwa majadiliano zaidi.



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 27 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kuthamini utu

Kuthamini utu ni kuwajali na kuwathamini binadamu kwa kuhakikisha kuwa hawapati mateso yoyote yasiyo ya lazima. Binadamu anayethamini utu huwa na upendo, huheshimu watu wengine na kutowavunjia haki na heshima yao.

### Umuhimu wa kuthamini utu

Katika maisha ya kila siku na katika mazingira yetu tuna watu wa aina na jinsi tofauti wanaotuzunguka. Watu hawa, wanahitaji matendo ya utu, hususan kuheshimiwa na kuthaminiwa utu wao.

Binadamu akioneshwa upendo wa kweli kwa kuthamini mahitaji yake muhimu kama vile chakula, malazi, mavazi na elimu, naye hujenga tabia ya upendo na kuheshimu utu wa watu wengine. Hali hii humwezesha kukuza mshikamano na watu wengine kwa sababu atajiona anathaminiwa katika jamii inayomzunguka na anapendwa kutokana na kutendewa matendo yenye kuthamini utu.

Haki za binadamu ndiyo msingi wa kujenga na kudumisha utu wa binadamu. Haki za binadamu zinaweza kugawanywa kwenye makundi manne ambayo ni haki za kisiasa, kijamii, kiuchumi, na kiutamaduni. Udumishaji wa haki za binadamu husaidia kuthamini utu kwa sababu haki za binadamu ndiyo mwongozo wa jinsi ya kuhusiana na binadamu wengine tofauti na jinsi tunavyohusiana na viumbe wengine.

Aidha, mtu anapothaminiwa utu wake katika jamii humfanya ajione ana wajibu mkubwa wa kutimiza katika jamii yake. Hali hii humfanya ajitoe kwa moyo wake wote kuitumikia, kuitetea na kuilinda jamii yake na pia kuiletea maendeleo. Hali kadhalika, mtu akiheshimiwa katika jamii humfanya aishi kwa amani na utulivu katika jamii yake.

### Vitendo vya kuthamini utu

Mwanzo wa kuthamini utu ni kujiheshimu. Kujiheshimu ni hali ya kutambua thamani ya utu ambayo humwezesha mtu kuvaa mavazi ya heshima na kuepuka vitendo viovu. Vitendo hivyo viovu ni kama vile ukahaba, utumiaji mihadarati na lugha ya matusi. Aidha, kila binadamu hana budi kuheshimu binadamu wenzake kwa kuthamini nafasi zao katika jamii. Nafasi hizo ni kama vile; wazazi, walezi, viongozi na watu wa umri mdogo na mkubwa. Watoto na vijana wanapaswa kuwaheshimu wazazi na watu wengine wenye umri unaowazidi kwa kuwasalimia na kuonesha utii kwao. Kuonesha na kutunza

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 28 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

heshima ni kitendo cha kuthamini utu.

Kupenda watu wengine na kuwajali katika hali zao, pia ni kitendo cha kuonesha utu. Kuonesha matendo kama vile kuwavusha barabara watoto wadogo katika barabara zenye msongamano wa magari na kuwapokea mizigo wazee ni vitendo vya upendo. Pia, kusaidia wazazi na majirani katika kazi za nyumbani na kuwahudumia wagonjwa na wenye uhitaji wa aina mbalimbali ni vitendo vinavyoonesha upendo na kujali utu. Hivyo, kutoa misaada ni kitendo kimojawapo cha kuthamini utu.

Aidha, mtu anayezingatia bidii na maadili katika kazi zake, atakuwa akidumisha utu wake katika jamii anamoishi au kufanya kazi. Kazi ni kipimo cha utu. Tendo jingine muhimu la kuthamini utu ni kujisitiri na kuwasitiri wengine kwa kauli njema au kutunza siri za watu wengine. Kwa mfano, kama ndugu au rafiki yako anakabiliwa na changamoto mbalimbali za kijamii na asingependa taarifa hiyo ijulikane kwa wengine, huna budi kumsaidia kwa kutunza siri hiyo.

**Zoezi la 2**

1. Eleza kwanini kutoa misaada kwa watu au taasisi ni kitendo cha kuthamini utu.
2. Je, kwa namna gani kuishi kwa kuzingatia maadili kunawezesha kuthamini utu?
3. Kwanini haki za binadamu ni nguzo muhimu katika kuthamini utu?
4. Eleza njia tano zinazoonesha kuthamini utu katika jamii.

**Kazi ya kufanya namba 2**



Kwa kushirikiana na wanafunzi wenzako katika kikundi, fanya majadiliano kuhusu vitendo vya kuthamini utu katika jamii unamoishi. Kisha, andika majibu mliyopata katika daftari lako la mazoezi.

### Uhuru na umoja wa Taifa letu

Uhuru wa taifa ni hali ya taifa moja kutotawaliwa na mtu au nchi nyingine kiuchumi, kisiasa na kijamii. Taifa lililo huru huwa na uwezo wa kufanya uamuzi wake bila kuingiliwa na taifa jingine. Uhuru wa taifa ni muhimu sana



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 29 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

katika kutekeleza mipango ya muda mfupi na muda mrefu katika masuala ya kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii. Tanzania ni Taifa huru linaloundwa na muungano wa nchi mbili, Tanganyika na Zanzibar zilizoungana mwaka 1964.

Umoja wa kitaifa ni hali ya watu wa taifa moja kuwa na ushirikiano na mshikamano katika mambo mbalimbali kama vile kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa. Pia, umoja wa kitaifa ni hali ya wananchi kuwa na msimamo mmoja kuhusu jambo au mambo yanayolihusu taifa lao. Umoja wa kitaifa ni nguzo muhimu kwani taifa lisilo na umoja hushindwa kujiletea maendeleo kutokana na kukosekana kwa nguvu ya pamoja katika kutekeleza mipango yake ya maendeleo. Tanzania ni kati ya mataifa yenye umoja imara barani Afrika kwa kuwa lina mshikamano imara na limeweza kupata maendeleo makubwa katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni.

Ulinzi wa Taifa huhitaji umoja wa wananchi wote. Kila mwananchi ana jukumu la kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama katika kulinda uhuru na umoja wa Taifa letu.

### Umuhimu wa kulinda uhuru na umoja wa Taifa

Nchi yenye uhuru na umoja hupata maendeleo haraka. Pia, nchi yenye uhuru na umoja hupata faida kubwa ya kuwa na nguvu ya pamoja katika masuala ya kitaifa katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Aidha, uhuru na umoja hudumisha amani katika taifa, na husaidia taifa kutekeleza mipango yake kwa mafanikio kutokana na ushiriki na uungwaji mkono wa wananchi katika malengo yanayotakiwa kufikiwa.

Nchi yenye uhuru na umoja hudumisha ulinzi na usalama wa watu na mali zao. Nchi inapokuwa huru, inakuwa na amani na salama ndani ya mipaka yake hivyo watu wake hupata muda wa kutekeleza mipango yao ya kiuchumi, kijamii na kisiasa bila kuwa na hofu ya kuingiliwa na yeyote.

Ushirikiano na mshikamano wa wananchi husaidia kufanya kazi kwa bidii ili kuwezesha nchi istawi. Hali hii huharakisha maendeleo ya nchi kwa kuwa kila mtu huona anastahili kuwajibika kwa ajili ya kuleta maendeleo binafsi na Taifa kwa ujumla. “Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu”.

### Vitendo vya kulinda uhuru na umoja wa Taifa

Kila taifa linatakiwa kufanya jitihada kuhakikisha uhuru na umoja wake



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

vinalindwa. Jambo hili linaweza kutimizwa ikiwa Serikali na wananchi kwa pamoja watafanya yafuatayo:

**(a)** **Kutii sheria:** Kila taifa lina sheria zake kwa mujibu wa katiba, ni lazima lihakikishe watu wake wanazifuata. Utii wa sheria, kanuni na taratibu katika nchi huondoa uwezekano wa kuibuka machafuko yanayoweza kupoteza amani ya nchi na hivyo watu wake kukosa umoja wao. Wananchi wa taifa fulani wanapotii sheria, kanuni na taratibu za nchi, amani na mshikamano katika taifa hutamalaki.

**(b)** **Kulinda mipaka ya nchi:** Ili nchi iweze kulinda uhuru na umoja wake ni lazima kulinda mipaka yake dhidi ya maadui kutoka nje. Maadui hawa ni kama wahamiaji haramu, vikundi vya kigaidi na kijasusi. Kuwapo kwa makundi haya huweza kuvuruga umoja na uhuru wa nchi. Kwa mfano, nchi ya Tanzania inasifika kwa amani na umoja wa kitaifa kutokana na kazi kubwa ya kulinda mipaka yake dhidi ya maadui. Jeshi la Wananchi wa Tanzania limepewa jukumu la kulinda mipaka ya nchi yetu. Hata hivyo, kila mwananchi ana wajibu wa kulinda mipaka ya nchi yetu na mali zake.

**(c)** **Kuheshimu haki za binadamu:** Taifa linaloheshimu haki za binadamu ni rahisi kulinda uhuru na umoja wa watu wake. Hii ni kwa sababu haki za binadamu zinapolindwa husaidia watu kuishi katika taifa lao kwa uhuru na amani. Kuheshimu haki za binadamu husaidia wananchi kujivunia na kuipenda nchi yao. Vilevile, huondoa migogoro inayoweza kusababisha uvunjifu wa amani na kuharibu umoja wa kitaifa. Wananchi wasipopata haki zao, huichukia nchi yao na hii ni hatari kwa uhuru na umoja wa kitaifa.

**(d)** **Kukemea vitendo viovu kwa wakati:** Ili nchi iweze kuendelea kulinda uhuru na umoja wa taifa lake ni muhimu kuwa na tabia ya kukemea vitendo viovu kama wizi, unyang'anyi, rushwa, uchochezi wa kisiasa na kikabila na vitendo vya kutotii sheria. Serikali haina budi kupiga marufuku vitendo hivyo na kuvikemea mara kwa mara ili kuhakikisha amani na mshikamano miongoni mwa wananchi vinadumishwa.

**(e)** **Kujenga uhusiano mwema na mataifa mengine:** Uhusiano mzuri na mataifa mengine huwezesha nchi kuwa na mipango ya pamoja katika uzalishaji mali, huduma za kijamii kama elimu na afya, usafirishaji, ulinzi na usalama. Kwa mfano, nchi ya Tanzania na nchi nyingine zilizo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, zinashirikiana katika kukomesha matendo ya kihalifu katika nchi zao. Kama mtu atafanya uhalifu nchini Tanzania na kukimbilia nchini Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi au Sudani Kusini, bado vyombo vya usalama katika nchi hizo huendelea kumsaka mtuhumiwa na endapo atakamatwa, atarudishwa nchini ili



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 31 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ashitakiwe kwa mujibu wa sheria.

## Zoezi la 3

1. Tofautisha dhana ya uhuru wa Taifa na umoja wa kitaifa.
2. Taja faida za kudumisha uhuru wa nchi yetu na umoja wa Taifa.
3. Ni kwa namna gani ulinzi wa mipaka ya nchi husaidia kulinda uhuru na umoja wa kitaifa?

### Kazi ya kufanya namba 3

Katika mazingira ya jamii yako, bainisha mambo mawili ambayo yanaweza kusababisha kupoteza uhuru na umoja katika jamii yako. Andika hatua unazoweza kuchukua kudhibiti mambo hayo ili yasilete madhara zaidi.

## Zoezi la 4

**A:** Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi.

1. Amani ni hali ya uhasama baina ya mtu na mtu au jamii na jamii nyingine.__________
2. Kutii sheria bila shuruti ni mojawapo ya vitendo vya kudumisha amani katika jamii._______
3. Mitandao ya kijamii inaweza kutumika kama njia mojawapo ya kuhamasisha amani katika jamii._________
4. Kuthamini utu ni hali ya kutoheshimu mtu mwingine.__________
5. Kutenda haki ni mojawapo ya vitendo vya kuthamini utu.___________

**B:** Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake kwenye kisanduku.

6. Lipi kati ya yafuatayo ni kitendo kisicho cha kudumisha amani katika jamii?
   (a) kutii sheria bila shuruti

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 32 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) kukemea vitendo viovu
(c) kulinda mipaka ya nchi
(d) kutotumia mitandao ya kijamii kulingana na sheria

7. Kati ya vitendo vifuatavyo kimojawapo si kitendo cha kusaidia kuhamasisha amani kwenye jamii.
(a) kubishana na majirani zako
(b) kutumia mitandao ya kijamii kupinga ubaguzi
(c) kutumia mikutano na semina kujadili umoja
(d) kuandaa kisamafunzo na ngonjera kuhamasisha upendo katika jamii

8. Kujisitiri na kuwasitiri wengine vinasaidiaje jamii?
(a) kuhamasisha amani katika jamii
(b) kuthamini utu
(c) kutokujipenda sana
(d) kujipenda kwanza na wengine baadaye

9. Kutenda haki husaidia kulinda uhuru na umoja wa Taifa kwa sababu gani?
(a) viongozi wa nchi hutoa maagizo
(b) watu huwa na uhuru wa kufanya lolote walipendalo
(c) raia huwa huru kufanya ugaidi
(d) wananchi huipenda nchi yao

10. Jukumu la kulinda uhuru na umoja wa Taifa letu ni jukumu la nani?
(a) usalama wa Taifa tu
(b) polisi tu
(c) idara ya uhamiaji tu
(d) kila mwananchi

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 33 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C:** Oanisha kipengele kutoka **Sehemu A** na maneno yaliyopo **Sehemu B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.

| Sehemu A | Jibu | Sehemu B |
|---|---|---|
| 11. Utu | | (a) kuwa na nguvu ya pamoja katika masuala ya kitaifa |
| 12. Umuhimu wa amani katika jamii | | (b) hali ya kuwa na tabia zisizo za kibinadamu |
| 13. Kuwa na umoja wa kitaifa | | (c) huduma za uhuru wa mawazo |
| 14. Kuheshimu haki za binadamu | | (d) Taifa kugawanyika |
| 15. Kutoa msaada kwa watu au taasisi | | (e) huchochea maendeleo katika jamii |
| | | (f) kitendo cha kuthamini utu |
| | | (g) vitendo vya kulinda uhuru na umoja wa Taifa |
| | | (h) hali ya kuwa na tabia nzuri ya kibinadamu |

### Msamiati

Adhimu — kitu chenye ubora wa pekee, chenye maana na umuhimu

Mihadarati — dawa za kulevya

Shuruti — lazima, bila hiyari

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 34 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

## Kujijali na kuwajali wenzetu

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza kutenda vitendo vinavyowavutia wenzako na kujiepusha na tabia hatarishi. Pia, ulijifunza umuhimu wa kuomba unasihi kila unapohitajika. Vilevile, ulijifunza umuhimu wa kuwatanguliza watu wenye uhitaji wa haraka kupata huduma na kutenda vitendo vinavyoonesha usawa. Katika sura hii, utajifunza kuhusu elimu ya afya ya uzazi pamoja na umuhimu wake. Pia, utajifunza njia za kutoa elimu ya afya ya uzazi. Vilevile, utajifunza namna ya kutoa elimu ya zimamoto na uokoaji katika jamii. Maarifa na ujuzi utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kujiepusha na tabia hatarishi zinazoathiri afya ya uzazi. Vilevile, utakuwezesha kutoa elimu kuhusu majanga ya moto na uokoaji wa waathirika wa majanga hayo katika jamii.*



**Fikiri**

Umuhimu wa elimu ya:

(a) afya ya uzazi; na

(b) zimamoto na uokoaji.

### Elimu ya afya ya uzazi

Afya ya uzazi ni hali ya ustawi wa mwili, akili na mahusiano ya jamii katika mambo yote yanayohusiana na mfumo wa uzazi kwa wanawake na wanaume. Afya ya uzazi inahusisha mfumo wa uzazi, ukuaji na balehe, ujauzito, masuala ya hedhi, uzazi wa mpango na magonjwa ya ngono. Elimu ya afya ya uzazi ni mafunzo yanayotolewa kuhusu masuala hayo ili kuwezesha walengwa kupata taarifa sahihi kuhusiana na afya ya uzazi. Elimu hii husaidia vijana wa kike na wa kiume kuhimili mihemko ya miili yao, kufanya uamuzi sahihi na kujiandaa kuwa wazazi bora katika jamii wanamoishi.

### Njia za kutoa elimu ya afya ya uzazi

Elimu ya afya ya uzazi hutolewa kwa njia mbalimbali katika jamii. Baadhi ya njia hizo ni pamoja na:

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 35 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) **Ufundishaji ndani na nje ya darasa:** Elimu ya afya ya uzazi hufundishwa darasani kupitia masomo mbalimbali. Mfano wa mada za afya ya uzazi zinazofundishwa darasani ni kama vile usafi wa mwili, via vya uzazi, mfumo wa uzazi na magonjwa ya ngono. Pia, elimu hii huweza kutolewa nje ya darasa kwa kualika mtaalamu wa afya kutoa elimu hiyo kwa wanafunzi wote shuleni. Vilevile, elimu hii huweza kutolewa shuleni kwa kutumia klabu za masuala mtambuka yakiwemo VVU na UKIMWI, rushwa, haki za mtoto, jinsia na shughuli za kundirika shuleni.

(b) **Vipeperushi na majarida:** Katika kuwafikishia walengwa elimu ya afya ya uzazi, vipeperushi na majarida hutumika kama nyenzo muhimu. Majarida na vipeperushi hivyo hutumika kutoa ujumbe maalumu unaokusudiwa kuwafikia walengwa. Kwa mfano, kipeperushi kinaweza kuwa na ujumbe ufuatao "Mimba za utotoni ni hatari kwa uhai wa mtoto, mkinge mwanao!" au "mkunje mbichi" "usisubiri avunje ungo, wabakaji hawasubiri". Vipeperushi hivi na majarida yenye picha na ujumbe hulenga kuwapa wahusika uelewa juu ya madhara ya mimba za utotoni na maambukizi ya magonjwa ya ngono.

(c) **Sanaa za maonesho:** Sanaa za maonesho kama vile ngoma, nyimbo, maigizo na ngonjera huwavutia zaidi vijana, hivyo kuwafikishia ujumbe uliokusudiwa kwa ukamilifu.

(d) **Semina na makongamano:** Semina na makongamano hutumika kuwakutanisha walengwa ili kuwaelimisha kuhusu afya ya uzazi. Wataalamu wa masuala ya afya ya uzazi hutumika kutoa mada mahususi juu ya masuala hayo. Walengwa wakuu ambao ni vijana hunufaika na elimu hii.

(e) **Mafundisho ya dini:** Viongozi wa dini wana nafasi kubwa ya kukutana na vijana na kuwapa mafundisho juu ya afya ya uzazi. Kwa kuwa kuna vijana wengi kwenye madhehebu ya dini, inakuwa rahisi kuwafikia na kuwapa elimu ya afya ya uzazi. Kwa mfano, kuelimishwa kuhusu mwenendo mwema, mahusiano, na afya ya uzazi.

(f) **Vyombo vya habari:** Vyombo vya habari hutumika katika mawasiliano na upashanaji habari. Vyombo hivyo ni redio, magazeti na televisheni. Vyombo vya habari vina wajibu mkubwa katika utoaji wa elimu ya afya ya uzazi kwa vijana. Vyombo hivi huandaa na kurusha vipindi na kutoa makala kuhusu elimu ya afya ya uzazi kwa vijana.

### Umuhimu wa elimu ya afya ya uzazi

Ni muhimu kwa vijana kupewa elimu ya afya ya uzazi. Hii huwasaidia kuepuka



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 36 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

athari za kiafya. Pia, itawawezesha kupata uelewa wa kutosha ili kukabiliana na mabadiliko ya mwili wakati wa balehe na kumudu shinikizo kutoka kwa kundirika. Mabadiliko ya mwili na shinikizo rika huweza kusababisha vijana kufanya uamuzi usio sahihi na hatimaye kuathirika kimwili, kiakili na kisaikolojia. Kwa mfano, huweza kusababisha kujihusisha na tabia za wizi, ulevi na uasherati. Vitendo hivi vinaweza kusababisha athari za kiafya, kiuchumi na kutofikia malengo ya maisha yaliyotarajiwa.

Kwa kupitia elimu hii, vijana huongeza uelewa kuhusu haki za binadamu, jinsi na jinsia, mahusiano, na haki za afya ya uzazi. Pia, elimu hii inaweza kusaidia kupunguza au kuondoa kabisa mimba za utotoni na ndoa katika umri mdogo. Vilevile, elimu hii huchangia kuleta mabadiliko ya tabia na mienendo isiyofaa kwa vijana. Hii huwawezesha kujenga mwelekeo chanya katika maisha ya kila siku na kuzingatia maadili. Aidha, itawawezesha kujiepusha na vitendo hatarishi vinavyochangia maambukizi ya magonjwa ya ngono.

**Zoezi la 1**

1. Eleza maana ya afya ya uzazi.
2. Fafanua umuhimu wa elimu ya afya ya uzazi kwa vijana.
3. Elezea namna vyombo vya habari vinavyoweza kusaidia vijana kupata elimu ya afya ya uzazi.

**Kazi ya kufanya namba 1**

Tunga shairi lenye beti 5 kuhamasisha utoaji wa elimu ya afya ya uzazi kwa vijana. Andika shairi hilo katika daftari lako la mazoezi.

### Elimu ya zimamoto na uokoaji katika jamii

Elimu ya zimamoto na uokoaji ni muhimu kutolewa kwa wanajamii ili kuweza kukabiliana na majanga ya moto katika mazingira yao. Zimamoto ni jumla ya vitendo vyote vinavyozuia moto usiendelee kuwaka mahali usipotakiwa. Uokoaji ni kitendo cha kutoa au kusaidia watu, wanyama, majengo na vifaa vingine visiendelee kuteketea kwa moto.

Zimamoto na uokoaji ni mchakato unaoshirikisha wadau mbalimbali katika



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 37 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kukabiliana na majanga ya moto yanayotokea katika mazingira yetu. Mchakato huo unahusisha uokoaji wa watu na mali zilizopo kwenye eneo la janga la moto. Katika nchi yetu, taasisi za kiserikali na binafsi hushiriki katika zimamoto na uokoaji pale majanga hayo yanapotokea. Taasisi iliyopewa kazi ya kuratibu shughuli za zimamoto na uokoaji ni Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Jeshi hili lilianzishwa kwa sheria ya Bunge namba 14 ya mwaka 2007.

### Umuhimu wa elimu ya zimamoto na uokoaji katika jamii

Ili kupunguza madhara ya moto ni muhimu jamii kupata elimu sahihi ya matumizi ya moto. Wananchi watakapopata elimu hii wataweza kutengeneza mazingira ambayo itakuwa vigumu kwa moto kutokea na kusambaa. Umuhimu wa elimu ya zimamoto na uokoaji ni kama ifuatavyo:

(a) **Kuwajengea wananchi uwezo wa kujikinga na majanga yatokanayo na moto:** Utoaji wa elimu ya zimamoto na uokoaji ni nyenzo muhimu katika kupunguza majanga ya moto. Elimu ya zimamoto na uokoaji huwajengea wananchi maarifa na ujasiri wa kukabiliana na majanga haya. Katika elimu ya zimamoto, mada zinazohusu visababishi vya majanga ya moto na namna ya kujiokoa na madhara ya moto hutolewa.

(b) **Kuwajengea watu tabia ya kujihami dhidi ya majanga ya moto:** Katika utoaji wa elimu ya zimamoto na uokoaji watu hufundishwa mbinu za kuzuia, kujiokoa, na kushirikiana na wataalamu wa zimamoto ili kurahisisha utoaji wa huduma. Nguvukazi ya zimamoto huongezeka watu wanapokuwa wamejengewa uwezo na kupewa nyenzo za kuzimia moto. Elimu inayotolewa huwaongezea tabia ya kujiamini na kuweza kushiriki ipasavyo katika matukio ya kuzima moto na uokoaji.

(c) **Kuongeza watu wenye ujuzi wa kukabiliana na majanga ya moto:** Moto huwa na nguvu na huweza kuongezeka kwa haraka. Juhudi za kuzima moto huhitaji ushirikiano wa watu wengi. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaweza likawa na vifaa lakini lisiwe na idadi ya kutosha ya askari. Hivyo, elimu husaidia kuongezeka kwa nguvukazi ya kukabiliana na majanga ya moto.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 38 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Angalia Kielelezo namba 1, kisha tafakari shughuli inayofanyika.




**Kielelezo namba 1:** *Shughuli za kuzima moto*

## Vifaa vya zimamoto na uokoaji

Katika kukabiliana na majanga mbalimbali ya moto, taasisi na wataalamu mahususi wamebuni vifaa mbalimbali vya kutumia katika kuzima moto. Kila kifaa kina namna ya kukitumia kwa ustadi ili kilete matokeo chanya kwenye shughuli au kazi ya kuzima moto. Baadhi ya vifaa hivyo ni pamoja na:

(a) **Ndoo zenye mchanga mkavu**: Hizi ni ndoo ambazo hupakwa rangi nyekundu na hutumika kuhifadhi mchanga wa kuzimia moto. Moto unapotokea, chukua ndoo yenye mchanga au kama haipo chukua kifaa uchote mchanga kwa haraka, kisha mwaga mchanga huo kwenye moto ili kuuzima.



**Kielelezo namba 2:** *Ndoo za rangi nyekundu zenye mchanga mkavu*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) **Gari la kuzima moto:** Hili ni gari maalumu lililoundwa kwa ajili ya kubeba maji na kemikali ya kuzimia moto. Gari la kuzima moto ni mojawapo ya vifaa muhimu na lina uwezo mkubwa wa kuzima moto. Limeundwa katika muundo wenye kuweza kumwaga maji mbali na kwa msukumo mkubwa. Askari wa zimamoto hufika na gari likiwa na maji katika eneo lililopata janga. Katika hatua za awali baada ya kujiridhisha hakuna nyaya zinazopitisha umeme, wataalamu huegesha gari mahali sahihi na kuanza kukunjua mipira ya maji. Askari wa zimamoto huelekeza mipira inayotoa maji kwenye moto ili kuuzima.





**Kielelezo namba 3**: *Gari la kuzima moto*

(c) **Mtungi wa kuzima moto:** Huu ni mtungi uliowekwa kemikali maalumu za kuzimia moto. Mitungi hii huwekwa kwenye vyombo vya usafiri, majengo ya umma, watu binafsi na biashara. Mtungi huu hutumika wakati majanga ya moto yanapotokea. Mtungi huu hutumika kwa kufuata hatua zifuatazo: Ondoa kamba ya usalama iliyofungwa kwenye mikono ya mtungi kisha chomoa pini iliyochomekwa kwenye mkono wa juu wa mtungi, halafu elekeza tundu la kutolea kizimamoto kwenye kitako cha moto.



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 40 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Kielelezo namba 4:** *Mtungi wa kemikali ya kuzimia moto*

(d) **Blanketi:** Hili ni blanketi maalumu ambalo hutumika kama kifaa cha kuzimia moto. Blanketi hili hutumika kuzima moto kwa kumfunika mtu anayeungua. Iwapo huna blanketi hili maalumu, unashauriwa kutumia blanketi la kawaida ambalo kabla ya kulitumia unalilowesha maji na baadaye unalitumia.




**Kielelezo namba 5:** *Blanketi la kuzimia moto*

(e) **Machela:** Hiki ni aina ya kitanda ambacho hutumika kuwabeba watu walioathirika na majanga ya moto kwenye harakati za kuwaokoa.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Waokoaji huwabeba majeruhi wakiwa wamelazwa kwenye machela hiyo. Pia, kiti, ngazi au blanketi vinaweza kutumika kubeba majeruhi.



**Kielelezo namba 6:** *Machela ya kubeba majeruhi wa moto*

(f) **Gari la wagonjwa:** Hili ni gari lililotengenezwa kwa ajili ya kubeba wagonjwa. Gari hili huweza kubeba mgonjwa wakati akiendelea kupatiwa huduma kabla ya kufikishwa hospitali. Katika shughuli ya uokoaji, gari la wagonjwa ni moja ya vitendea kazi muhimu. Watu walioungua na waliopata mshituko hubebwa na kupelekwa hospitali ili kupatiwa huduma ya kwanza na matibabu.




**Kielelezo namba 7:** *Gari la kubeba wagonjwa wakati wa dharura ya ajali ya moto*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(g) **Helikopta:** Helikopta hutumika kama sehemu ya vifaa vya zimamoto na uokoaji. Rubani hupewa amri ya kuelekea eneo la tukio, ili kubeba majeruhi. Pia, hutumika kwa kuzima moto kutokea angani kwa kutumia bomba maalumu lililofungwa ndani ya helikopta na kuachia maji yatoke iwapo mazingira hayaruhusu magari ya zimamoto kufika.

Vilevile, kwenye eneo lenye watu wengi, sehemu maalumu hutengwa na kuwekwa alama au kibao kuonesha kuwa ni mahali pa kukusanyika wakati wa majanga ya moto. Wakati wa janga la moto watu hukimbilia hapo kujinusuru na kubaini kama kuna mtu anakosekana kati ya watu wanaofanya kazi katika eneo moto ulipotokea. Huwa ni eneo lenye uwazi na lisiloweza kushika moto.

**Zoezi la 2**

1. Kwa kutumia mifano, eleza faida za kupata elimu ya zimamoto na uokoaji.
2. Chora mchoro wa mtungi wa kemikali ya kuzimia moto, onesha sehemu muhimu za mtungi huo.
3. Elezea hatua za kufuata kuzima moto kwa kutumia ndoo zenye mchanga mkavu.
4. Taja vifaa vya zimamoto vilivyopo katika mazingira unayoishi.

**Kazi ya kufanya namba 2**

Andaa igizodhima kuonesha namna ya kukabiliana na janga la moto katika mazingira ya nyumbani na liandike katika daftari lako.

## Hadhari za kuchukua kabla, wakati na baada ya janga la moto

Ni vema kuchukua hadhari wakati wa kukabiliana na janga la moto ili kuepusha madhara kwa jamii. Hadhari hizi hutegemea hatua ya tukio la moto.

Hadhari inayofaa katika hatua za awali kabla ya majanga kutokea ni elimu kwa wananchi kuhusu zimamoto na uokoaji. Wananchi waelimishwe namna ya kujenga nyumba zenye milango na madirisha ya dharura ili kusaidia shughuli ya uokoaji. Milango na madirisha ya dharura ni muhimu kwa sababu watu wanaweza kuokolewa au kujiokoa kupitia upande mwingine ambao moto



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 43 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

haujafika. Katika uelimishaji kuhusu majanga ya moto, watu waelimishwe umuhimu wa kuchora alama za kuonesha sehemu za kutokea pindi janga la moto linapotokea.

Pia, wananchi waelimishwe jinsi ya kutunza vifaa vya zimamoto eneo salama. Utunzaji endelevu wa vifaa hivi utasaidia kuviweka katika hali nzuri na salama ili kutumika wakati wa majanga. Pamoja na utunzaji mzuri wa vifaa, ni vyema kujifunza kuepuka matendo yanayoweza kusababisha kutokea kwa milipuko. Aidha, ni vizuri kuweka bima ya majanga ya moto.

Hadhari za kuchukua wakati janga la moto linapotokea ni pamoja na kuwasha king'ora/kengele ya hadhari au kupiga yowe ili kutoa taarifa au kuomba msaada. Wakati unafanya haya ukae mbali na eneo la moto ili kujinusuru na madhara ya moto. Unashauriwa kutoa taarifa kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kupiga simu namba **114** ili kupata msaada wa haraka. Wakati unajiokoa na janga la moto katika majengo marefu, unashauriwa usitumie lifti kujiokoa kwa kuwa upo uwezekano mkubwa wa kukatika kwa umeme na wewe ukanasa au kukosa hewa na kupoteza maisha. Ziba au funika mdomo kwa kitambaa ili usivute hewa chafu. Wataalamu wa majanga ya moto wanashauri usiguse vitu vinavyoweza kuongeza mlipuko wakati wa kujiokoa na usaidie wengine pale tu unapoona inawezekana. Pia, funga milango ya sehemu unazopita kuzuia moto kusambaa kwa haraka.

Baada ya janga la moto kutokea, tunashauriwa kutokuingia ndani ya jengo lililoungua kabla ya mamlaka zinazohusika kufanya ukaguzi wa eneo kujiridhisha juu ya usalama wake. Pia, tunahimizwa kuendelea kuwasaidia majeruhi wa janga la moto kama wapo kwa kutoa huduma ya kwanza na misaada mbalimbali. Baada ya uokoaji, hatua ya kutambua idadi ya watu waliokuwapo ni muhimu ili kujiridhisha kama watu wote wametoka. Panapokuwa na mabaki ya vitu vinavyoashiria mlipuko hakikisha huvigusi ili kuepusha mlipuko mwingine. Vitu vyenye kulipuka kwa urahisi vikiguswa hulipuka kwa haraka kwa sababu vinakuwa vimepata joto la ziada hivyo kuongeza uwezekano wa mlipuko. Usisogeze kitu chochote iwapo si lazima kufanya hivyo kwa kuwa unaweza kuharibu ushahidi wakati wa uchunguzi.



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 44 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 3**

1. Bainisha madhara yanayoweza kutokea kutokana na kushindwa kuchukua hadhari kabla, wakati na baada ya majanga ya moto.
2. Eleza umuhimu wa kuchukua hadhari ya majanga ya moto kabla hayajatokea.
3. Hatua zipi utachukua kukabiliana na majanga ya moto yakitokea kwenye eneo la shule yako?

**Kazi ya kufanya namba 3**

Fanya utafiti kuhusu vifaa vya kuzimia moto shuleni, kisha andaa hoja ya kushawishi uongozi wa shule uweke vifaa hivyo au kuboresha vilivyopo.

## Maadili ya kuzingatia wakati wa uokoaji katika janga la moto

Kabla ya kuanza zoezi la uokoaji unatakiwa kufanya tathmini ya eneo la tukio, lengo la kwanza ikiwa ni usalama wako na wengine waliopo eneo la tukio. Ili kutekeleza kwa weledi shughuli ya uokoaji, ni vyema mwokoaji akawa na moyo wa upendo kwa waathirika wa janga la moto. Ukiwa na moyo wa upendo ni dhahiri utamtendea mwathirika kila lililo jema ili kumwepusha na athari zaidi. Kazi ya uokoaji si rahisi, kwa hiyo inatakiwa mwokoaji awe na msukumo wa kusaidia kutoka moyoni mwake, na si kwa amri.

Pamoja na kuwaokoa watu waliopatwa na janga la moto, ni muhimu kutowadhuru au kuiba mali zao. Ni vyema kusaidia kuokoa mali zao baada ya kuwaokoa wao kwanza. Uokoaji uwe unaowajali waathirika na njia sahihi zitumike kulingana na mazingira ya janga. Pia, waathirika wa janga la moto wapatiwe hifadhi ili kulinda haki zao za kibinadamu. Aidha, baada ya kufanya kazi ya uokoaji, taarifa sahihi kuhusu tukio lilivyotokea itolewe.

## Majukumu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

Majukumu makuu ya jeshi hili ni pamoja na:

(a) Kuzima moto;

(b) Kufanya uchunguzi na ukaguzi wa kinga na hadhari ya moto kwa madhumuni ya kupata taarifa za chanzo cha moto na hasara zake;



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 45 30/07/2021 20:42


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) Kufanya uchunguzi ili kubaini kama matukio ya moto ni ya makusudi au ya bahati mbaya;
(d) Kufanya mafunzo kwa watumishi, maofisa wengineo na wazimamoto wa kujitolea;
(e) Kuhamasisha uelewa wa jamii kuhusu kuzuia matukio ya moto na huduma zinazotolewa na zimamoto;
(f) Kutayarisha mipango ya kuzuia majanga ya moto kwa kuzingatia mipango ya kuzuia maafa; na
(g) Kukagua michoro na usalama wa ujenzi wa miundombinu ya viwanda, miundombinu ya bidhaa za mafuta na gesi.

## Zoezi la 4

1. Ni matendo gani yanayopaswa kukemewa wakati wa uokoaji kwenye majanga ya moto?
2. Ni mahitaji gani ya kibinadamu wanayopaswa kupata waathirika wa majanga ya moto?
3. Ni matukio gani yanayoweza kujitokeza wakati wa uokoaji katika majanga ya moto?
4. Eleza umuhimu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

## Kazi ya kufanya namba 4



Kwa kushirikiana na wanafunzi wenzako katika vikundi, na kwa kuzingatia maadili, andaa igizodhima la namna ya kumhudumia mwathirika wa janga la moto.

## Zoezi la 5

**A:** Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi.

1. Unapoona janga la moto kwenye nyumba unapoishi haraka kimbilia chumbani ukachomoe redio kwenye swichi ya umeme ili kuokoa isiungue.________________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Ili kuharakisha shughuli ya kujiokoa na kuwaokoa wenzako walio ghorofani ni vizuri ukatumia lifti kama nyenzo ya kujiokoa kwa haraka zaidi.________________

3. Elimu ya zimamoto na uokoaji hutolewa madarasani tu kwa kuwa ndipo walipo wanafunzi wengi.________________

4. Elimu ya afya ya uzazi husaidia kuepusha mimba za utotoni.________

5. Blanketi si kifaa muhimu cha uokoaji katika majanga ya moto._______

**B:** Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake kwenye kisanduku.

6. Lipi kati ya yafuatayo si lengo sahihi la elimu ya afya ya uzazi?
   (a) kusaidia kuondoa mila potofu zinazoathiri afya ya uzazi
   (b) kupunguza idadi ya watu wasio na ajira duniani
   (c) kuepusha mimba za utotoni
   (d) kuwajengea vijana uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya mwili katika makuzi

7. Jeshi la Zimatoto na Uokoaji Tanzania lilianzishwa mwaka gani?
   (a) 1975
   (b) 1993
   (c) 2005
   (d) 2007

8. Ipi ni hatua ya hadhari ya kuchukua kabla ya janga la moto kutokea?
   (a) kuziba mdomo na blanketi
   (b) kuwapa majeruhi matibabu
   (c) kujenga nyumba zenye milango na madirisha ya mbele
   (d) kujenga nyumba zenye milango na madirisha ya dharura

9. Ni jaribio lipi hatari zaidi linaloweza kuleta na kusababisha mlipuko wa moto katika maeneo yetu?
   (a) matumizi ya mkaa wa kisasa
   (b) kutumia jiko la mafuta ya taa kwa uangalifu



FOR ONLINE USE ONLY

URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 47 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) kuwasha jiko la gesi bila kuzingatia taratibu za kiusalama
(d) majibu a, b na c yote ni sahihi

**C:** Oanisha kipengele kutoka **Sehemu A** na maneno yaliyopo **Sehemu B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.

| Sehemu A | jibu | Sehemu B |
|---|---|---|
| 10. Kuoa wake wengi | | (a) wakati wa kupata uelewa wa kutosha ili kukabiliana na mabadiliko ya mwili |
| 11. Zimamoto | | (b) husaidia vijana kujikinga na maradhi |
| 12. Wakati wa ujana | | (c) mchango mkubwa kwenye maambukizi ya magonjwa ya zinaa |
| 13. Hatua za awali za kukabiliana na majanga ya moto | | (d) jumla ya vitendo vya kuzuia kitu au vitu visiendelee kuwaka au kuteketea kwa moto |
| 14. Elimu ya afya ya uzazi | | (e) kufundisha watu jinsi ya kutumia vifaa vya kuzimia moto |
| | | (f) husaidia kujiajiri |
| | | (g) si wakati wa kupata elimu ya afya ya uzazi |

### Msamiati

Dhahiri — kitu kinachofahamika na kisicho na kificho, waziwazi

Hadhari — hatua za kuzuia jambo baya lisitokee

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 48 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

## Kujenga uhusiano mzuri na watu wengine

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza vitendo vinavyojenga maelewano katika jamii na kubaini ushauri wenye kujenga uhusiano mzuri na wenzako. Vilevile, ulijifunza namna ya kudumisha urafiki mzuri miongoni mwa wanafunzi wenzako na namna ya kutatua migogoro katika jamii unamoishi. Katika sura hii, utajifunza namna ya kujenga uhusiano mzuri na vitendo vinavyoonesha uaminifu na uhusiano mzuri katika jamii. Vilevile, utajifunza namna ya kushiriki katika kukemea vitendo vinavyoweza kuharibu uhusiano mzuri katika jamii. Maarifa na ujuzi utakaoupata katika sura hii, vitakusaidia kujenga na kuimarisha uhusiano mzuri katika jamii.*



**Fikiri**

Kwanini ni muhimu kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii?

### Uhusiano mzuri na wenzetu katika jamii

Jamii yenye ustawi na maendeleo ni ile iliyojengwa na watu wenye uhusiano mzuri. Uhusiano mzuri hujengwa kwa matendo mazuri yanayotendwa na wanajamii. Kuna vitendo mbalimbali vinavyojenga uhusiano mzuri katika jamii. Kwa mfano, mtu mkweli na muwazi hueleza jambo lilivyo bila kificho au kutoa uhalisia wa jambo bila kulipotosha. Tabia hii ni nzuri na ya kuigwa na wanajamii wengine. Mwanafunzi mwenye kuonesha vitendo vinavyoashiria ukweli na uwazi hupendwa na wanafunzi wenzake, walimu, na wanajamii wote kwa ujumla.



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 49 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pia, kujali na kuhifadhi vizuri rasilimali zilizopo hujenga uhusiano mzuri na watu wengine. Mtu mwenye kuonesha vitendo vya kutunza rasilimali, huthaminiwa na hupendwa na wanajamii wenzake. Vitendo hivi hufanya mtu anayetunza rasilimali kuaminiwa, hivyo kuwa na uhusiano mzuri na wanajamii wengine. Utunzaji rasilimali ni pamoja na kutunza viti na madawati, kutochafua kuta za shule na nyumba, na kulinda vifaa vya shule dhidi ya wezi.

Njia nyingine ya kutunza uhusiano mzuri ni kushirikiana katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya kijamii. Kushirikiana ni kufanya jambo kwa kuhusisha watu wengine katika jamii ili kufikia lengo. Mtu mwenye kupenda kushirikiana na watu wengine katika shughuli za kimaendeleo au za kijamii, hujenga na kukuza uhusiano mzuri na jamii inayomzunguka.

Mwanafunzi mwenye kuonesha vitendo vya heshima hupendwa na kufurahiwa na wanajamii wote. Vitendo vya heshima vinavyooneshwa na mwanafunzi kama vile, kusalimia wakubwa na kufanya shughuli za kijamii hujenga na kudumisha uhusiano mzuri katika jamii anamoishi.

Vilevile, uhusiano mzuri hudumishwa kwa njia ya kujitolea. Mtu anayejali watu wengine hutumia muda wake, elimu yake, na mali zake kuwasaidia wanajamii wenzake kupata maendeleo. Aidha, mtu anayejali watu wengine huwa na utashi wa kuona jamii inaondokana na changamoto mbalimbali. Hivyo, hufanya mambo mbalimbali yaliyotukuka kwa wanajamii na matokeo yake hujenga uhusiano mzuri na mwema katika jamii anamoishi.

### Vitendo vinavyoharibu uhusiano mzuri katika jamii

Kuna baadhi ya vitendo ambavyo watu hufanya katika jamii kwa kujua au kutokujua. Vitendo hivyo, huharibu ukaribu, udugu, amani na pengine kujenga chuki miongoni mwa watu. Mojawapo ya vitendo vinavyoharibu uhusiano mzuri ni tabia ya kumchukia mtu au watu fulani kwa sababu fulani. Chuki inaweza kusababisha watu kuuana au kuwa na kesi zinazochelewesha juhudi za kujiletea maendeleo. Mtu mwenye chuki au kinyongo hawezi kupendwa au kukubalika miongoni mwa wanajamii. Watu wanapokoseana, ni muhimu kusameheana na kupatana mapema.

Pia, tabia ya wizi au kushiriki katika shughuli za kujipatia kipato zisizo za halali huharibu uhusiano mzuri miongoni mwa wanajamii. Wizi husababisha hasara na mtu aliye mwizi huchukiwa na wenzake. Wakati mwingine mwizi

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 50 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

hupigwa na hata kuuawa. Hali hii huonesha kuvunjika kwa uhusiano mzuri katika jamii.

Vilevile, migogoro mingi katika jamii huharibu uhusiano mzuri miongoni mwa watu. Migogoro isipotatuliwa kwa makini na kwa haraka huweza kuleta hasara kubwa kwa jamii. Kwa mfano, migogoro kati ya walimu na wanafunzi, husababisha wanafunzi kufeli mitihani au wengine kufukuzwa shule. Vilevile, wanafunzi wanapogombana wao kwa wao, huweza kuumizana.

Aidha, uvivu au kutokutimiza wajibu ni tabia nyingine inayoweza kuharibu uhusiano mzuri katika jamii. Mtu mvivu au mzembe husababisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa majukumu katika jamii. Hali hii huweza kufanya watu wachukiane. Kwa mfano, wanafunzi wanapokubaliana kujisomea katika kikundi, kila mmoja anapaswa kutimiza jukumu lake.Endapo mmojawapo atakuwa mzembe, wenzake wataudhika au watamfukuza kwa sababu atakuwa anakwamisha malengo ya kikundi.

Hali kadhalika, mtu anapokuwa na tabia ya ubinafsi na kutojali wenzake, huchukiwa na wenzake na hivyo kufifisha uhusiano mzuri katika jamii anamoishi. Ili kujenga jamii imara yenye uhusiano mzuri, ni muhimu kushirikiana na wenzako katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya wote. Kwa mfano, mwanafunzi anayesoma peke yake na hapendi kushirikiana na wenzake, halafu akashindwa kuelewa swali fulani. Je, mwanafunzi huyu atamuuliza nani wakati yeye hapendi kushirikiana wala kuongea na wenzake?

FOR ONLINE USE ONLY

**Zoezi la 1**

1. Eleza kwa kifupi maana ya kauli zifuatazo:
   (a) “Mtu mwenye kinyongo ni hatari kwa jamii”
   (b) “Ukiwa mkweli watu watakupenda”
2. Eleza ni kwa namna gani kujitolea hukuza uhusiano mzuri katika jamii.



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 51 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 1**

Chunguza baadhi ya matendo yanayofanywa na watu katika jamii unapoishi ambayo yanaharibu uhusiano mzuri miongoni mwa wanajamii. Andika maelezo mafupi kuhusu matendo hayo na wasilisha darasani.

## Mikakati ya kukemea vitendo vinavyoharibu uhusiano mzuri na watu wengine

Mwanafunzi, unaweza kutenda matendo mbalimbali ili kuzuia vitendo vinavyoharibu uhusiano mzuri katika jamii. Unaweza kutoa kauli mbalimbali za kuhimiza umoja na mshikamano katika jamii. Kwa mfano, kupitia mkutano wa wanafunzi wote, unaweza kuhamasisha ushiriki wa kila mwanafunzi katika zoezi la uchaguzi wa viongozi shuleni. Pia, unaweza kutoa kauli inayohimiza wanafunzi wenzako kuunda kikundi cha kujisomea pamoja ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kufaulu vizuri katika mtihani wa Taifa. Vilevile, unaweza kuunda klabu mbalimbali zenye malengo ya kukemea, kuwafundisha na kuwaonya wanafunzi wote wavivu, watoro, wakorofi, wagomvi na wale wenye majivuno au chuki dhidi ya wenzao.

Hali kadhalika, ili kudumisha uhusiano mzuri shuleni, unaweza kushirikiana na wenzako kuunda kamati ndogo ya usuluhishi katika darasa, familia, katika kijiji au mtaa unamoishi. Kamati hii itashirikisha watu wenye upeo tofauti katika kushauri, kukemea au kuripoti watu wote wanaokwenda kinyume na maadili ya jamii. Pia, kamati hii inaweza kuunda kikosikazi kidogo cha kusimamia usuluhishi wa migogoro. Ni muhimu kukumbuka kwamba hata wewe mwanafunzi unao uwezo wa kuhamasisha wanafunzi wenzako, familia au jamii unamoishi kufanya matendo yanayodumisha uhusiano mzuri katika jamii yako.

**Zoezi la 2**

1. Ni matendo gani matatu yanayokusaidia kujenga uhusiano mzuri na wenzako darasani?
2. Kuna manufaa gani ya kuwa na uhusiano mzuri na wanajamii katika mazingira yetu tunayoishi?
3. Eleza kwa kifupi namna uhusiano mzuri unavyochangia wanajamii kupata maendeleo yao kwa haraka.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 52 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 2**

Chunguza matendo matatu katika jamii unamoishi ambayo yamefanywa na baadhi ya watu na yamejenga uhusiano mzuri miongoni mwa wanajamii. Andika maelezo mafupi kuhusu matendo hayo kwenye daftari lako la mazoezi.

### Umuhimu wa uhusiano mzuri katika jamii

Uhusiano mzuri katika jamii una umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya jamii. Uhusiano mwema hukuza umoja. Jamii yenye uhusiano mzuri huwa na sauti moja na mshikamano. Umoja huu huleta maendeleo kwa haraka katika jamii.

Mahali penye uhusiano mzuri wanajamii wenye uzoefu wa aina tofauti hushirikiana kwa manufaa ya jamii nzima. Kwa mfano, tunapohitaji kujenga majengo ya shule, wapo watu wenye uzoefu wa kuhamasisha wanajamii watoe michango. Aidha, wapo mafundi wenye ujuzi na uzoefu tofauti tofauti ambao wanaweza kujitolea kujenga majengo ya shule kwa kuzingatia fani zao. Mathalan, fundi mwashi, atajitolea kutengeneza matofali, seremala atajitolea katika ujenzi wa paa la jengo, na fundi wa kupaka rangi atajitolea kupaka rangi majengo yaliyojengwa.

Jamii yenye uhusiano mzuri hujiwekea sheria na taratibu za kufuata ili kujenga na kudumisha nidhamu. Nidhamu katika jamii huwezesha kuimarisha ulinzi na usalama. Pia, huwezesha wanajamii kushirikiana kulinda katika vikundi vya ulinzi na kufanya mazingira kuwa salama. Ulinzi hujumuisha watu, mali zao na rasilimali nyingine zilizopo katika jamii. Uhusiano mzuri huondoa hila na chuki hivyo kuweka mazingira mazuri ya uwajibikaji na kushirikiana katika kuilinda jamii husika.

**Zoezi la 3**

1. Fafanua vitendo vinne vinavyoweza kuharibu uhusiano mzuri kati yako na rafiki zako au jamii unamoishi.
2. Orodhesha na ufafanue mikakati unayoweza kupanga ili kujenga uhusiano mzuri na rafiki zako au wanafunzi wenzako darasani.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Eleza faida nne za kudumisha uhusiano mzuri kati yako na jamii inayokuzunguka.

### Kazi ya kufanya namba 3



Kwa kushirikiana na wanafunzi wenzako, undeni kikundi cha usuluhishi wa migogoro katika darasa. Andikeni mikakati yenu na muwasilishe darasani kwa majadiliano zaidi.

## Zoezi la 4

**A:** Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi.

1. Uhusiano mzuri miongoni mwa jamii hujenga ustawi na maendeleo ya watu.__________

2. Chuki, ubinafsi na roho mbaya hujenga umoja na mshikamano katika jamii unamoishi.____________

3. Uvumilivu na ustahimilivu wa matatizo yako na ya watu wengine ni njia ya kuwa na umoja na amani katika jamii.____________

4. Wanafunzi hawana mchango wowote katika kujenga jamii bora yenye maelewano kwa sababu wao bado ni wadogo.___________

5. Maandamano miongoni mwa wanafunzi ni njia bora ya kudumisha uhusiano mwema katika jamii.____________



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 54 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B.** Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake kwenye kisanduku.

6. Ni njia ipi kati ya zifuatazo hujenga umoja na mshikamano katika jamii?
   (a) kuwa mvivu na kujenga chuki kwa wanaokuchukia
   (b) kuchagua marafiki wenye akili timamu na wenye fedha tu
   (c) kuwapenda zaidi ndugu zako na kuwapendelea kuliko watu usiowafahamu
   (d) kuheshimu kila mtu bila kujali rika lake, itikadi yake au dini yake

7. Kuheshimu jamii, kuwajali wengine, kuwa mkweli na kuwajibika kwa jamii vinasaidiaje watu?
   (a) hujenga kujiamini na uthubutu
   (b) hujenga uhusiano mzuri katika jamii
   (c) hujenga uadui baina ya watu katika jamii
   (d) hujenga hofu na kuogopa wanaokuzidi umri

8. Ni lipi jukumu lako katika kudumisha umoja miongoni mwa wanafunzi wenzako?
   (a) kutoa kauli mbalimbali au kushiriki shughuli zinazodumisha umoja kama vile kusoma pamoja
   (b) kuongoza wanafunzi wengine kuandamana na kudai haki pale wanapokosa uji au chai shuleni
   (c) kutetea wavivu na wazembe katika shughuli za darasani
   (d) kujitenga na wanafunzi wenzako ili uweze kufanya vizuri darasani

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C.** Oanisha kipengele kutoka **Sehemu A** na maneno yaliyopo **Sehemu B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.

| Sehemu A | Jibu | Sehemu B |
|---|---|---|
| 9. Chuki | | (a) njia ya kudumisha umoja na mshikamano katika jamii |
| 10. Uaminifu | | (b) hujenga uadui na kudumaza maendeleo |
| 11. Vikundi shirikishi | | (c) moja ya mikakati au mbinu ambazo mwanafunzi anaweza kutumia kuzuia vitendo vinavyovunja umoja katika jamii. |
| 12. Ulinzi na usalama | | (d) matokeo ya uhusiano mzuri katika jamii |
| 13. Uchochezi | | (e) haki na wajibu wa kila mtu |
| | | (f) kushawishi au kuhamasisha watu wengine kufanya makosa |
| | | (g) kushawishi au kuhamasisha watu kupinga Serikali |
| | | (h) ni kitendo cha kutokuwa mkweli na muwazi katika jamii |

**Msamiati**

Utashi shauku au hali ya kutamani kufanya kitu fulani

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Sita

## Kulinda rasilimali kwa masilahi ya nchi

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza wajibu wa jamii katika shughuli za maendeleo ya Taifa, tabia ya mtu anayetumia elimu yake kuleta maendeleo ya Taifa na kubaini vitendo vya kulinda usalama wa Taifa. Vilevile, ulijifunza mbinu stahiki za kulinda mali za umma, vitendo vya matumizi mabaya ya mali za umma, njia madhubuti za kupambana na matumizi mabaya ya mali za umma na shughuli za kuleta maendeleo ya nchi. Katika sura hii, utajifunza namna ya kulinda rasilimali kwa masilahi ya nchi. Aidha, utajifunza namna ya kushiriki kutoa elimu dhidi ya rushwa ili kulinda masilahi ya Taifa letu. Maarifa na ujuzi huu utakuwezesha kujenga tabia ya kuwa mzalendo kwa nchi yako katika kupambana na vitendo vya kutoa na kupokea rushwa katika jamii unamoishi.*



**Fikiri**

Mali za nchi yetu zinalindwa na nani?

### Athari za rushwa kwa rasilimali za nchi

Rasilimali ni vitu muhimu na vya thamani vinavyomilikiwa na nchi, shirika au mtu binafsi. Rasilimali za nchi ni muhimu kwa maendeleo ya nchi na ustawi wa wananchi wake. Hata hivyo, rushwa inaposhamiri husababisha madhara mengi katika matumizi ya rasilimali za nchi. Baadhi ya athari za rushwa kwa rasilimali za nchi ni pamoja na:

(a) **Kuathiri upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo:** Viongozi wasio waaminifu wanaweza kupokea rushwa na kuandaa mipango mibovu ambayo si thabiti katika kuendeleza na kulinda rasilimali za nchi. Hali hii inaweza kusababishwa na kupokea rushwa ili waandae au wapitishe mipango yenye upendeleo kwao au watu waliowapa rushwa. Mipango kama ya uendelezaji wa elimu ngazi mbalimbali, ulindaji wa



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 57 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

wanyamapori, uchimbaji wa madini, na utunzaji wa vyanzo vya maji inaweza kuathirika kwa sababu ya rushwa. Hivyo, rushwa ikidhibitiwa husaidia kuwapo na mipango thabiti ya kuendeleza na kulinda rasilimali za nchi.

(b) **Ukiukwaji wa sheria na upotoshaji wa haki:** Kitendo cha kupokea rushwa kwa baadhi ya viongozi husababisha ukiukwaji wa sheria na haki hivyo kinaweza kuleta ugomvi miongoni mwa wananchi. Kwa mfano, viongozi wanaweza kugawa maeneo ya wafugaji kwa wakulima au kugawa maeneo ya wakulima kwa wafugaji baada ya kupokea rushwa. Hali hii husababisha wananchi kugombea ardhi na hivyo kuibua migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji.

(c) **Ukosefu wa huduma za kijamii:** Rushwa inaweza kusababisha upendeleo katika utoaji wa huduma za afya, elimu, maji na nyinginezo. Serikali huwekeza fedha nyingi katika huduma za kijamii lakini rushwa huzuia upatikanaji wake kwa wananchi. Hali hii hutokea endapo baadhi ya viongozi wasio waaminifu watatumia fedha hizo kwa ajili ya manufaa yao binafsi. Kwa mfano, rushwa katika utoaji wa zabuni za ujenzi wa miundombinu ya huduma za jamii husababisha ujenzi kufanyika kwa kiwango cha chini. Hali hii husababisha miundombinu kuharibika mapema na hivyo kusababisha ukosefu wa huduma za jamii kwa wananchi na Serikali hupata hasara.

(d) **Ukiukwaji wa utaratibu sahihi wa matumizi ya rasilimali:** Rushwa inaweza kufanya viongozi kupindisha utaratibu wa matumizi ya rasilimali kwa manufaa yao binafsi au watu waliowapa rushwa. Endapo utaratibu wa matumizi ya rasilimali haufuatwi kwa mujibu wa sheria, matumizi mabaya ya rasilimali za nchi hujitokeza. Hali hii hukwamisha ukamilikaji wa miradi ya Serikali na hivyo kuchelewesha utoaji wa huduma za kijamii na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

**Zoezi la 1**

1. Fafanua kwa mifano jinsi rushwa inavyoweza kuathiri mipango ya kuendeleza na kulinda rasilimali za nchi.
2. Rushwa inawezaje kusababisha ukosefu wa amani na utulivu katika jamii?
3. Eleza jinsi huduma za jamii zinavyoweza kuathiriwa na rushwa.



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 58 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Toa mapendekezo ya kuzuia rushwa kwenye matumizi ya rasilimali za nchi.

**Kazi ya kufanya namba 1**



Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu vitendo vinavyoonesha kuwapo kwa rushwa katika jamii unamoishi. Toa mapendekezo ya njia za kudhibiti vitendo hivyo na wasilisha darasani kwa majadiliano zaidi.

## Ushiriki wa asasi zisizo za kiserikali katika ulinzi wa rasilimali za nchi

Masilahi ya nchi ni kitu chochote ambacho nchi inaona ni muhimu kwa ustawi wa jamii ambacho ipo tayari kukilinda au kugharamia kukipata. Pia, masilahi ya nchi ni mambo yote yanayoinufaisha nchi na wananchi wake kwa msingi wa kuleta ustawi wa nchi. Masilahi ya nchi yanatakiwa kulindwa na kila mwananchi na taasisi zote ikiwa ni pamoja na madhehebu ya dini na taasisi nyingine sizizo za kiserikali. Taasisi hizi zinaweza kushiriki katika kutoa elimu dhidi ya rushwa ili kulinda masilahi ya nchi.

Taasisi za kidini hutoa mafundisho kwa waumini wao juu ya rushwa na athari zake. Mafundisho haya husaidia kuwajenga waumini kukataa na kupambana na rushwa. Asasi zisizo za kiserikali ni pamoja na taasisi za dini, mashirika ya kujitolea, na asasi za kiraia ambazo zinajihusisha na kutoa huduma za kijamii, kiuchumi na kisheria bila faida. Asasi za kidini zimekuwa na mchango mkubwa katika kuelimisha jamii juu ya madhara ya kutoa na kupokea rushwa.

Elimu inayotolewa na asasi zisizo za kiserikali husaidia wananchi kuelewa kwa kina jinsi ya kulinda rasilimali za nchi. Pia, elimu hii inawezesha kupata mbinu na mikakati ya kupambana na rushwa zinazoathiri rasilimali za nchi na kufichua maovu yanayohusiana na rushwa. Aidha, elimu inayotolewa inawawezesha wananchi kujua sheria na kuwahamasisha kupambana na vitendo vya rushwa.

FOR ONLINE USE ONLY

**Zoezi la 2**

1. Toa mapendekezo yako jinsi asasi zisizo za kiserikali zinavyoweza kushiriki katika utoaji wa elimu dhidi ya rushwa.



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 59 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Taasisi za dini zina mchango gani katika mapambano dhidi ya rushwa?
3. Vyombo vya habari vina mchango gani katika kutoa elimu dhidi ya rushwa?

**Kazi ya kufanya namba 2**

Kwa kushirikiana na wanafunzi wenzako katika kikundi, tembelea asasi za kisheria, kijamii au dini zilizopo jirani na maeneo ya shule na muulize mikakati wanayotumia kuelimisha jamii juu ya kuzuia na kupambana na rushwa. Andika majibu mliyojadiliana katika daftari lako la mazoezi.

### Changamoto zinazokabili utoaji wa elimu dhidi ya rushwa

Taasisi za kiserikali na asasi zisizo za kiserikali zinakabiliwa na changamoto mbalimbali katika utoaji wa elimu dhidi ya rushwa. Baadhi ya changamoto hizo ni kama zifuatavyo:

(a) **Uhaba wa rasilimali watu na fedha:** Rasilimali watu na fedha ni nyenzo muhimu katika kuwezesha utoaji wa elimu kwa jamii dhidi ya rushwa. Uhaba wa fedha na rasilimali watu hukwamisha utoaji wa elimu kuhusu rushwa.

(b) **Ukosefu wa jukwaa la kitaifa:** Katika utoaji wa elimu dhidi ya rushwa kwa jamii, jukwaa la kitaifa ni muhimu kwa kuwa linatoa nafasi kuwapo kwa mijadala mbalimbali ya wazi kuhusu rushwa. Mijadala hiyo itatoa nafasi kwa wadau mbalimbali kupata mafunzo juu ya kuzuia na kupambana na rushwa. Kukosekana kwa jukwaa la kitaifa kumesababisha jamii kukosa fursa ya kupata elimu dhidi ya rushwa. Kwa mfano, sababu za rushwa, athari za rushwa na njia za kuzuia na kupambana na rushwa.

(c) **Mitazamo tofauti katika jamii:** Mitazamo tofauti ya uelewa wa madhara ya rushwa katika jamii husababisha kukosekana kwa mwelekeo wa pamoja katika kupambana na rushwa. Baadhi ya wananchi wanaamini kwamba bila kutoa rushwa hawawezi kupata huduma stahiki katika ofisi za umma na binafsi. Katika maeneo mengine rushwa inachukuliwa kama zawadi au asante kwa kupata huduma kwenye ofisi fulani. Wananchi wengine wanaamini rushwa ni mfumo usiokwepeka na upo tangu kale, hivyo hawaoni uwezekano wa kuiondoa.

(d) **Ushirikishwaji hafifu wa sekta binafsi:** Sekta binafsi ni wadau muhimu katika mapambano dhidi ya rushwa. Sekta hii inashughulika na masuala ya msingi ya kijamii kama vile afya, kilimo, biashara, elimu



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 60 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

na maeneo mengine. Hata hivyo, sekta hii imekuwa na ushiriki hafifu katika mapambano dhidi ya rushwa. Hali hii inasababisha sekta hii kushindwa kutoa mchango wake wa kutosha katika utoaji wa elimu na mapambano dhidi ya rushwa.

## Zoezi la 3

1. Taja njia tatu zinazoweza kusaidia kutatua tatizo la utoaji na upokeaji rushwa.
2. Kwa kutumia mifano, eleza namna rushwa inavyoweza kurudisha nyuma maendeleo yako binafsi.
3. Elezea kwa kifupi changamoto nne za utoaji wa elimu dhidi ya rushwa nchini.

## Kazi ya kufanya namba 3



Jadiliana na wanafunzi wenzako katika kikundi na uandae mpangokazi wa kutokomeza matukio yanayoashiria rushwa shuleni kwako au katika jamii unamoishi. Kisha, andika mpangokazi huo katika daftari lako la mazoezi.

## Zoezi la 4

**A.** Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi.

1. Asasi zisizo za kiserikali zina jukumu la kupambana na rushwa zote kasoro rushwa ya ngono.__________
2. Kukosekana kwa maadili na uadilifu katika jamii ni chanzo kikubwa cha kushamiri kwa rushwa nchini.___________
3. Ufanisi katika ujenzi wa miundombinu katika nchi yetu ni ishara ya mafanikio katika mapambano dhidi ya rushwa.___________
4. Mapambano dhidi ya rushwa ni kazi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa tu.___________
5. Ukiukwaji wa haki za binadamu ni matokeo ya kushamiri kwa utoaji



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 61 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

na upokeaji wa rushwa katika jamii.__________

6. Baadhi ya watumishi wa Serikali hupoteza ushahidi wa mienendo ya uchunguzi wa rushwa kwa masilahi ya nchi.__________

7. Ili Taifa liweze kuendelea ni lazima rushwa ipigwe vita katika sehemu za kazi tu.__________

8. Asasi zisizo za kiserikali zinasaidia kutoa elimu dhidi ya rushwa kwa wananchi.__________

9. Mijadala ya wazi dhidi ya rushwa huwajengea wananchi uwezo wa kupambana na rushwa.__________

10. Mapambano dhidi ya rushwa katika kulinda rasilimali za nchi ni jukumu la Serikali tu.__________

**B.** Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake kwenye kisanduku.

11. Kuendelea kwa tatizo la rushwa ni changamoto inayozikabili taasisi za Serikali na asasi zisizo za kiserikali kwa sababu gani?
    (a) wananchi wana imani kwamba rushwa ni nzuri
    (b) wananchi wa Tanzania ni wakarimu
    (c) maadili na uadilifu unakosekana
    (d) watu wanataka kuwa na maendeleo binafsi na ya nchi

12. Taasisi zisizo za kiserikali zina wajibu gani katika jamii?
    (a) kuelimisha walioathiriwa na rushwa tu
    (b) kuwapa msaada wa kifedha walioathiriwa na matukio ya rushwa
    (c) kutoa elimu kwa umma juu ya madhara ya rushwa
    (d) kupambana na wanaotoa taarifa za rushwa kwenye jamii

13. Kuzuia na kupambana na rushwa nchini husaidia kukuza uchumi wa nchi na kuleta maendeleo katika uboreshaji wa jambo lipi katika Taifa?
    (a) miundombinu
    (b) masilahi ya watu wachache

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 62 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) watoa rushwa
(d) afya za wapokea rushwa

14. Ni kwanini mitazamo tofauti ya madhara ya rushwa katika jamii hutokea?
    (a) utendaji duni wa kazi
    (b) elimu duni juu ya rushwa
    (c) ukosefu wa mipango
    (d) watoaji na wapokeaji wa rushwa kutoshitakiwa

15. Kipi kati ya yafuatayo si madhara ya rushwa kwa rasilimali za nchi?
    (a) kukosekana kwa mipango thabiti ya kulinda rasilimali
    (b) ukosefu wa huduma bora kwa wananchi
    (c) thamani halisi ya rasilimali kutojulikana
    (d) kuimarika kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa

**Msamiati**

Waumini — watu wanaoamini na kufuata itikadi ya dini fulani

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba

## Kutekeleza majukumu katika jamii

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza kutambua majukumu yako kama kiongozi katika ngazi ya familia na shule. Pia, uliweza kubaini njia mbadala za kutatua matatizo, kupendekeza njia sahihi za kuboresha utendaji kazi, kushirikiana na watu wengine na hasara za kutokuwashirikisha wengine katika utekelezaji wa majukumu. Vilevile, ulijifunza kushirikiana na wanajamii katika shughuli za maendeleo na kufichua maovu yanayohusiana na ubadhirifu na ufisadi katika utekelezaji wa majukumu. Katika sura hii, utajifunza namna ya kutekeleza majukumu yako katika jamii kwa kujitolea. Maarifa na ujuzi utakaopata katika sura hii utakuwezesha kutekeleza majukumu yako na kushiriki katika shughuli za kijamii ili kuleta maendeleo yako na ya jamii kwa ujumla.*

**Fikiri**

Mwanafunzi ana majukumu gani katika jamii inayomzunguka?

### Kutekeleza majukumu katika jamii yako

Kutekeleza majukumu katika jamii ni kufanya kazi au shughuli ambazo unatakiwa au unatarajiwa kuzifanya kulingana na nafasi uliyonayo katika jamii unamoishi. Mwanafunzi ni sehemu ya jamii, kwa hiyo, analo jukumu kubwa la kushiriki katika shughuli za kijamii ili kuleta maendeleo. Maendeleo yanaweza kuwa ya mtu binafsi au ya wanajamii kwa ujumla. Mwanafunzi anaweza kutekeleza majukumu yake ya kijamii akiwa shuleni na nyumbani.

Katika jamii mwanafunzi anaweza kushiriki kufanya kazi ndogondogo zinazoendana na umri wake. Shughuli hizi ni muhimu sana kwani humwandaa mwanafunzi kujifunza jinsi ya kutekeleza majukumu yake na ya kijamii atakapohitimu elimu ya msingi. Mfano, mwanafunzi anaweza kushiriki kwa kusaidia kusogeza vifaa vya ujenzi kama mchanga, mawe na mbao karibu na eneo la shughuli za ujenzi wa vyumba vya madarasa, ofisi za walimu, nyumba

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 64 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

za walimu na vyoo vya shule. Pia, mwanafunzi anaweza kushiriki katika ujenzi wa majengo ya shule kwa kumwagilia maji kuta za majengo yaliyojengwa ili kuzifanya kuwa imara. Ushiriki wa wanafunzi katika kazi za ujenzi husaidia kujenga tabia ya uwajibikaji na uzalendo miongoni mwa wanafunzi. Aidha, husaidia kujenga stadi za kiufundi kwa njia ya kuona wenye ujuzi wanavyofanya kazi. Ushiriki wa wanafunzi katika shughuli za jamii hufanyika katika muda wa ziada bila kuathiri mahudhurio ya vipindi darasani. Pia, kazi atakazofanya lazima ziendane na umri wake na zisiwe hatarishi.

### Kushiriki kutoa huduma za jamii

Mwanafunzi anaweza kushiriki katika kuhakikisha jamii inapata huduma bora na kwa wakati. Katika kutekeleza jambo hili, mwanafunzi kwa kushirikiana na wazazi au walezi wake anaweza kutoa huduma katika jamii kwa kutoa vyakula kwa watu wenye uhitaji. Pia, anaweza kushawishi shule kutoa sehemu ya mazao yanayolimwa na shule iwapo shule ina shamba.

Vilevile, mwanafunzi mzuri na mwadilifu anaweza kufundisha watoto na wanajamii wengine kusoma, kuandika na kuhesabu. Huduma hii itasaidia kupunguza idadi ya watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu kwenye jamii.

Njia nyingine ni kushiriki katika kutunza mazingira na mali za watu kwa kuepuka kutupa taka au kuwasha moto ovyo. Pia, mwanafunzi anaweza kuchukua jukumu la kulinda usalama wa wanajamii na mali zao kwa kutoa taarifa juu ya viashiria vyovyote vya hatari katika mazingira ya jamii inayomzunguka na kukemea uharibifu wowote unaoweza kutokea kwenye mazingira yake.

Mwanafunzi anaweza kushiriki kutunza vyanzo vya maji ili huduma ya maji iendelee kupatikana bila usumbufu. Hii itawezekana kwa kupanda miti kuzunguka vyanzo vya maji. Pamoja na hayo, mwanafunzi anaweza kutoa taarifa ya uharibifu wa miundombinu unaofanywa na watu wenye nia mbaya.

Hali kadhalika, ili kuhakikisha jamii inaelewa umuhimu na namna ya kutunza mazingira, mwanafunzi mwadilifu anapaswa kuelimisha jamii kwa vitendo ikiwa ni pamoja na kuandaa kazimradi ili kutunza mazingira. Katika kutekeleza jukumu la utunzaji wa mazingira, kazimradi inaweza kujumuisha; upandaji wa miti, kufyeka majani, kukusanya taka, kulinda vyanzo vya maji na kuzuia uchafuzi wa hewa. Kazimradi inaweza kutekelezwa na mwanafunzi katika

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mazingira ya shule au nyumbani.

## Kuandaa na kutekeleza kazimradi ili kuboresha mazingira

Kazimradi ni shughuli zinazopangwa na kutekelezwa ili kufikia lengo maalumu kwa muda uliopangwa. Kuna hatua mbalimbali za kuzingatia katika uandaaji na utekelezaji wa kazimradi. Hatua hizo ni pamoja na; kubaini tatizo na chanzo chake, kuweka malengo na mikakati ya jinsi ya kutatua tatizo. Hatua zingine ni kuandaa mpangokazi, kubainisha shughuli zitakazotekelezwa, vifaa vitakavyotumika, gharama, muda wa utekelezaji na kufanya tathmini endelevu na tathmini tamati.

Uandaaji na utekelezaji wa kazimradi una faida mbalimbali kwa mwanafunzi na jamii kwa ujumla. Katika utunzaji wa mazingira, kwa mfano, kazimradi humjengea mwanafunzi na jamii ubunifu wa namna mbalimbali za kukabiliana na uharibifu wa mazingira. Pia, kazimradi humjengea mwanafunzi uwezo wa kuelewa kwa undani mazingira anamoishi na hivyo kuweza kuielimisha jamii juu ya utunzaji wake. Vilevile, kazimradi inamjengea mwanafunzi uwezo wa kujiamini katika kukabiliana na changamoto mbalimbali za mazingira.

### Zoezi la 1

1. Eleza umuhimu wa kushiriki katika kutoa huduma za jamii.
2. Ni kwa namna gani mwanafunzi anaweza kutunza vyanzo vya maji katika jamii yake?
3. Taja njia tatu utakazotumia kushiriki katika shughuli za maendeleo kwenye jamii yako.
4. Eleza kwa kifupi umuhimu wa kuwafundisha wanajamii wasiojua kusoma na kuandika katika jamii unamoishi.
5. Fafanua hatua na faida za kuandaa na kutekeleza kazimradi.

### Kazi ya kufanya namba 1



Jadiliana na wanafunzi wenzako jinsi mtakavyoshiriki kuelimisha wanajamii kutunza mazingira na mali zao katika eneo unaloishi. Wasilisha majibu darasani kwa majadiliano zaidi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Rasilimali zinazoweza kumsaidia mwanafunzi kutekeleza majukumu yake katika jamii

Jamii inapaswa kuwa na rasilimali muhimu ili kumsaidia mwanafunzi kutekeleza majukumu mbalimbali. Baadhi ya rasilimali hizo ni muda, ardhi, fedha, watu, misitu, mifugo, vyanzo vya maji, vyombo vya usafiri, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

**Muda:** Muda ni rasilimali adimu sana duniani. Hii ni kwa sababu muda ukishapotea hauwezi kupatikana tena. Tunahitaji muda ili tutekeleze majukumu yetu ipasavyo.

**Ardhi:** Kuwapo kwa ardhi humsaidia mwanafunzi kushiriki katika shughuli mbalimbali zinazoweza kuinufaisha jamii yake. Ardhi inaweza kumsaidia mwanafunzi kulima bustani pamoja na mazao ya chakula na ya biashara. Ushiriki wa mwanafunzi katika shughuli za kilimo husaidia kumjengea dhamira ya uwajibikaji na ujuzi katika kilimo. Pia, humsaidia kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, hivyo kuipatia familia yake chakula na fedha kwa matumizi ya kila siku.

**Fedha:** Rasilimali fedha ni muhimu katika kufanikisha majukumu mbalimbali katika jamii. Kuwapo kwa fedha humsaidia mwanafunzi kununua pembejeo za kilimo na ufugaji na hivyo kuinua uchumi wa jamii yake. Kwa mfano, ili mwanafunzi aweze kuanzisha kilimo cha mbogamboga nyumbani, anahitaji fedha ya kununulia mbegu sahihi ambazo zinastawi katika eneo analoishi ili kutoa mazao bora. Mwanafunzi anaweza pia kuwa na uwezo wa kufanya biashara ndogo ndogo kulingana na mazingira yake. Shughuli hizi zinaweza kufanyika bila kuathiri ratiba ya masomo yake.

**Rasilimali watu:** Ili mwanafunzi aweze kutimiza majukumu mbalimbali kwenye jamii yake anahitaji watu wa kushirikiana naye. Watu wanaomzunguka wanaweza kushirikiana naye katika kutimiza majukumu mbalimbali katika jamii yake. Kuwapo kwa watu humsaidia mwanafunzi kushiriki katika shughuli mbalimbali zikiwamo za ujenzi wa miundombinu ya barabara, madarasa na vyoo vya shule au shughuli za kilimo. Iwapo mwanafunzi atakuwa anataka kuuza bidhaa, rasilimali watu ndiyo wahusika wa ununuzi wa bidhaa zinazohusika.

**Misitu:** Kuwapo kwa misitu katika mazingira ya jamii inayohusika humsaidia mwanafunzi kutekeleza majukumu ya kujifunza na kuwasaidia wanajamii

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

wengine. Baadhi ya misitu huwa makazi ya wanyama wa kipekee ambao ni fursa ya mwanafunzi kujifunza. Aidha, misitu inasaidia kuleta mvua, kutunza unyevu na kuhifadhi vyanzo vya maji. Mvua husaidia kukuza mazao ambayo mwanafunzi amelima.

**Mifugo:** Mwanafunzi anaweza kushiriki katika shughuli za ufugaji ili kusaidia jamii kupata mahitaji ya mazao ya ufugaji kama nyama na maziwa. Kwa mfano, kupitia ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo, sungura, bata na kuku, mwanafunzi anaweza kutimiza jukumu la uzalishaji mali katika jamii. Pia, mwanafunzi anaweza kushiriki katika kulisha mifugo ya familia baada ya ratiba ya shule kukamilika.

**Vyanzo vya maji:** Mito, maziwa, mabwawa, chemchemi, mvua na bahari ni rasilimali muhimu sana ambazo mwanafunzi anaweza kuzitumia kutekeleza majukumu yake katika jamii anamoishi. Kuwapo kwa vyanzo vya maji humsaidia mwanafunzi kushiriki katika shughuli za uvuvi hasa kipindi cha likizo au baada ya muda wa masomo. Vilevile, humsaidia kutimiza jukumu la kuchota maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

**Vyombo vya usafiri:** Vyombo vya usafiri kama vile magari, pikipiki, na baiskeli humsaidia mwanafunzi kutekeleza majukumu yake kwenye jamii. Vyombo hivi vya usafiri humsaidia mwanafunzi kuwahi shule na kuhudhuria masomo ipasavyo. Pia, husaidia kubeba mazao kutoka shambani na kupeleka nyumbani au sokoni.

**Zoezi la 2**

1. Ardhi ina manufaa gani katika kutekeleza majukumu yako katika jamii?
2. Bainisha rasilimali tano ambazo unaweza kuzitumia katika kutekeleza majukumu yako katika jamii.
3. Kwanini unahitaji watu ili kutekeleza majukumu kwenye jamii yako?
4. Kwa kutumia mifano, fafanua jinsi maji yanavyokusaidia kutekeleza majukumu yako kwenye jamii.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 68 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 2**

Chunguza ardhi ilivyo katika eneo unaloishi kisha bainisha jinsi unavyoweza kuitumia kutekeleza majukumu yako katika familia. Andaa taarifa fupi inayobainisha namna nzuri ya kuitumia ili ilete maendeleo na kisha wasilisha darasani kwa majadiliano zaidi.

### Faida za kushiriki katika shughuli za kijamii

Mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kijamii hujenga uwezo wa kujiamini na kujituma katika shughuli mbalimbali za kijamii na kuwa mfano bora wa kuigwa. Baadhi ya faida za kushiriki katika shughuli za kijamii ni kama zifuatavyo:

(a) **Kumjengea mwanafunzi maarifa na ujuzi mpya:** Kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii, humpatia mwanafunzi maarifa na ujuzi mpya. Ushiriki katika shughuli za uzalishaji mali, ujenzi wa miundombinu na kutunza mazingira, humsaidia mwanafunzi kujua njia mbalimbali na bora za utendaji wa majukumu hayo. Kwa mfano, kama mwanafunzi atashiriki katika shughuli za kilimo, atapata maarifa zaidi juu ya namna mazao yanavyozalishwa shambani.

(b) **Kukuza uhusiano mzuri baina ya mwanafunzi na jamii yake:** Mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kijamii na zile za uzalishaji mali, humsaidia kufahamika na kuaminika. Pia, hutambuliwa na wanajamii na hivyo kuwa na uwanja mpana wa kushirikishwa katika fursa mbalimbali za kimaendeleo.

(c) **Kujenga ari ya kujitolea na kufanya kazi za maendeleo:** Kushiriki kwa mwanafunzi katika shughuli mbalimbali katika jamii, humsaidia kuwa na juhudi na moyo wa kujitolea katika kufanya shughuli zinazochochea maendeleo na uzalishaji mali kwenye jamii.

(d) **Kumjengea mwanafunzi tabia ya kutumia muda ipasavyo:** Ushiriki katika shughuli za kijamii humfanya mwanafunzi kujenga mazoea na uwezo mzuri wa kutumia muda wake vizuri. Ili kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali kama kilimo, uvuvi na ufugaji, mwanafunzi atapaswa kutumia vizuri muda wake baada ya masomo, wakati wa mapumziko au wakati wa likizo. Hali hii humfanya mwanafunzi kutekeleza majukumu ya kimasomo kwa wakati ili aweze kupata wasaa wa kushiriki katika shughuli za kijamii.

(e) **Husaidia kuoanisha nadharia na vitendo:** Kupitia kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii, mwanafunzi huweza kupata wasaa mzuri wa kuoanisha maarifa aliyoyapata kinadharia darasani na vitendo halisi katika uzalishaji mali. Kwa njia hii huweka katika vitendo ujuzi



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY

alioupata darasani. DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

1. Taja faida tano za kushiriki katika shughuli za maendeleo.
2. Eleza kwanini ushiriki wako katika shughuli za kijamii hukusaidia kutumia muda ipasavyo.
3. Je, ni kwanini unaweza kuaminika na jamii iwapo utashiriki katika shughuli za kijamii?
4. Eleza jinsi ushiriki wako katika shughuli za kijamii unavyokuwezesha kuoanisha nadharia na vitendo.

### Kazi ya kufanya namba 3



Jadiliana na wanafunzi wenzako katika kikundi kuhusu rasilimali iliyopo kwenye mazingira ya jamii mnamoishi. Kisha eleza jinsi mtakavyoitumia kutekeleza majukumu yenu ya kijamii.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 4

**A:** Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi.

1. Mwanafunzi anatakiwa ahudhurie shule na kushiriki katika kutekeleza majukumu katika jamii anamoishi. __________
2. Kitendo cha mwanafunzi kusaidia kazi shuleni ni namna mojawapo ya kushiriki katika kutekeleza majukumu katika jamii yake. ________
3. Kushiriki katika shughuli za ujenzi wa miundombinu ya shule ni kupoteza muda wa masomo .__________
4. Kushiriki katika kufundisha wanajamii kusoma, kuandika na kuhesabu ni jukumu la mwanafunzi tu. __________
5. Fedha, muda, watu, mifugo na vyombo vya usafiri ni rasilimali. __________



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 70 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B:** Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake kwenye kisanduku.

6. Kulisha mifugo bila kuathiri mazingira ni mojawapo ya namna mwanafunzi anavyoweza kushiriki katika kutoa huduma gani?
   (a) huduma binafsi
   (b) huduma za shule
   (c) huduma za jamii
   (d) huduma za Serikali

7. Mwanafunzi anawezaje kushiriki kazi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara?
   (a) kuendesha mitambo ya kujenga barabara
   (b) kulima barabara na kufukia mashimo katikati ya barabara
   (c) kukagua na kubaini mashimo ya barabara tu
   (d) kuwaelimisha mafundi ujenzi namna ya kujenga barabara

8. Kutunza vyanzo vya maji kama mito, maziwa na bahari huleta faida gani katika jamii?
   (a) husaidia wasiojiweza kupata huduma za maji
   (b) kufanya maji yaishe haraka ili kutafuta vyanzo vingine
   (c) kuongeza wigo wa upatikanaji wa maji ya uhakika
   (d) hupunguza upatikanaji wa maji na shughuli za uzalishaji mali

9. Ipi kati ya zifuatazo si faida ya kushiriki kutekeleza majukumu katika jamii?
   (a) kujenga ari ya kujitolea
   (b) kujenga maarifa na ujuzi mpya
   (c) kuongeza utengano katika jamii
   (d) kujenga tabia ya kutumia muda ipasavyo

10. Ipi kati ya yafuatayo siyo matumizi sahihi ya fedha kwa mwanafunzi kutekeleza majukumu yake katika jamii?
   (a) kutumia fedha kwa ajili ya matembezi na kula vyakula vizuri
   (b) kuanzisha shughuli mbalimbali za uzalishaji mali kama kilimo
   (c) kununulia vifaa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za kilimo
   (d) kutumia fedha kujifunza mafunzo ya ujasiriamali ili kupata maarifa ya uwekezaji

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 71 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C:** Oanisha kipengele kutoka **Sehemu A** na maneno yaliyopo **Sehemu B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.

| Sehemu A | Jibu | Sehemu B |
|---|---|---|
| 11. Kutoa vyakula kwa wahitaji | | (a) kushiriki katika maendeleo ya jamii |
| 12. Watu | | (b) faida ya kushiriki katika shughuli za kijamii |
| 13. Kujenga umoja katika jamii | | (c) barabara, madaraja, reli, madarasa, ofisi, masoko na vyoo |
| 14. Miundombinu | | (d) kushiriki katika kutoa huduma za jamii |
| 15. Uzalendo | | (e) rasilimali ambazo mwanafunzi anaweza kuzitumia kutekeleza majukumu katika jamii yake |
| | | (f) kujitoa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili kuiletea jamii yako maendeleo |
| | | (g) madarasa, barabara, maziwa, reli na ofisi |

**Msamiati**

Ari   juhudi anazoonesha mtu katika kutekeleza jambo

FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nane

## Kutii sheria na kanuni

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza kutambua sheria za nchi, kuzifuata na kuoanisha utekelezaji wa sheria na kanuni katika maisha. Pia, ulijifunza umuhimu wa kuhoji sheria na kanuni zilizopo na kutathmini hatua zinazochukuliwa kudhibiti uvunjifu wa sheria. Katika sura hii, utajifunza kutii sheria na kanuni za mitandao ya mawasiliano. Vilevile, utajifunza namna ya kuepuka uhalifu mtandaoni na kushiriki kuelimisha jamii juu ya matumizi sahihi ya mitandao ya mawasiliano. Maarifa na ujuzi utakaopata katika sura hii, utakusaidia kutii sheria na kanuni za matumizi sahihi ya mitandao ya mawasiliano na kuepuka matumizi yasiyo sahihi ya mitandao ya mawasiliano.*



**Fikiri**

Ukiwa kiongozi halafu ukaona mtu anavunja sheria, utachukua hatua gani?

### Maana ya sheria

Sheria ni mfumo wa kanuni na taratibu zilizowekwa na mamlaka kwenye jamii kwa ajili ya kuongoza matendo na uhusiano miongoni mwa wanajamii. Pia, ni utaratibu unaotengeneza mfumo au mwelekeo wa maisha chini ya mamlaka husika. Sheria na kanuni zipo hata kwenye ngazi ya familia. Kwa mfano, kwenye baadhi ya familia, muda wa mwisho kurejea nyumbani ni saa mbili usiku. Vivyo hivyo, taasisi za kiserikali na asasi zisizo za kiserikali, zimejiwekea sheria na kanuni zinazowaongoza katika utendaji wake. Kwa mfano, shule zina sheria zinazowahusu wanafunzi, walimu na wafanyakazi wengine. Kulingana na sheria na kanuni zilizopitishwa, mtu anayezivunja au kuzikiuka hukabiliwa na adhabu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 1**



Katika kikundi cha wanafunzi wasiozidi sita, chunguza na andika; kisha wasilisha darasani kuhusu sheria zifuatazo:

(a) Sheria zote za shule zinazowahusu wanafunzi.
(b) Sheria ndogondogo zinazowahusu wanajamii katika kijiji au mtaa wako.

## Sheria ya Makosa ya Mtandao

Sheria ya Makosa ya Mtandao ni kanuni na taratibu zilizotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kudhibiti na kuratibu matumizi sahihi ya mawasiliano yote ya mitandao nchini Tanzania. Sheria hii ilipitishwa na Bunge tarehe 1 Aprili, 2015 na kuidhinishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 25 Aprili, 2015. Sheria hii inabainisha makosa na adhabu ambazo zinatokana na matumizi mabaya ya mifumo ya kompyuta na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Sheria hii iliandaliwa baada ya matumizi ya TEHAMA kuongezeka kwa kasi sana hapa nchini.

Mtandao ni mfumo wa kompyuta na vifaa vingine vya kielektroniki vilivyounganishwa pamoja kwa ajili ya mawasiliano. Mfumo huu wa vifaa vya kielektroniki hurahisisha usafirishaji wa habari kwa haraka kutoka upande wa mtoa taarifa na kwenda kwa mpokea taarifa. Baadhi ya mitandao inayotumia mfumo wa kielektroniki ni pamoja na; tovuti, “Twitter”, “WhatsApp”, “Instagram”, “Facebook”, na “Youtube”.

## Matendo yanayoonesha kutii Sheria ya Makosa ya Mtandao

Baadhi ya matendo yanayoonesha utii wa Sheria ya Makosa ya Mtandao ni pamoja na:

(a) **Kutoa takwimu au taarifa sahihi:** Ili kuonesha utii wa Sheria ya Makosa ya Mtandao, ni sharti kutoa takwimu au taarifa zilizo sahihi. Ili kutekeleza hili ni muhimu kufanya juhudi na kupata takwimu au taarifa sahihi kutoka kwa mhusika mwenyewe au kwa mamlaka yenye jukumu hilo.

(b) **Kusambaza picha zenye maadili:** Katika sheria hii, ni kosa la jinai kuchapisha au kusambaza picha za ngono au picha zozote zinazodhalilisha utu au hadhi ya binadamu. Ili kutii sheria hii, ni muhimu kuhakikisha kwamba unasambaza picha zenye maadili ambazo zinaheshimu na kulinda hadhi na utu wa binadamu. Kwa mfano, kusambaza picha za watu waliokufa kwenye ajali au walioungua moto si kitendo cha



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 74 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuheshimu hadhi yao.

(c) **Kuheshimu usawa wa binadamu:** Kwa mujibu wa sheria hii ni kosa la jinai kutengeneza taarifa zinazolenga kudhalilisha watu na kuwabagua kwa misingi ya rangi, ukabila, dini au mahali wanakotoka. Ili kutii sheria hii, ni muhimu kuheshimu haki za binadamu. Ni lazima kujua kwamba binadamu wote ni sawa na kwamba hakuna watu walio bora kuliko wengine.

(d) **Kuandaa na kutuma ujumbe sahihi:** Sheria ya Makosa ya Mtandao inapiga marufuku kuanzisha au kuzambaza ujumbe usio sahihi wala rasmi kwa lengo la kudanganya jamii kwa manufaa binafsi. Ili kutii sheria hii, ni lazima kuandaa na kusambaza ujumbe ulio sahihi na rasmi tu na usio na lengo la kudanganya au kupotosha jamii.

(e) **Utunzaji wa siri:** Sheria ya Makosa ya Mtandao inapiga marufuku kutoa bila idhini taarifa za kiupelelezi au uchunguzi. Ili kutii kipengele hiki cha sheria, ni muhimu kujiepusha na usambazaji wa taarifa hizi ambazo hupaswa kuwa siri na hutolewa na mamlaka husika tu kama vile Jeshi la Polisi au Mahakama.

Mtu yeyote anayetoa takwimu au taarifa sahihi, anayesambaza picha zenye maadili, anayeheshimu usawa wa binadamu, anayetuma ujumbe sahihi na anayetunza siri atakuwa ametenda matendo yanayoonesha kutii Sheria ya Makosa ya Mtandao.

**Zoezi la 1**

1. Eleza kwa kifupi maana ya Sheria ya Makosa ya Mtandao.
2. Kwanini ni kosa la jinai kwa mtu kutumia taarifa za siri za Serikali, taasisi au asasi za watu binafsi?
3. Jadili matumizi ya mitandao na athari zake kwa jamii, hususan kwa vijana.

**Kazi ya kufanya namba 2**



Mkiwa katika kundi la darasa zima, tembeleeni taasisi za Serikali kama vile Mahakama, Kituo cha Polisi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa au Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ili kupata taarifa juu ya makosa ya mitandao ya mawasiliano. Kisha katika kikundi cha wanafunzi watano andaeni na wasilisheni taarifa darasani baada ya wiki moja.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 75 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Umuhimu wa Sheria ya Makosa ya Mtandao

Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 ina umuhimu ufuatao:

(a) Kuzuia udhalilishaji kwa viongozi wa Serikali na watu binafsi;
(b) Kuzuia au kudhibiti vitendo viovu kama wizi, uhalifu, biashara haramu na ukiukwaji wa haki za binadamu;
(c) Kuelimisha jamii juu ya usalama na amani ndani ya nchi; na
(d) Kujenga uhusiano mwema miongoni mwa wananchi na kati ya wananchi na Serikali.

### Njia za kuepuka kufanya makosa wakati wa kutumia mitandao ya mawasiliano

Mtu yeyote ambaye anamiliki kifaa cha mawasiliano ya mtandaoni hana budi kujifunza sheria, kanuni na jinsi ya kutumia kifaa hicho cha mawasiliano kwa usahihi. Ni muhimu kila mtu kusoma na kuelewa sheria ya matumizi ya mitandao iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2015. Hivyo, kila mtumiaji hana budi kutii sheria na kanuni hizo bila shuruti ili kuepuka kushtakiwa na kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria.

Njia nyingine ya kuepuka kufanya makosa ya jinai ni kubaini mtoaji na mpokeaji sahihi wa taarifa. Hatua hii itasaidia mtu asitoe au kusambaza taarifa kutoka kwenye chanzo asichokielewa. Inapotokea kuwa mtu amepokea taarifa anayohisi siyo rasmi anashauriwa kutoituma kwa wengine na anapaswa kuifuta mara moja.

Ni muhimu kuhakiki usahihi wa taarifa kabla ya kuzituma taarifa hizo. Kubaini usahihi wa taarifa uliyoipokea kabla ya kuisambaza kutamuweka mtuma taarifa katika hali ya usalama, yeye binafsi na jamii kwa ujumla.

**Zoezi la 2**

1. Eleza kwa ufupi kwanini ni muhimu kujua sheria na kanuni za mitandao ya mawasiliano.
2. Fafanua umuhimu wa kuhakiki usahihi wa taarifa kabla ya kusambaza.
3. Taja njia nne za kuepuka kutenda makosa ya mitandao ya mawasiliano.
4. Eleza hatua utakazochukua iwapo utagundua mtu anatumia

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mawasiliano kwa njia ya mtandao kusambaza taarifa za upotoshaji.

5. Taja mfano wa umuhimu mwingine wa kuwa na Sheria ya Makosa ya Mtandao ambao haukutajwa hapo juu.

**Kazi ya kufanya namba 3**

Jadiliana na wanafunzi wenzako namna mitandao ya mawasiliano inavyosababisha mmomonyoko wa maadili katika jamii unamoishi.

## Faida za mitandao ya mawasiliano

Mawasiliano ni upashanaji habari au taarifa kwa njia ya mdomo, barua, simu, baruapepe, redio, televisheni, magazeti, ishara, na lugha ya alama. Pia, mawasiliano yanamaanisha njia wanazotumia watu au zinazowawezesha watu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

Mitandao imekuwa chombo muhimu sana cha upashanaji habari au taarifa mbalimbali kama elimu ya afya, misiba, maafa au majanga mbalimbali. Hali hii imeleta maendeleo ya mawasiliano baina ya watu na taasisi kwa kurahisisha utumaji na upokeaji wa taarifa kwa haraka na gharama nafuu.

Kupitia huduma zitolewazo na makampuni ya mawasiliano, watu hufanya miamala ya pesa kwa njia ya mitandao kama vile T-Pesa, M-Pesa, Tigo Pesa, “Airtel Money”, Halo Pesa, na “Easy” Pesa. Wafanyabiashara na wateja wao wanapata urahisi wa kufanya biashara. Faida nyingine ya mitandao ya mawasiliano ni kuwawezesha wafanyabiashara kutangaza kwa haraka na kwa watu wengi upatikanaji wa bidhaa mbalimbali.

Mitandao ya mawasiliano huimarisha udugu katika jamii na huchangia kujenga urafiki kwa kuwa na mawasiliano ya mara kwa mara. Aidha, upashanaji wa habari kwa haraka husaidia kazi ya ulinzi na usalama, na hupunguza safari zisizo za lazima.

**zoezi la 3**

1. Eleza kwa ufupi jinsi matumizi sahihi ya mitandao ya mawasiliano yanavyorahisisha maendeleo katika jamii.
2. Ni kwa jinsi gani mitandao ya mawasiliano inaweza kuimarisha umoja na mshikamano katika jamii?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Taja faida za kijamii zitokanazo na mitandao ya mawasiliano nchini.

**Kazi za kufanya namba 4**

Fanya uchunguzi jinsi mitandao ya mawasiliano inavyokuza uchumi wa wananchi katika eneo unaloishi. Kisha andika taarifa fupi kwenye daftari lako la mazoezi.

## Njia za kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mitandao ya mawasiliano

Kuna njia mbalimbali zinazoweza kutumika kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mitandao ya mawasiliano. Njia zifuatazo ni muhimu kulingana na mazingira ya Tanzania:

(a) **Kupitia makundirika:** Njia hii ni rahisi kuwafikia watumiaji wa mitandao ya mawasiliano, kwani watu wa kundirika moja ni rahisi kuelimishana wao kwa wao kutokana na kuwa na utashi unaofanana. Kwa mfano, kundi la vijana wenye umri kati ya 18-35, ni watumiaji wakubwa wa simu na mitandao. Hivyo, elimu kwa kundi hili la vijana ni muhimu ili kuepuka makosa na matumizi mabaya ya mitandao ya mawasiliano.

(b) **Kutumia machapisho kutoka vyombo vya habari na mamlaka ya mawasiliano:** Machapisho ya taasisi hizi hutoa maelezo juu ya matumizi sahihi ya mitandao ya mawasiliano. Kwa mfano, machapisho yanaweza kuwa na taarifa juu ya habari zipi hazipaswi kuwekwa au kusambazwa katika mitandao. Vyombo hivyo ni pamoja na magazeti, redio, televisheni na mitandao ya kijamii.

(c) **Semina, ziara, mikutano, midahalo, na makongamano:** Njia hizi huwezesha kufikisha elimu au ujumbe kwa haraka juu ya matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii. Semina na makongamano, midahalo na mikutano huwa na makundi makubwa ya watu hivyo kusaidia kufikisha ujumbe kwa urahisi. Njia nyingine ni kutembelea ofisi za mamlaka zinazohusika na mawasiliano ili kupata taarifa sahihi.

(d) **Madhehebu ya dini na vikundi vya utamaduni na sanaa:** Taasisi hizi ni muhimu zitumike ili kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii. Madhehebu ya dini ni rahisi kutoa elimu kwani wafuasi wanaamini na kufuata mafundisho yanayotolewa na viongozi wao. Vilevile, vikundi vya utamaduni na sanaa ni rahisi kufikisha ujumbe kuhusu matumizi sahihi ya mitandao kwa kuwa watu wengi wanavutiwa na kazi za sanaa.



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 78 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

1. Je, kutumia semina, mikutano, midahalo na makongamano kunawezaje kutoa elimu sahihi ya matumizi ya mitandao ya mawasiliano?
2. Ni namna gani mitandao ya kijamii kama vile “Twitter” au “Instagram” inaweza kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mitandao kwa jamii?
3. Eleza kwa nini makundirika ni muhimu katika mchakato wa elimu ya matumizi sahihi ya mitandao ya mawasiliano.

## Zoezi la 5

**A.** Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi.

1. Kupiga na kusambaza picha zisizo na maadili ya Kitanzania mitandaoni ni kosa la jinai.__________
2. Kuzijua na kuzitekeleza sheria na kanuni zinazohusu mitandao siyo njia sahihi ya kuepuka kufanya makosa ya mitandao ya mawasiliano.__________
3. Kudumisha mawasiliano katika jamii ni mojawapo ya hasara ya matumizi ya mitandao ya kijamii.__________
4. Kutii sheria na kanuni ni njia ya kuepusha makosa ya mitandao ya mawasiliano.__________
5. Mitandao ni mfumo wa mawasiliano unaoruhusu watu kuwasiliana kwa kutumia ujumbe mfupi wa maandishi, picha au video.__________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B.** Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake kwenye kisanduku.

6. Kuwa mwangalifu katika matumizi ya mitandao kuna faida gani katika jamii?
   (a) kutatua migogoro ya kifedha
   (b) kuboresha biashara zetu
   (c) kuepuka kuvunja sheria
   (d) kujitenga na watu

7. Ipi ni njia mojawapo ya kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mitandao ya mawasiliano?
   (a) midahalo na makongamano
   (b) kutoa huduma kwa wateja
   (c) kuheshimu matumizi sahihi ya dini zetu
   (d) kufuata sheria za matumizi ya mitandao

8. Ipi kati ya njia zifuatazo ni sahihi kuepuka kufanya makosa ya mitandao ya mawasiliano?
   (a) kufungua kesi polisi
   (b) kutii sheria na kanuni
   (c) kutotumia mitandao
   (d) kutotumia simu za mikononi

9. Ipi kati ya zifuatazo ni faida ya matumizi sahihi ya mitandao ya mawasiliano?
   (a) kurahisisha kutoa na kupata taarifa
   (b) kurahisisha kupata ajira kwa vijana kwa njia ya mkato
   (c) kurahisisha kupata maadui wengi
   (d) kurahisisha kutofanya kazi

10. Ipi kati ya zifuatazo ni maana sahihi ya neno mawasiliano?
   (a) mfumo wa kupashana habari na ujumbe
   (b) taaluma ya utafutaji habari
   (c) kazi za kujitolea kutafuta habari
   (d) mfumo wa kujua habari zilizofichwa

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 80 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C**. Oanisha kipengele kutoka **Sehemu A** na maneno yaliyopo **Sehemu B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.

| Sehemu A | Jibu | Sehemu B |
|---|---|---|
| 11. Mitandao ya kijamii | | (a) elimu ya matumizi sahihi ya mitandao |
| 12. Kosa la mtandao wa mawasiliano | | (b) "Twitter","Instagram","WhatsApp", "Youtube" |
| 13. Husaidia kazi ya ulinzi na usalama | | (c) kutumia lugha isiyofaa mitandaoni |
| 14. Sheria ya mtandao | | (d) matumizi sahihi ya mitandao ya mawasiliano |
| 15. Kuhakikisha usahihi wa taarifa kabla ya kutumia | | (e) njia ya kuepuka kufanya makosa ya mitandaoni |
| | | (f) kanuni na masharti ya kudhibiti matumizi ya mitandao ya mawasiliano |

**Msamiati**

Takwimu — data za kiidadi zinazodhihirisha ukweli wa jambo fulani

FOR ONLINE USE ONLY
FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 81 30/07/2021 20:42


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tisa

## Kujenga tabia ya uvumilivu

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza kutenda vitendo vya kuhimili changamoto zinazokukabili na kuhamasisha wengine kukabiliana na changamoto za maisha kwa kutumia uzoefu wako. Vilevile, ulijifunza namna ya kuishi kwa matumaini wakati unakabiliana na changamoto mbalimbali. Katika sura hii, utajifunza namna ya kujenga tabia ya uvumilivu na kutawala hisia na mihemko katika maisha yako. Maarifa na ujuzi utakaopata katika sura hii utakuwezesha kujenga tabia ya uvumilivu na kuwa mfano wa kuigwa na watu wengine.*



**Fikiri**

Waswahili husema “mvumilivu hula mbivu”. Maana yake ni nini?

### Kuvumilia katika maisha

Uvumilivu ni hali ya kustahimili matatizo na changamoto za maisha. Uvumilivu unajumuisha pia tabia ya kuwa na subira. Kwa mfano, ukiwa mwanafunzi, ili usome kuanzia Darasa la Kwanza hadi la Saba unahitaji kuvumilia kwa kipindi cha miaka saba. Utaamka asubuhi na kwenda shule na pia utafanya kazi unazopewa darasani na nyumbani. Vilevile, utafanya mitihani ya kila muhula wa masomo na mitihani ya majaribio ya ngazi ya mkoa na ya Taifa. Mwanafunzi anapovumilia, inamsaidia kumaliza elimu ya msingi na kuendelea na masomo ya sekondari endapo atakuwa amefaulu mtihani wake wa mwisho wa elimu ya msingi.

### Faida za kuwa mvumilivu

Unapokuwa mvumilivu katika maisha ya shule na nyumbani utapata faida mbalimbali. Zifuatazo ni baadhi ya faida za kuwa na uvumilivu katika maisha:

(a) **Kujenga uhusiano mzuri na wenzako:** Uvumilivu humsaidia mwanafunzi kuwa na uhusiano mzuri na wenzake. Hii ni kutokana na kwamba uvumilivu humfanya mtu kutopinga wengine kwa kutumia lugha na kauli za ukali na hivyo kuepuka ugomvi usio na sababu. Hali hii husababisha kusameheana na kuwa na uhusiano mzuri.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 82 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) **Hudumisha mitazamo chanya ya mafanikio:** Uvumilivu humsaidia mwanafunzi kuwa na mtazamo chanya katika kutafuta mafanikio. Uvumilivu hujenga hali ya kujiamini kuwa ukifanya kazi na kutimiza lengo, utafanikiwa na kutimiza ndoto zako. Kwa mfano, mwanafunzi anayestahimili kuamka mapema kila siku ili awahi shuleni, anakuwa anaamini kuwa uvumilivu huo utamwezesha kuhudhuria vipindi vyote na kupata muda wa kufanya kazi zote za shule na hatimaye kufaulu vizuri mitihani yake yote.

(c) **Kuweza kufanya uamuzi sahihi:** Uvumilivu humsaidia mwanafunzi kufanya uamuzi sahihi juu ya kuendelea au kutokuendelea na jambo fulani. Hali ya uvumilivu husaidia kupata muda wa kutosha wa kufikiri na kutafuta majibu ya changamoto zinazomkabili. Kwa mfano, mwanafunzi anapokutana na masomo magumu anatakiwa kutafuta njia mbadala badala ya kuacha shule.

(d) **Kuweza kufikia malengo:** Uvumilivu humwezesha mtu kuyafikia malengo yake kwa wakati. Hii inatokana na kuwa na uamuzi sahihi na kufanya kazi kwa bidii. Kwa mfano, mwanafunzi anapoanza Darasa la Kwanza, akakutana na changamoto ya ugumu wa masomo, lakini akiamua kuvumilia na kumsikiliza mwalimu itamwezesha kumaliza Darasa la Saba kwa mafanikio.

(e) **Kujifunza mambo mapya:** Uvumilivu humfanya mtu kuheshimu na kusikiliza mawazo ya wengine. Kwa kusikiliza wengine mtu anaweza kujifunza mambo mapya.

### Zoezi la 1

1. Nini maana ya uvumilivu?
2. Bainisha ni kwa jinsi gani uvumilivu unaweza kukusaidia kufikia malengo yako kwa wakati.
3. Ainisha faida tano za kuwa na uvumilivu katika maisha ya kila siku.
4. Taja matatizo mawili uliyokumbana nayo ukiwa katika mazingira ya nyumbani na eleza jinsi ulivyoweza kuyavumilia.


FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 83 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 1**



Katika kikundi cha wanafunzi watano, chunguza tatizo kubwa mnalokabiliana nalo hapo shuleni na ambalo linahitaji uvumilivu kabla ya kulitatua. Fanyeni tathmini jinsi gani mnaweza kuvumilia na kukabiliana nalo ili kumaliza shule vizuri na kwa mafanikio. Wasilisha tathmini yenu darasani kwa majadiliano zaidi.

### Vitendo vinavyoonesha uvumilivu

Mtu mwenye uvumilivu huonesha vitendo mbalimbali katika kukabiliana na changamoto zinazomkabili. Vifuatavyo ni vitendo vya uvumilivu ambavyo mwanafunzi anapaswa kuvionesha pale anapopungukiwa na mahitaji:

(a) **Kuepuka kuandaa, kushawishi na kufanya migomo:** Unapokuwa na mahitaji ambayo hayajatimizwa, ni muhimu kuwa mvumilivu. Uvumilivu utakuepusha kuandaa, kujiunga, au kushawishi wenzako kufanya migomo inayochochea uvunjifu wa amani katika jamii. Kwa mfano, shule huwapa wanafunzi uji kila asubuhi wakati wa mapumziko, lakini siku moja haukupikwa kutokana na tatizo la unga kuchelewa kuletwa shuleni au maji kukatika. Katika dharura kama hii, haupaswi kuwashawishi wanafunzi wenzako kugoma na kufanya vurugu. Badala yake unatakiwa kuvumilia kwani uji utapikwa baada ya unga kufika au maji kupatikana.

(b) **Kufuata sheria, kanuni na taratibu za kuwasilisha malalamiko kwa vyombo vinavyohusika:** Unapokosa mahitaji ambayo ni haki yako kutoka kwa mtu mwingine au taasisi fulani, ni vyema kuwa mvumilivu na kufuata sheria, kanuni na taratibu. Hii itakusaidia kuwasilisha malalamiko yako kwenye vyombo vinavyohusika. Kwa mfano, umemwazima mwanafunzi mwenzako kitabu na hataki kukurudishia, si vyema kulipiza kisasi kwa kumpiga, badala yake unapaswa kumshitaki kwa mwalimu ili amchukulie hatua za kinidhamu.

(c) **Kuwa na subira:** Unapopungukiwa na mahitaji ya lazima, ni muhimu kuvuta subira wakati unaendelea kutafuta njia mbadala za kupata mahitaji hayo. Kwa mfano, mwanafunzi anapoahidiwa zawadi baada ya kufanya vizuri katika masomo hana budi kuwa na subira hadi zawadi hiyo itakapotolewa. Subira husaidia kupata muda wa kutosha kutafuta njia za kufanikisha upatikanaji wa mahitaji hayo.

(d) **Kuwa na tabia ya kuomba na kutoa msamaha kwa wengine:** Tunapokosea ni muhimu kuomba msamaha kwa tuliowakosea hata kama ni wadogo kwa umri. Kuomba msamaha huonesha uvumilivu

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 84 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kwako. Pia, yule anayekusamehe anakubali kuvumilia. Tunapokosewa na wengine ni muhimu kuvumilia hasa pale wanapoomba msamaha. Ni vyema kusamehe hata kama mtu aliyekukosea hakuomba msamaha. Msamaha husaidia kujenga uelewano mpya baada ya kosa au makosa kutokea.

**Zoezi la 2**

1. Kwanini tunahitaji kuwa na subira katika maisha?
2. Eleza umuhimu wa msamaha katika jamii.
3. Fafanua ni kwa namna gani uvumilivu unaweza kuondoa tabia ya kulipiza kisasi katika jamii.
4. Kwanini kufuata sheria, kanuni na taratibu ni kitendo cha uvumilivu?

### Matumizi ya njia mbadala katika kutatua tatizo

Matatizo ni sehemu ya maisha ya binadamu kwani hayakwepeki. Ili kutatua tatizo linalokukabili, ni muhimu kuwa na namna mbalimbali za utatuzi. Jambo la kwanza ni kubainisha kiini au chanzo cha tatizo. Baada ya kubainisha chanzo cha tatizo, jambo linalofuata ni kuonesha ukubwa wa tatizo, rasilimali na muda unaohitajika kulitatua. Hatua nyingine ni kutafuta njia za kutatua tatizo hilo. Aghalabu, kutakuwa na njia mbalimbali za kutatua tatizo linalokukabili, hivyo itakubidi kuchagua njia mojawapo kati ya hizo. Njia utakayochagua kutatua tatizo linalokukabili itakuwa njia ya awali ya utatuzi wa tatizo.

Njia ya awali ni namna ya kwanza mtu anayofikiri itamsaidia kutatua tatizo linalomkabili mara tu linapotokea. Mara nyingi njia za awali huja kutokana na uzito wa tatizo lenyewe. Kwa mfano, kama mwanafunzi hafanyi vizuri darasani, njia ya awali ya kutatua tatizo hili ni kutafuta vitabu vingi vya kumsaidia kufanya mazoezi. Endapo njia ya awali itashindwa kutatua tatizo na hivyo mwanafunzi kuendelea kufanya vibaya darasani, njia mbadala itahitajika.

Njia mbadala ni namna nyingine inayomwezesha mtu kupata ufumbuzi wa tatizo linalomkabili baada ya njia iliyochaguliwa awali kushindwa kutatua tatizo. Kwa mfano, mwanafunzi alikuwa na tatizo la kusinzia darasani wakati mwalimu anafundisha, mwalimu aliamua kumuweka dawati la mbele ili amwone kwa karibu. Lakini mwanafunzi huyo hakuweza kuacha kusinzia darasani, hivyo



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mwalimu akaamua kutumia njia mbadala ambayo ni kuwaweka wanafunzi katika vikundi na kuwapa kazi ya kujadiliana. Hatimaye, mwanafunzi huyo aliacha kusinzia darasani. Hivyo, njia mbadala, inaweza kuwa na matokeo mazuri na kutatua tatizo linalomkabili mwanafunzi katika mazingira yake ya kujifunza.

### Mambo ya kuzingatia katika kutumia njia mbadala

Katika kutumia njia mbadala kutatua tatizo, ni muhimu kuzingatia baadhi ya mambo ikiwa ni pamoja na:

(a) **Kutafakari kwa kina tatizo linalokukabili:** Ili kutumia njia mbadala kutatua tatizo ni muhimu kufikiri na kujua vizuri tatizo linalokukabili. Hii husaidia kubaini chanzo, uzito na matokeo yanayoweza kutokea baada ya kutumia njia mbadala.

(b) **Kubuni njia mbadala za kutatua tatizo lililojitokeza:** Katika kutatua tatizo, buni njia mbadala itakayotumika pindi njia ya awali inapokwama. Njia mbadala ni muhimu kwani humfanya mtu anayekabiliwa na tatizo kuweza kupata ufumbuzi.

(c) **Kutathmini juu ya uzuri na ubaya wa njia mbadala:** Inashauriwa kujua uzuri na ubaya wa njia mbadala ulizoainisha katika kutatua tatizo. Ni muhimu kutathmini faida na hasara za kila mbinu ya utatuzi wa tatizo ili kuchagua njia iliyo sahihi kulingana na tatizo linalokukabili. Kujua faida na hasara za njia za utatuzi wa tatizo husaidia kufanya uamuzi sahihi kukabiliana na tatizo lililopo.

(d) **Kulinganisha njia mbadala na uwezo wa kuzitumia:** Inashauriwa kupima uwezo wa kutumia njia hizo, kisha chagua njia moja itakayokuwa rahisi kwako. Ni lazima kuchagua njia ambayo unauwezo wa kuitumia. Uwezo huu lazima uangalie kiwango cha ujuzi wa mtu ili kuweza kustahimili matumizi ya njia mbadala na utayari wa kuzikabili faida na hasara zake.

(e) **Kulinganisha rasilimali zilizopo kama zinaendana na njia uliyoichagua:** Inashauriwa kutafakari na kulinganisha muda na rasilimali zilizopo kama zinakidhi mahitaji ya njia iliyochaguliwa. Hii itasaidia kuchagua njia unayomudu kuitumia vizuri kulingana na rasilimali ulizonazo.

(f) **Kutumia njia mbadala iliyochaguliwa kati ya nyingi:** Ni muhimu kuchagua njia moja tu ambayo utaimudu kulingana na ujuzi na uwezo wa kifedha. Hii itakusaidia kuchagua njia mbadala unayoweza kuitumia na kuleta matokeo chanya. Baada ya kuchagua njia mbadala, anza

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuitumia na kutathmini matokeo ya njia hiyo. Kama njia iliyochaguliwa haina matokeo mazuri, unaweza kuiacha ama kuchagua njia nyingine.

### Zoezi la 3

1. Eleza maana ya njia mbadala.
2. Fafanua umuhimu wa kuwa na njia mbadala katika kutatua tatizo.
3. Kwanini ni muhimu kubaini kiini cha tatizo kabla ya kuchagua njia mbadala ya kutumia kutatua tatizo husika?
4. Bainisha umuhimu wa kulinganisha uwezo wa rasilimali na njia uliyoichagua kutatua tatizo.
5. Eleza ni kwa nini tathmini huhitajika ili kubaini uzuri na ubaya wa njia ya kutatua tatizo.

### Kazi ya kufanya namba 2

Jadiliana na wanafunzi wenzako katika kikundi na bainisha njia tano tofauti mbadala za kutatua tatizo la uharibifu wa madawati shuleni kwenu. Andika njia hizo katika daftari lako la mazoezi.

## Kutawala hisia na mihemko katika maisha

Hisia ni uwezo wa kiumbe, kutambua kuwapo kwa kitu au hali fulani kupitia ung'amuzi wa mwili au akili. Akili ya binadamu ina uwezo wa kubaini, kutafakari na kuchanganua juu ya jambo lililotokea na madhara yake. Kwa mfano, mtu anapofiwa na mtu wake wa karibu mfano mzazi wake, mwenza au rafiki hupata hisia kali juu ya kumpoteza mtu huyo. Wakati mwingine baadhi ya watu hushindwa kuzuia hisia zao kwani husikitika na kulia sana na hata kufikia kiwango cha kuzimia.

Mihemko ni hali ya mtu kuwa na hisia kali kama vile hasira, ashiki, hamu au woga. Mihemko husababisha hamu kubwa ya kufanya jambo na mara nyingi huisha baada ya kufanya jambo hilo. Hisia na mihemko humfanya mtu kuamua haraka na wakati mwingine kuchukua hatua ambazo ni hatarishi katika maisha. Kwa mfano, mtu anapomkamata mwizi akimwibia, kutokana na hasira, anaweza kumpiga na kumjeruhi au hata kumuua. Athari zake



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 87 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ni kwamba mtu aliyeua au kujeruhi atafunguliwa mashtaka ya kujeruhi au mauaji. Si vema kufanya uamuzi ukiwa na mhemko.

### Umuhimu wa kutawala hisia na mihemko katika maisha

Katika maisha ya kila siku, kila mtu anatakiwa kujifunza jinsi ya kutawala hisia na mihemko yake ili aweze kuishi na wenzake vizuri. Hisia na mihemko isipotawaliwa, mhusika anaweza kuleta madhara makubwa kwa jamii. Vilevile, mtu aliyetawaliwa na hisia na mihemuko anaweza kufanya uamuzi wa kuwaumiza watu wengine na mhusika kupata athari kama kushitakiwa na kufungwa jela.

Kutawala hisia na mihemko humsaidia mtu kuwa na uwezo mkubwa wa kufanya tafakari kwa kina kabla ya kuchukua uamuzi wowote. Kufanya tafakari kwa kina humsaidia mtu kuainisha uzuri na ubaya wa uamuzi anaotaka kuchukua. Hii husaidia mtu kufanya uamuzi akiwa na utulivu wa akili na baada ya kutafakari vizuri faida na hasara za hatua atakayochukua. Kwa mfano, mtu mwenye uwezo wa kutawala hisia na mihemko anaweza kuepukana na kujiingiza kwenye tabia hatarishi kama uasherati na matumizi ya dawa za kulevya.

Pia, kutawala hisia na mihemko huweza kumsaidia mtu kuwa na uhusiano mzuri na watu wengine kutokana na uwezo wake wa kufanya uamuzi ambao hauleti matokeo hasi kwa jamii yake. Hali hii humfanya kupendwa na wenzake na hivyo kujenga uhusiano mzuri na wanafamilia, marafiki na jamii kwa ujumla. Vilevile, humsadia mtu kuheshimika kutokana na uwezo wake wa kutafakari kwa kina mambo anayokutana nayo na hivyo kufanya uamuzi ambao hauwezi kuathiri watu wengine. Wanajamii humheshimu mtu wa namna hiyo kwani uamuzi wake huungwa mkono na watu wengine.

**Zoezi la 4**

1. Bainisha tofauti kati ya hisia na mihemko.
2. Eleza umuhimu wa kutawala hisia na mihemuko katika kufikia uamuzi sahihi.
3. Ainisha faida tano za mtu kutawala hisia na mihemko katika jamii.
4. Fafanua ni kwa namna gani kutawala hisia na mihemko husaidia mtu kuwa na afya nzuri ya mwili na akili.



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 88 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 3**

Ni tukio gani ambalo lilishawahi kutokea katika maisha yako na kukufanya kupata hisia na mihemko? Andika katika daftari lako la mazoezi maelezo ya jinsi ulivyokabiliana nalo na matokeo yake.

### Stadi za kutawala hisia na mihemko

Zipo stadi mbalimbali ambazo mtu anahitaji ili aweze kutawala hisia na mihemko katika maisha ya kila siku. Zifuatazo ni baadhi ya stadi za kutawala na kukabiliana na hisia na mihemko:

(a) **Fanya mazoezi ya mwili na viungo:** Ili kuzitawala hisia na mihemko ni muhimu kujishughulisha kwa kufanya mazoezi ya viungo vya mwili. Kwa mfano, kucheza michezo mbalimbali kama vile mpira wa miguu, pete, wavu, kikapu na riadha humsaidia mwanafunzi kutumia muda vizuri. Mwanafunzi anapokaa bila majukumu hujenga hisia potofu katika akili yake na kupata mihemko itakayomletea madhara kiakili na kimwili. Kwa hiyo, kushiriki katika michezo ni suala muhimu kwa ustawi wa mwanafunzi na jamii inayomzunguka kwani inaepusha kujihusisha na matendo hatarishi.

(b) **Epuka mazingira hatarishi:** Ili kuzitawala hisia na mihemko ni vyema mwanafunzi aepuke maeneo ambayo huchochea hisia na mihemko. Maeneo kama vile baa, madanguro, maeneo wanapokaa wavuta bangi na maeneo mengine kama hayo ni hatarishi.

(c) **Shirikisha wenzako juu ya tatizo linalokukabili:** Ili kuepuka kutawaliwa na hisia na mihemko, ni muhimu kueleza tatizo linalokukabili ili upate msaada au ushauri kutoka kwa watu uliowashirikisha. Ni vyema kuwashirikisha watu unaowaamini na watu wenye uzoefu ambao walishawahi kupitia matatizo kama yako na hivyo wanajua njia mbalimbali za utatuzi.

(d) **Jenga mtazamo chanya kuwa unaweza kutatua tatizo linalokukabili:** Ni muhimu kujiamini kuwa unaweza kutatua tatizo linalokukabili na kuwasaidia wenzako kutatua matatizo yao. Hii itakusaidia kujenga mtazamo chanya ambao utakuwezesha kukabiliana na hisia na mihemko hasi katika jamii.

(e) **Hudhuria na zingatia mafundisho ya dini:** Ni muhimu kuhudhuria, kushiriki na kuzingatia mafundisho ya dini. Mafundisho ya dini husisitiza amani, upendo, mshikamano na kusamehe pale unapokuwa umekosewa na hivyo husaidia kupunguza hisia na mihemko.



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 89 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**(f) Tafuta taarifa muhimu na shiriki katika shughuli za kijamii:** Ni muhimu kupata muda wa kuchangamana pamoja na watu wengine na kufanya shughuli za kijamii kama vile kushiriki katika matukio ya huzuni na furaha. Pia, soma vitabu na machapisho mengine kama vile magazeti. Tumia muda wako kupata taarifa muhimu kwa njia za kutazama televisheni na kusikiliza redio. Vitendo hivi humsaidia mtu kuwa na mtazamo chanya katika jamii, hivyo kusaidia kupunguza na kutawala hisia na mihemko.

### Zoezi la 5

1. Eleza ni kwa jinsi gani unaweza kutawala hisia na mihemko.
2. Kwanini ni muhimu kumshirikisha mwenzako juu ya changamoto zako?
3. Eleza ni kwa jinsi gani mafundisho ya dini husaidia kuzitawala hisia na mihemko.
4. Kwanini tunashauriwa kuepuka mazingira hatarishi ili kuzitawala hisia na mihemko?

### Kazi ya kufanya namba 4



Katika kikundi cha wanafunzi watano, igiza kisamafunzo juu ya namna ya kuzitawala hisia na mihemko kwa wanafunzi wa shule ili kujiepusha na matendo hatarishi. Katika kuigiza kwenu, onesha namna ambavyo wanafunzi wanaweza kukwepa vishawishi vya kujiingiza katika matendo hatarishi.

### Zoezi la 6

**A:** Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi.

1. Uvumilivu ni hali ya kustahimili shida, taabu na matatizo.__________
2. Kujiamini na kuwasaidia wanafunzi wenzako kukabiliana na matatizo

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ni mtazamo hasi kwa walimu.__________

3. Kutawala hisia na mihemko ni njia mojawapo ya kuepuka vishawishi.__________

4. Kufuata sheria na taratibu ni njia mojawapo ya kuonesha uvumilivu.__________

5. Njia mbadala ni namna ya kufanya jambo baada ya kufanikiwa kwa njia ya awali.__________

**B:** Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake kwenye kisanduku.

6. Lipi kati ya majibu yafuatayo si faida ya uvumilivu?
   (a) hujenga busara
   (b) hujenga hofu
   (c) huchochea utulivu wa akili
   (d) husaidia kufanya uamuzi sahihi

7. Ipi kati ya zifuatazo si faida za kubuni njia mbadala katika kukabiliana na tatizo?
   (a) husaidia kutatua changamoto iliyoshindikana
   (b) husaidia kushughulikia tatizo lililokosa ufumbuzi
   (c) husaidia kupata utatuzi wa tatizo jipya
   (d) husaidia kupata muda wa ziada wa kujifurahisha na kutafakari

8. Ipi kati ya njia zifuatazo ni muhimu katika kutatua tatizo pindi njia ya awali inaposhindikana?
   (a) njia ya majadiliano
   (b) njia ya usuluhishi
   (c) njia mbadala
   (d) njia ya majibizano

9. Kwa nini mihemko humfanya mtu ashindwe kufanya uamuzi sahihi?
   (a) hutanguliza faida mbele

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) hana muda wa kufanya tathmini ya athari za uamuzi wake
(c) huongozwa na mihemko kutenda jambo
(d) hutafakari sana na kutenda jambo baadaye

10. Ipi kati ya zifuatazo si faida za kutawala hisia na mihemko katika maisha?
(a) hulinda afya ya mwili na akili
(b) huepusha madhara yanayoweza kujitokeza
(c) husaidia kufikia uamuzi sahihi
(d) hujenga wivu na chuki kwa aliyekuudhi

**C:** Oanisha kipengele kutoka **Sehemu A** na maneno yaliyopo **Sehemu B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.

| Sehemu A | Jibu | Sehemu B |
|---|---|---|
| 11. Kitendo cha uvumilivu | | (a) kutokuwa tayari kusikiliza wengine |
| 12. Mambo ya kuzingatia katika kutumia njia mbadala | | (b) namna ya kutatua tatizo |
| 13. Mihemko | | (c) namna ya kutawala hisia na mihemko |
| 14. Kujenga ujasiri katika utendaji | | (d) hisia kali anazokuwa nazo mtu kama jazba, woga au ashiki juu ya jambo fulani |
| 15. Kushirikisha wenzako juu ya tatizo linalokukabili | | (e) uwezo wa mtu kujibu athari yoyote kupitia ung'amuzi wa mwili, akili na moyo |
| | | (f) kuonesha tabia ya kuwa na subira |
| | | (g) kujua kiini cha tatizo, kuchagua njia mbadala na kuainisha rasilimali za kutatua tatizo |
| | | (h) faida za kutawala mihemko na hisia |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 92 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Ashiki | kupenda sana kitu au tamaa kubwa ya kujamiiana |
| Busara | uwezo wa kufikiria, kutenda na kufanya uamuzi wa mambo yanayofaa |
| Mbadala | kitu au jambo lingine linaloweza kutumika badala ya lile la awali |
| Subira | tabia ya kutokuwa na haraka katika kushughulikia suala hata baada ya kupatwa na jambo gumu |
| Uasherati | tabia ya mtu ya kupenda kufanya ngono mara kwa mara na watu ambao hana uhusiano nao wa kindoa |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 93 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi

## Jinsi ya kufikia malengo

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza umuhimu wa kubaini vipaumbele vyako na kuvizingatia. Pia, ulijifunza jinsi ya kutekeleza majukumu yako na kushuhudia ukweli kwa mifano dhahiri katika maisha yako ya kila siku. Aidha, ulijifunza tabia ya kupiga vita unafiki katika maisha. Katika sura hii, utajifunza umuhimu wa kujiwekea malengo katika maisha na jinsi ya kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kujiwekea malengo na kuyafikia kwa wakati. Maarifa na ujuzi utakaopata katika sura hii utakuwezesha kujenga tabia ya kuishi kwa kupanga na kufikia malengo yako. Aidha, utakuwa mshauri bora kwa jamii juu ya uwekaji wa malengo na utekelezaji wa mipango.*

**Fikiri**

Mwanafunzi mmoja alisema: "Mimi nataka kuwa miongoni mwa wanafunzi kumi bora katika Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba." Je, wewe ungemshauri nini?

### Maana ya malengo

Malengo ni dhamira au kusudio la kutekeleza jambo lililopangwa kwa kipindi au muda fulani. Ni jambo ambalo mtu anakusudia kulifanikisha. Mara nyingi malengo husukumwa na nia, tamaa, kiu au ndoto ya kufikia upeo au kikomo cha jambo lililokusudiwa. Malengo huenda pamoja na mpango mkakati unaoonesha hatua mahususi za jinsi ya kutimiza malengo katika muda mrefu au muda mfupi.

### Aina za malengo

Kuna aina kuu mbili za malengo. Aina hizi zinatofautiana kulingana na muda wa utekelezaji. Kuna malengo ya muda mfupi na malengo ya muda mrefu. Malengo ya muda mfupi ni sehemu ya malengo ya muda mrefu ambayo utekelezaji wake ni wa muda mfupi. Kwa mfano, kuwapima wanafunzi kitaaluma kila wiki



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 94 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

au mwezi. Malengo ya muda mrefu ni yale yanayokusudiwa kutekelezwa kwa muda mrefu, kwa mfano, kuwezesha wanafunzi kufaulu vizuri Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba. Lengo hili linaweza kuchukua miaka mingi.

### Njia bora za kutekeleza mipango ili kufikia malengo

Kujiwekea malengo kunaambatana na matarajio ya mtu katika maisha. Matarajio haya yanaweza kuwa ya kijamii, kiuchumi au kiimani. Ili malengo yaweze kufikiwa kwa wakati ni vyema kuchagua njia bora za kutekeleza mipango ya kufikia malengo hayo. Njia bora ya kufikia malengo ni kufuata hatua katika utekelezaji wa mipango. Hatua za utekelezaji wa mipango zimebainishwa hapa chini kama ifuatavyo:

(a) **Kuainisha shughuli muhimu za kufanya:** Ni muhimu kuainisha kazi muhimu utakazofanya ili kufanikisha malengo uliyojiwekea. Hii inahusisha kuchagua shughuli muhimu ambazo baada ya kuzifanya zitakuwezesha kufikia lengo ulilojiwekea. Uchaguzi wa shughuli utategemea aina ya tatizo linalokukabili katika masomo yako. Miongoni mwa shughuli zinazoweza kuchaguliwa ni pamoja na; kuandaa ratiba ya kujisomea, kununua au kutafuta vitabu vya masomo yote, kusoma mada mbalimbali kwa bidii, kufanya majadiliano na wanafunzi wengine na kuorodhesha njia za kutafuta msaada endapo utashindwa kuelewa baadhi ya mada katika masomo mbalimbali.

(b) **Kuainisha mahitaji muhimu:** Wakati wa utekelezaji wa mipango ni muhimu ukaainisha mahitaji muhimu ili uweze kutekeleza mipango yako uliyojiwekea. Mfano, kama malengo ya mwanafunzi ni kufaulu Mtihani wa Darasa la Saba, ni vizuri akaandaa mahitaji muhimu yatakayomwezesha kufanya vizuri katika masomo na hatimaye Mtihani wa Darasa la Saba. Kwa mfano, mahitaji muhimu yanaweza kuwa ni vitabu, madaftari, kalamu na penseli za kutosha, kuhudhuria vipindi darasani, pamoja na kujisomea kwa bidii.

(c) **Kuchagua mbinu za utekelezaji:** Katika kufikia malengo ni muhimu kuchagua mbinu sahihi za utekelezaji. Pamoja na kufundishwa darasani na mwalimu, mwanafunzi anaweza kutenga muda wa kujisomea mwenyewe kwenye mazingira tulivu, au kujadiliana na wenzake, na kufanya mazoezi binafsi. Kisha atampelekea mwalimu ili amsahihishie. Mbinu hizi na nyinginezo zinaweza zikatumiwa kwa umakini na kumwezesha mwanafunzi kutumia muda wake wa ziada vizuri na kupata mazoezi ya kutosha zaidi ya yale atakayofanya darasani.

(d) **Kuweka vipaumbele:** Katika utekelezaji wa mipango yoyote ni muhimu



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 95 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuwa na vipaumbele vya kutekeleza kwanza. Mwanafunzi ili aweze kufikia malengo yake aliyojiwekea ni lazima kuelekeza nguvu zake kwenye jambo moja ili alikamilishe kwa wakati. Kwa mfano, mwanafunzi anapaswa kuzingatia masomo yake muda wote anapokuwa darasani na kukamilisha kwa wakati kazi za darasani anazopewa na mwalimu. Mwanafunzi akitekeleza mambo mengi kwa wakati mmoja atashindwa kuweka kipaumbele katika jambo moja na hivyo kushindwa kufanikisha malengo aliyojiwekea.

(e) **Kufanya tathmini:** Tathmini inatakiwa ifanyike katika kipindi chote cha utekelezaji wa mipango. Katika kutekeleza mipango ni muhimu kufanya tathmini kwa kila hatua. Hatua za utekelezaji wa mipango ni muhimu zikazingatia malengo na ufanikishaji wake kwa kila hatua. Pia, ufuatiliaji wa mara kwa mara ni muhimu katika kutathmini utekelezaji. Hii itasaidia kujua mafanikio na udhaifu katika utekelezaji na hivyo kuwezesha kutambua mapema sababu za kutofanikisha kazi zilizopangwa. Kufuatilia na kufanya tathmini mara kwa mara kitasadia kujirekebisha kwa kubuni njia mbadala ili kufikia malengo yaliyowekwa.

### Umuhimu wa kujiwekea malengo katika maisha

Malengo husaidia kuleta mabadiliko katika maisha ya watu. Umuhimu wa kujiwekea malengo katika maisha unaonekana wazi katika faida zake. Kwanza, kujiwekea malengo kunakupa hamasa ya kuandaa mikakati ya kufanikisha au kuwezesha kulifikia lengo. Kwa kuwa malengo huambatana na mkakati au mpango wa utekelezaji, mbinu mbalimbali hubuniwa ili kufikia lengo lililokusudiwa.

Pili, kujiwekea malengo husaidia kufanya uamuzi sahihi kwani hatua mbalimbali huzingatiwa. Kwa mfano, kuna muda maalumu wa kutafakari, kupanga, kuandaa gharama za utekelezaji na kuainisha faida au hasara zinazoweza kutokea kutokana na malengo yaliyowekwa. Kuna uamuzi unaokupeleka kwenye lengo na kuna uamuzi unaokutoa kwenye lengo. Mtu makini huchagua uamuzi utakaompeleka kwenye lengo lake.

Tatu, malengo husaidia kutumia muda ipasavyo kwa kuwa ukishaweka malengo ni lazima kupanga ratiba na muda wa utekelezaji. Hata kama lengo ni la muda mfupi au mrefu, muda lazima utumike vizuri kulingana na mpango wa utekelezaji. Mwanafunzi anapopanga ratiba ya kujisomea humwezesha kutumia muda wake vyema na kufanikisha malengo yake.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Nne, kujiwekea malengo huongeza uwezo wa kujitathmini katika utendaji na utekelezaji wa mipango. Kuwa na malengo hutoa fursa ya kujiuliza maswali juu ya uwezo, na muda ambao unatarajia kufikia lengo lililokusudiwa na hivyo kuchochea tabia ya uwajibikaji kwa mhusika. Mwanafunzi anaweza kujitathmini kwenye masomo yake kutokana na malengo aliyojiwekea.


Mwisho, kujiwekea malengo hukuza ubunifu kwa kuwa ili kufanikiwa huna budi kubuni na kutumia mbinu mbalimbali. Hatua ya kubuni mbinu mbalimbali za kutekeleza malengo husaidia mtu kuwa mbunifu katika kufikia malengo aliyojiwekea.

**Zoezi la 1**

1. Bainisha tofauti kati ya malengo ya muda mfupi na malengo ya muda mrefu.
2. Eleza uhusiano uliopo kati ya kujiwekea malengo katika maisha na kufanya uamuzi sahihi.
3. Jadili ni kwa jinsi gani kujiwekea malengo katika maisha kunachochea maendeleo ya haraka.
4. Ili malengo yaweze kufikiwa kwa wakati ni vyema kuchagua njia bora za kutekeleza mpango. Orodhesha njia hizo.
5. Ainisha njia bora utakazozitumia ili kufikia malengo uliyojiwekea katika kufaulu mtihani wa kumaliza elimu ya msingi.

FOR ONLINE USE ONLY

**Kazi ya kufanya namba 1**



Jadiliana na wanafunzi wenzako kwenye kikundi na bainisha malengo mliyojiwekea kabla ya kumaliza elimu ya msingi. Kisha orodhesha shughuli mlizopanga kuzitekeleza ili kufikia malengo na ziandike kwenye daftari lako la mazoezi.

### Faida za kufuata hatua za utekelezaji wa mpango

Ukifuata hatua hizi katika utekelezaji wa mpango wako utapata faida zifuatazo:

(a) **Kutambua rasilimali:** Katika mchakato wa kutekeleza mpango, rasilimali



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 97 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mbalimbali hubainishwa na kufanyiwa tathmini ili kuona kama zinakidhi mahitaji ya lengo ulilojiwekea. Rasilimali hizo ni pamoja na fedha, vifaa, watu au utaalamu.

(b) **Kuongeza ufanisi:** Kufuata hatua za utekelezaji wa mpango huongeza ufanisi katika utekelezaji kwa kuwa utambuzi wa njia huzingatia mahitaji muhimu kama gharama, nguvukazi na muda. Pia, ni kwa sababu kunakuwa na uwiano kati ya rasilimali zinazohitajika na malengo yaliyokusudiwa.

(c) **Kutumia muda vizuri:** Kufuata hatua za utekelezaji wa mpango husaidia kuleta nidhamu katika utekelezaji. Nidhamu ya kutunza muda husaidia kutekeleza kwa wakati shughuli zilizopangwa na hivyo kufikia malengo.

(d) **Kujiamini:** Kujiamini kunaweza kujengeka ikiwa utajiwekea malengo na kufuata hatua za utekelezaji. Hali ya kujiamini itajengeka kwa kuwa utakuwa na uhakika na kitu unachokifanya. Aidha, hali ya kujiamini huongeza uvumilivu na iwapo kutatokea shida yoyote, utakuwa na subira kwa kujua au kuamini kuwa lengo litafikiwa.

(e) **Msukumo chanya:** Hatua za kutekeleza mipango huongeza ari na kujenga imani kuwa mafanikio yataonekana katika kila hatua ya utekelezaji. Hali hii itatokea kwa sababu shughuli mbalimbali zitakazokuwa zimepangwa zitatekelezwa kwa muda tofauti na hivyo kuleta msukumo chanya wa kutekeleza shughuli zilizobakia. Mafanikio ya hatua moja huleta msukumo wa kuendelea na hatua ya pili.

**Zoezi la 2**

1. Orodhesha umuhimu wa kujiwekea malengo katika maisha.
2. Njia za utekelezaji wa mipango zinakusaidiaje katika kufikia malengo?
3. Taja faida za kutumia muda vizuri katika utekelezaji wa mpango.
4. Eleza kwa kifupi jinsi utekelezaji wa mipango unavyoleta ufanisi.
5. Jadili mbinu za kuongeza ufanisi ili kufikia malengo bila kuathiri ubora.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 98 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 2**

Andika njia utakazotumia ili kufaulu vizuri mtihani wako wa Darasa la Saba. Kisha, eleza kwa kifupi namna utakavyotumia njia hizo.

## Kutatua changamoto wakati wa kutekeleza mipango

Utekelezaji wa mipango ili kufikia malengo haukosi kuwa na changamoto. Utatuzi wa changamoto wakati wa utekelezaji wa mipango ni jambo muhimu sana. Ili kutatua changamoto inabidi kufanya yafuatayo:

(a) **Kubaini kiini na ukubwa wa changamoto:** Katika hatua hii ya kwanza ni muhimu kudadavua sababu za msingi za kuwapo kwa changamoto hizo. Hapa utajiuliza maswali kama, Je, hali ya uchumi ikoje? Je, rasilimali zilizopo zinatosheleza kutatua changamoto hizi? Maswali haya na mengine yatakuwezesha kupata kiini au chanzo cha changamoto zinazojitokeza.

(b) **Kubaini njia sahihi za kutatua changamoto:** Ni muhimu kutafuta njia mbalimbali za kutatua changamoto. Kwa mfano, kama changamoto ni upungufu wa fedha, itakulazimu kuangalia vyanzo vingine vya kupata fedha kama vile mikopo au msaada toka kwa ndugu na marafiki. Ikiwa changamoto ni ukosefu wa soko basi buni njia za kutangaza biashara yako.

(c) **Kupima ufanisi wa njia za utekelezaji:** Ni muhimu kupima ufanisi wa njia za utekelezaji kadiri unavyoendelea kutekeleza mipango yako. Bainisha ufanisi na changamoto unazopitia wakati wa kutumia njia fulani ili kuweza kuziboresha kulingana na uwezo uliopo.

(d) **Kutumia kwa makini njia ulizochagua:** Baada ya upimaji kufanyika, tumia njia uliyochagua kwa kuzingatia mikakati uliyojiwekea. Umakini katika kutumia njia uliyochagua ni muhimu ili kuepuka makosa ambayo yatazuia au kudhoofisha ufanisi wa utekelezaji wa mipango.

(e) **Kufanya tathmini:** Ni muhimu kufanya tathmini ili kubainisha matokeo ya utekelezaji wa mipango. Hatua hii itakuwezesha kutambua iwapo umefanikiwa au haujafanikiwa kwa kiwango gani. Matokeo ya tathmini yatakuwezesha kuandaa mikakati mipya itakayokuwezesha kutekeleza mambo ambayo hayakufanikiwa kama ilivyokusudiwa.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 99 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

1. Eleza kwa kifupi sababu za kubuni njia sahihi za kutatua changamoto.
2. Jadili umuhimu wa kufuata hatua za utatuzi wa changamoto.
3. Eleza kwa ufupi jinsi ya kubaini kiini cha changamoto.

### Njia za kuelimisha jamii umuhimu wa kujiwekea malengo katika maisha

Si kila mtu ana elimu ya umuhimu wa kujiwekea malengo katika maisha. Ni muhimu kufahamu njia za kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kujiwekea malengo. Baadhi ya njia hizo ni kama zifuatazo:

(a) **Igizodhima:** Njia hii ni bora katika kuelimisha jamii ili kujiwekea malengo kwa kuwa inawavutia na kuwaburudisha watazamaji wa igizo.

(b) **Midahalo:** Njia hii ni muhimu katika kutoa elimu kwa kuwa hushirikisha mawazo ya watu wengi juu ya umuhimu wa kujiwekea malengo.

(c) **Hotuba:** Njia hii huweza kutumika hasa kwenye mikutano ya hadhara ambapo viongozi au watu maalumu wanaweza kuhutubia umma juu ya umuhimu wa kujiwekea malengo.

(d) **Ngonjera:** Kwa kutumia ngonjera zenye maudhui ya kuelimisha jamii kujiwekea malengo, mwanafunzi anaweza kujifunza namna atakavyojiwekea malengo katika maisha yake.

(e) **Mashairi:** Kwa kutumia mashairi yenye maudhui ya kujiwekea malengo, hadhira inaweza kupata elimu kuhusu kujiwekea malengo kwenye maisha.

(f) **Majadiliano:** Majadiliano kati ya wanafunzi huwajengea uelewa na kubaini njia sahihi katika kuweka malengo na kutekeleza mipango yao.

## Zoezi la 4

1. Eleza kwa kifupi njia tano za kuelimisha jamii juu ya kujiwekea malengo.
2. Fafanua njia ya hotuba inavyoweza kuelimisha jamii juu ya kujiwekea malengo katika maisha.
3. Njia ipi ni bora zaidi kuelimisha vijana kujiwekea malengo katika maisha? Toa sababu kwanini njia hiyo ni bora zaidi.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 100 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 3**

Tunga igizodhima kuhusu umuhimu wa wanafunzi kujiwekea malengo katika maisha. Kisha wasilisha kazi yako darasani.

## Zoezi la 5

**A:** Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi.

1. Malengo ya muda mrefu ni malengo yanayokusudiwa kufikiwa kwa muda mrefu.__________
2. Utekelezaji wa mipango ya maisha kwa muda mwafaka kulingana na rasilimali zilizopo husaidia kuleta ufisadi katika jamii.__________
3. Kazimradi ni njia mojawapo ya uelimishwaji wa jamii kujiwekea malengo katika maisha.__________
4. Malengo ya muda mfupi ni sehemu ya malengo ya muda mrefu. __________

**B:** Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake kwenye kisanduku.

5. Lipi kati ya mambo yafuatayo si muhimu katika kujiwekea malengo katika maisha?
   (a) ujuzi wa kutathmini
   (b) kuandaa rasilimali
   (c) kujua Kiingereza
   (d) ari ya kufikia lengo

   [ ]

6. Utekelezaji wa mipango katika maisha kwa muda mwafaka kulingana na rasilimali zilizopo una faida gani?
   (a) kuongeza msukumo chanya wa kutekeleza mipango
   (b) kupiga vita utekelezaji wa mipango
   (c) kuongeza msukumo hasi wa kutekeleza mipango
   (d) kushindwa kutekeleza mipango

   [ ]



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 101 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

7. Ipi ni hatua mojawapo muhimu katika kutatua changamoto wakati wa kutekeleza mipango?
   (a) kubaini kiini na ukubwa wa changamoto
   (b) kuwekeza zaidi katika utekelezaji wa mipango
   (c) kupata ushauri wa namna ya kutekeleza mipango
   (d) kuvumilia changamoto katika utekelezaji wa mipango

8. Ipi kati ya zifuatazo si njia za kuelimisha jamii juu ya kutekeleza mipango?
   (a) igizodhima
   (b) hotuba na midahalo
   (c) mashairi na ngonjera
   (d) historia na hotuba

9. Njia ipi kati ya zifuatazo ni njia sahihi ya utekelezaji wa mipango?
   (a) kujitenga na watu
   (b) kujitenga na watu wasiokujua
   (c) kushirikiana na watu wengine
   (d) kujitenga na watu wasiokupenda

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 102 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C:** Oanisha kipengele kutoka **Sehemu A** na maneno yaliyopo **Sehemu B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.

| Sehemu A | Jibu | Sehemu B |
|---|---|---|
| 10. Malengo ya muda mrefu | | (a) njia za kuelimisha juu ya kupata utajiri |
| 11. Igizodhima | | (b) njia za kuelimisha jamii juu ya kujiwekea malengo |
| 12. Kukuza ubunifu | | (c) namna ya kutatua changamoto |
| 13. Tathmini ya utekelezwaji wa mipango | | (d) jambo la kwanza la kubaini katika kutatua changamoto |
| 14. Kiini cha changamoto | | (e) hatua ya mwisho katika kutatua changamoto |
| | | (f) umuhimu wa kujiwekea malengo katika maisha |
| | | (g) mambo yanayotakiwa kutekelezwa ndani ya muda mfupi |
| | | (h) mambo yanayotakiwa kutekelezwa kwa muda mrefu |
| | | (i) utekelezaji wa mipango katika maisha |

**Msamiati**

Dhahiri — bayana, waziwazi bila kificho

Kudadavua — kuchambua na kuweka dhahiri jambo; kueleza jambo kwa undani, kufafanua kwa kina

FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na moja

## Kuchanganua mambo kiyakinifu

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza jinsi ya kufanya udadisi katika mazingira yako na kutathmini uwezo wako katika kujifunza. Pia, ulijifunza umuhimu wa kushirikiana na watu wengine katika kujifunza. Katika sura hii, utajifunza namna ya kuchanganua mambo kiyakinifu. Vilevile, utajifunza stadi za kutumia wakati wa kujifunza kiyakinifu na kuwa mwajibikaji katika kujifunza. Maarifa na ujuzi huu ni muhimu kwako kwa sababu utakuwezesha kufanya uamuzi ulio sahihi katika mchakato wa ujifunzaji. Aidha, utakuwezesha kuwa mbunifu na mdadisi katika kukabiliana na changamoto katika kujifunza.*



**Fikiri**

Kuna umuhimu gani wa kujifunza kiyakinifu?

### Kujifunza kiyakinifu na kiuwajibikaji

Kujifunza kiyakinifu ni mfumo wa ujifunzaji unaolenga kumjengea mwanafunzi uwezo wa kuhusianisha anachojifunza na hali halisi ya mazingira ya maisha yake ya kila siku. Namna hii ya kujifunza ni tofauti na kujifunza kwa kukariri. Mwanafunzi akijifunza kwa kukariri hupata uwezo wa kukumbuka lakini hukosa uwezo wa kutumia anachokumbuka kutatua matatizo anayokabiliana nayo katika mazingira anayoishi.

Kujifunza kiuwajibikaji ni njia inayomjengea mwanafunzi uwezo wa kujifunza na kujitambua yeye mwenyewe pamoja na wajibu wake katika mchakato mzima wa kujifunza. Mwanafunzi anajijengea utamaduni wa kubaini vitu vya kujifunza na jinsi yeye mwenyewe atakavyowajibika katika ujifunzaji huo bila kusukumwa na mtu mwingine, bali kwa kuzingatia maelekezo anayopewa.

### Umuhimu wa kujifunza kiyakinifu na kiuwajibikaji

Mwanafunzi anayejifunza kiyakinifu huwa na taarifa na vielelezo vya kutosha, hivyo kutotegemea hisia zake tu katika kuelezea jambo fulani. Pia, kujifunza

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kiyakinifu humsaidia mwanafunzi kuwa mbunifu na mdadisi katika shughuli zake za kila siku. Ubunifu humwezesha mwanafunzi kukabiliana na changamoto mbalimbali katika mchakato mzima wa ujifunzaji kwa kushirikiana na wenzake. Hivyo, kujifunza kiyakinifu humsaidia mwanafunzi kuwa mwajibikaji katika kujituma na kujitolea kikamilifu katika shughuli zake za kila siku pasipo kutegemea tu hisia zake.

Mwanafunzi anapojifunza mambo kiyakinifu, hudadisi mambo mbalimbali katika kujifunza kwake. Kutokana na kuwa na uwezo wa kudadisi na kuchanganua mambo kwa ustadi, mwanafunzi huwa na mifano na uzoefu wa kutosha. Uzoefu huo humjengea stadi za kujiamini zaidi. Mwanafunzi anapofanya mambo kwa kujiamini na kwa ustadi mkubwa huongeza wigo wa kufanya jambo kwa usahihi na kulichanganua kwa kina.

Kujifunza kiyakinifu na kiudadisi humjengea mwanafunzi uwezo wa kutafakari na kuwasilisha hoja kwa ufasaha. Mwanafunzi anapojifunza kiyakinifu huwa na uwezo mkubwa wa kuchambua mambo ambayo ameshayatafakari. Kwa mfano, mwanafunzi anapaswa kuwa na uelewa wa hoja anayowasilisha. Pia, anawajibika kufahamu misingi ya hoja yenyewe na awe na uwezo wa kufafanua hoja akiwa na vielelezo, ili upande atakaoelekea uwe na ushahidi. Kutafakari na kuwasilisha hoja kwa ufasaha humjengea mwanafunzi uwezo wa kubaini na kukabiliana na changamoto wakati wa kujifunza.

**Zoezi la 1**

1. Tofautisha kati ya kujifunza kiyakinifu na kujifunza kwa kukariri.
2. Eleza umuhimu wa kujifunza kiyakinifu.
3. Eleza kwa kifupi jinsi ujifunzaji kiyakinifu unavyoweza kukusaidia kutatua changamoto katika kujifunza.

**Kazi ya kufanya namba 1**

Chandya ni mwanafunzi wa Darasa la Saba. Katika mitihani ya muhula wa kwanza alipata alama chini ya wastani. Buni mbinu atakazotumia Chandya ili kufanya vizuri katika Mtihani wa Taifa.

## Stadi za kutumia wakati wa kujifunza kiyakinifu na kiuwajibikaji

Kufanya uchunguzi ni sifa muhimu katika kujifunza kiyakinifu. Usomaji wa kiyakinifu unapaswa kuendana na kufanya utafiti ili kupata majibu ama



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 105 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

vielelezo muhimu katika kujenga hoja. Kwa mfano, wanafunzi katika somo la Uraia na Maadili, wapewe fursa ya kutembelea mihimili ya dola ambayo ni Serikali, Bunge, Mahakama na taasisi zake ili kujionea jinsi zinavyofanya kazi. Fursa hizi zitawawezesha kuhusisha nadharia wanayopata darasani na hali halisi.

Katika kufanya uchambuzi wa hoja au jambo fulani, hatua na vielelezo mbalimbali kuhusiana na jambo hilo ni muhimu ili kupata majibu halisia. Ni muhimu kufahamu dhana halisi ya jambo linalojadiliwa, na kuwa na vyanzo sahihi vya taarifa.

Ili usomaji yakinifu uwe na maana, ni muhimu kufahamu maana na tafsiri sahihi ya kila jambo wakati unatafuta maana halisi. Tofauti na usomaji wa nadharia ambao mwanafunzi hukariri bila kuelewa maana ya mambo yaliyojadiliwa, usomaji yakinifu hujengwa katika muktadha wa kuelewa kuliko kukariri. Mwanafunzi anapoelewa jambo hujenga uwezo na ujuzi na kumfanya kuwa mdadisi na hatimaye kuwa mgunduzi.

Kusoma kiyakinifu ni usomaji unaohitaji kumjengea msomaji tafakari ya mambo anayopaswa kuyasoma. Tafakari kama nguzo muhimu ya usomaji yakinifu, huweza kuongeza uwezo wa kitaaluma, ubunifu, na uwajibikaji wa mwanafunzi. Tafakari husaidia mwanafunzi kupangilia mambo na kuyatekeleza ipasavyo. Hivyo, kusoma kwa kutafakari humwezesha mwanafunzi kupanga mikakati madhubuti itakayomsaidia kuongeza mafanikio na kurekebisha upungufu unaojitokeza.

**Zoezi la 2**

1. Ainisha stadi tatu utakazoweza kuzitumia unapojifunza kiyakinifu.
2. Eleza kwa kifupi namna stadi za kujifunza kiyakinifu zitakavyokusaidia katika kujifunza.
3. Bainisha hatua utakazozitumia katika kufanya uamuzi sahihi.

**Kazi za kufanya namba 2**

Tembelea ofisi ya kata na chunguza hatua zinazofuatwa na Baraza la Kata katika kutatua migogoro. Andika hatua hizo kwenye daftari lako kisha uwasilishe darasani kwa majadiliano.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 106 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Mbinu za kuhamasisha tabia ya kujifunza kiyakinifu

Zipo mbinu mbalimbali ambazo mwanafunzi anaweza kuzitumia ili aweze kuhamasika na kujijengea tabia ya kujifunza kiyakinifu. Baadhi ya mbinu hizo ni kushiriki katika igizodhima, kutumia visamafunzo, kujadiliana katika vikundi na kufanya kazi za uongozi na za uzalishaji mali.

Kushiriki katika maigizo huondoa tabia ya aibu na kumjengea mwanafunzi ujasiri wa kuwasilisha hoja mbele ya watu. Igizodhima humfanya mwanafunzi kuweka mambo katika hali ya uhalisia. Kwa kutenda vitendo katika igizodhima, mwanafunzi hutumia umahiri wake kutoa ujuzi alionao kinadharia na kuuweka katika hoja thabiti pamoja na vitendo. Pia, kwa kufanya igizodhima mwanafunzi anaweza kuiga ujasiri na mbinu mbalimbali za kuweka nadharia katika vitendo.

Njia nyingine ya kuhamasisha kujifunza kiyakinifu kwa mwanafunzi ni kutumia visamafunzo. Visamafunzo hutumia wahusika kama watu, ndege, wanyama na vitu ili kuelezea tabia fulani za watu katika jamii. Vilevile, hutoa mafunzo juu ya kipi ni kitu chema cha kuigwa na kipi ni kibaya cha kuepukwa. Visamafunzo vina faida sawa na kuangalia igizodhima.

Pia, mijadala ya vikundi inaweza kutumika. Hii humsaidia mwanafunzi kujenga hoja kiyakinifu. Katika mijadala mwanafunzi hujitathmini na kuona hoja zilizo bora na zile zilizo dhaifu. Jinsi mwanafunzi anavyozidi kufanikiwa katika kujenga hoja bora na za kukubalika na wenzake, ndivyo anavyohamasika kuwa myakinifu zaidi.

Mwisho, kufanya kazi za uongozi kama vile kuwa kiranja shuleni humsaidia mwanafunzi kujenga tabia ya uyakinifu. Kiongozi huwa na uwezo na fursa ya kuweka sera na sheria katika vitendo. Vilevile, kufanya kazi za uzalishaji husaidia kujenga tabia ya uyakinifu. Kwa mfano, baada ya kujifunza darasani juu ya namna ya kuandaa kitalu cha miche ya miti, mwanafunzi anaweza kushiriki katika kazi ya kuandaa kitalu hicho kivitendo. Mbinu hizi zote husaidia kumjengea mwanafunzi tabia ya kujifunza kiyakinifu.

**Zoezi la 3**

1. Taja mbinu mbalimbali zinazohamasisha tabia ya kujifunza kiyakinifu.
2. Eleza ni kwa namna gani kufanya kazi ya uongozi hufanya mwanafunzi ajenge tabia ya kiyakinifu.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 107 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Eleza namna utakavyomsaidia mwenzako asiyependa kushiriki kwenye mijadala ya vikundi.

**Kazi za kufanya namba 3**

Chunguza mambo yanayosababisha baadhi ya wanafunzi kupenda na wengine kutopenda kujifunza katika vikundi. Kisha, eleza faida za kujifunza katika vikundi na hasara kwa wale wasiopenda kujifunza katika vikundi.

## Zoezi la 4

**A:** Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi.

1. Kujifunza kiyakinifu ni bora zaidi kuliko kujifunza kwa kukariri.__________
2. Kujifunza kiuwajibikaji ni mfumo usiomwandaa mwanafunzi kujitambua.__________
3. Moja ya faida ya kujifunza kiyakinifu ni kukuza ubunifu.__________
4. Kutafiti jambo kabla ya kulifanyia uamuzi ni kupoteza muda.__________
5. Moja ya stadi za kujenga wakati wa kujifunza kiyakinifu ni kutafakari jambo.__________

**B:** Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake kwenye kisanduku.

6. Ipi kati ya zifuatazo si hatua za kufanya uamuzi sahihi?
   (a) kufahamu tatizo
   (b) kutengeneza mikakati
   (c) kutathmini
   (d) kutokukubaliana na changamoto
7. Mijadala kwa vikundi ni njia ya majadiliano yenye faida gani kwa mwanafunzi?
   (a) humwezesha kuuliza maswali
   (b) humfanya kuwa huru kujadili
   (c) humsaidia kupoteza muda
   (d) hujifunza namna ya kujenga hoja bora
8. Kufanya kazi kwa vitendo humsaidia mwanafunzi kutumia milango

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

gani ya fahamu?
(a) pua na mdomo
(b) milango yote ya fahamu
(c) macho na ngozi
(d) ulimi na pua

9. Mwanafunzi hutegemea nini anapowajibika na kujituma katika shughuli zake?
(a) hisia zake
(b) hisia za watu wengine
(c) hisia za wazazi
(d) hisia za walimu

10. Ipi kati ya mbinu zifuatazo hazihamasishi kujenga tabia ya kujifunza kiyakinifu miongoni mwa wanafunzi na jamii?
(a) kufanya kazi kwa vitendo
(b) mijadala kwa vikundi
(c) kisamafunzo
(d) kisa mkasa

**C:** Oanisha kipengele kutoka **Sehemu A** na maneno yaliyopo **Sehemu B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.

| Sehemu A | Jibu | Sehemu B |
|---|---|---|
| 11. Igizodhima | | (a) hatua na vielelezo |
| 12. Kuchambua jambo | | (b) mbinu za kuhamasisha kujenga tabia ya kujifunza kiyakinifu na kiuwajibikaji |
| 13. Usomaji kiyakinifu | | (c) kujifunza kwa vitendo |
| 14. Uwezo wa kutafakari | | (d) humjengea uelewa wa haraka |
| 15. Kujifunza kwa kukariri | | (e) utafiti, kubuni na kudadisi |
| 16. Kisamafunzo | | (f) kujifunza kwa nadharia |
| | | (g) kuwasilisha hoja kwa ufasaha |

**Msamiati**

Kiyakinifu — namna ya jambo kuwa la ukweli kwa uthibitisho wa utafiti makini

Mchakato — mfuatano wa mambo ambayo yamepangiliwa kufanyika kwa utaratibu maalumu



FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Mbili

## Kuaminika katika jamii

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza kutathmini utekelezaji wa wajibu wako na kujiepusha na vitendo vinavyosababisha kutokuaminika katika jamii. Katika sura hii, utajifunza vitendo vinavyoonesha uaminifu shuleni na katika jamii, kuheshimu imani na itikadi za watu wengine na njia sahihi za kutimiza majukumu yako. Pia, utajifunza namna ya kushiriki chaguzi mbalimbali shuleni. Maarifa na ujuzi utakaopata katika sura hii, utakuwezesha kufanya vitendo vitakavyokufanya kuaminika shuleni na katika jamii unamoishi.*



**Fikiri**

Vitendo ulivyowahi kuvifanya katika jamii ambavyo vinaonesha uaminifu.

### Vitendo vinavyoonesha uaminifu shuleni na katika jamii

Uaminifu ni nguzo muhimu inayokuwezesha kuishi na kukubalika kwa wenzako katika mazingira ya shule na jamii kwa ujumla. Mwanafunzi anapokuwa mwaminifu katika jamii humwezesha kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi. Vifuatavyo ni baadhi ya vitendo vinavyofanya mwanafunzi aweze kuaminika shuleni na katika jamii:

(a) **Kutii sheria za shule:** Ili mwanafunzi aaminike katika shule na jamii inayomzunguka, ni muhimu kuheshimu sheria na taratibu za shule. Kutii sheria za shule ni pamoja na kuwahi shuleni, kutunza mali za shule, kuhudhuria masomo kwa kufuata ratiba ya shule na kuheshimu Wimbo na Bendera ya Taifa. Pia, mwanafunzi anapaswa kutokujihusisha na vitendo viovu kama wizi na matumizi ya dawa za kulevya.

(b) **Kuwa na heshima:** Mwanafunzi huaminika katika shule na jamii yake kutokana na kuheshimu wakubwa, kuheshimu viongozi na hata wanafunzi wengine wa rika lake. Hii humwongezea mwanafunzi uwezo wa kujenga uhusiano na maelewano mema katika jamii inayomzunguka.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 110 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pia, kuheshimu watu humfanya mwanafunzi kuaminika na kupendwa na wanafunzi wenzake, walimu na wanajamii. Hali hii humfanya mwanafunzi kushirikishwa kwenye shughuli za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kwa mwanafunzi wa Kitanzania, heshima kwa viongozi huanzia kwa wale wa ngazi ya darasa hadi wale wa Taifa.

(c) **Kutunza mali za shule:** Kutunza vizuri mali za shule humjengea mwanafunzi uaminifu kwa wenzake na walimu. Mwanafunzi huaminika kwa wanafunzi wenzake, walimu na jamii yake kwa ujumla. Hii hutokana na umakini wake wa utunzaji wa mali za shule.

(d) **Kuwa mkweli na muwazi:** Mwanafunzi anapokuwa mkweli na muwazi kwa masuala yake binafsi na yale yanayohusu shule na jamii kwa ujumla, huaminiwa na wanafunzi wenzake, walimu na wanajamii. Tabia ya ukweli na uwazi humsaidia mwanafunzi kushirikishwa na wanafunzi au wanajamii wenzake katika shughuli mbalimbali. Kwa mfano, mwanafunzi anapoomba ruhusa ya kutohudhuria masomo kwa sababu ya ugonjwa, ni lazima awe mgonjwa kweli ili kila aliye na uhusiano naye aamini taarifa hiyo.

(e) **Kufanya kazi kwa bidii:** Mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kwenye shughuli za kijamii huaminika zaidi. Mwanafunzi mwenye bidii anawajibika katika kila jukumu linalokuwa mbele yake, hivyo, kupendwa na wanafunzi, walimu na wanajamii. Kwa mfano, katika ngazi ya shule, mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na shughuli nyingine za shule anaweza kupendekezwa kuongoza wenzake.

(f) **Kuwa na uhusiano mzuri na wenzake:** Mwanafunzi huaminika na wanafunzi, walimu na wanajamii wenzake kutokana na kuweza kujenga uhusiano mzuri miongoni mwao. Kwa mfano, mwanafunzi hujenga uhusiano mzuri kwa kujiheshimu, kuwaheshimu, kuwapenda na kuwasaidia wenzake wanapokuwa na uhitaji.

FOR ONLINE USE ONLY

**Zoezi la 1**

1. Ni vitendo gani unavyovifanya shuleni na nyumbani ambavyo vinakujengea uaminifu kwa wenzako?
2. Eleza kwa kifupi jinsi ukweli na uwazi ulivyokujengea uaminifu katika jamii yako.
3. Ni kwa namna gani kufanya kazi kwa bidii humwezesha mwanafunzi kuaminika na jamii au shule yake?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Kwa nini kutunza mali za shule humfanya mwanafunzi kuaminika kwa wanafunzi, walimu na hata jamii kwa ujumla?

**Kazi ya kufanya namba 1**

Eleza matendo unayoyatenda shuleni ambayo yanakuwezesha kuaminika kwa wanafunzi wenzako na walimu wanaokufundisha.

### Kuheshimu imani na itikadi za watu wengine

Jamii yenye amani na mshikamano huheshimu imani na itikadi za watu wengine. Kuheshimu imani na itikadi za watu wengine hujenga upendo, amani na ushirikiano miongoni mwa wanajamii. Tabia ya kuheshimu imani na itikadi za watu wengine huwafanya wanajamii kushirikiana bila kubaguana. Ushirikiano huo huweza kuwa katika masuala mbalimbali ya kijamii, kwa mfano misiba na sherehe. Yafuatayo ni baadhi ya matendo yanayoonesha kuheshimu imani na itikadi za watu wengine katika jamii:

(a) **Kutokashifu au kubeza imani na itikadi za watu wengine:** Ili kuhakikisha watu wanaheshimu itikadi na imani za watu wengine, ni muhimu kutokubeza wala kukashifu itikadi au imani ya mtu mwingine. Imani na itikadi hubeba dhana ya maisha ya mtu kiroho na kimwili. Ni muhimu kwa kila mtu kutenda matendo anayoyaamini kuwa ni sehemu ya imani na itikadi hizo alimradi havunji sheria au kukashifu imani za watu wengine. Kuheshimu imani na itikadi za watu wengine husaidia kuleta uhusiano mzuri baina ya wanajamii. Muumini wa imani fulani hujisikia amani anapojua mwenzake anatambua na kuheshimu imani yake.

(b) **Kujenga ushirikiano na watu wa imani na itikadi nyingine:** Ili kuheshimu imani na itikadi za watu wengine, ni muhimu kujenga ushirikiano na watu hao katika masuala mbalimbali ya kijamii. Ushirikiano na watu wa itikadi tofauti hujenga upendo na mshikamano miongoni mwao bila kuwa na mipaka ya kiimani na kiitikadi.

(c) **Makongamano na mikutano ya pamoja:** Mikutano na makongamano yanayohusisha imani au itikadi tofauti huhamasisha watu wenye itikadi na imani tofauti kufahamu kinachokubalika na kisichokubalika katika jamii. Hii husaidia watu kuheshimu itikadi na imani za watu wengine wakifahamu mipaka ya kiimani na kuepuka migogoro.



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 112 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 2**

1. Eleza kwa kifupi faida za kuheshimu itikadi na imani za wanafunzi wenzako.
2. Taja mambo matatu yanayoweza kufanyika ili watu waheshimu itikadi na imani za watu wengine.
3. Ni mambo gani ambayo watu wanapaswa kushirikiana bila kujali itikadi na imani zao?
4. Je, unawashauri nini wanafunzi wenzako wanaobeza na kukashifu imani na itikadi za watu wengine?

**Kazi ya kufanya namba 2**

Katika kikundi cha wanafunzi watano, jadili faida tano za kuvumiliana katika imani za dini tofauti. Kisha, wasilisha darasani kwa majadiliano ya pamoja.

## Njia sahihi za kutimiza majukumu

Ili kutimiza majukumu katika shule yako kwa usahihi, ni muhimu kufanya mambo yanayotakiwa kutimizwa kwa ufanisi kulingana na taratibu za shule. Mwanafunzi anatakiwa kufanya mambo mbalimbali ili kuweza kutimiza majukumu yake katika kujifunza. Zifuatazo ni baadhi ya njia sahihi kwa mwanafunzi kutimiza majukumu yake vizuri awapo shuleni:

(a) **Kuhudhuria masomo darasani:** Mwanafunzi anatakiwa kutimiza jukumu la kuhudhuria shuleni na kushiriki kikamilifu katika kujifunza masomo yote darasani. Mwanafunzi anapotimiza jukumu hili, hupata fursa ya kushiriki katika shughuli mbalimbali kama vile uzalishaji mali, michezo, kutunza mazingira na kujifunza kikamilifu.

(b) **Kufuata ratiba ya kila siku ya masomo:** Mwanafunzi anatakiwa kufuata ratiba ya masomo ya kila siku. Anatakiwa kuhakikisha anashiriki kujifunza kwa kuandaa vifaa vinavyotakiwa. Vifaa hivyo ni madaftari na vitabu vya masomo anayosoma, kalamu ya wino, kalamu ya risasi, rula na mkebe wa vifaa vya jometri kama ratiba inavyoelekeza. Hii humsaidia mwanafunzi kujifunza masomo yote kikamilifu na hivyo kuongeza ufanisi katika masomo yake.

(c) **Kusikiliza walimu kwa umakini:** Mwanafunzi anapokuwa darasani lazima awe msikivu kwa walimu wanaomfundisha masomo yote.

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 113 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mwanafunzi anatakiwa kuwa makini ili kuweza kusikiliza na kumwelewa mwalimu kwa yale aliyokusudia kuyafundisha. Mwanafunzi anapaswa kutokubagua masomo na badala yake anatakiwa kuonesha bidii katika masomo yote.

(d) **Kutunza mazingira ya shule:** Ili mwanafunzi aweze kutimiza majukumu yake awapo shuleni, ni lazima atunze mazingira ili kumwezesha kupata utulivu wakati wa kujifunza. Mwanafunzi anatakiwa kutunza mazingira yake kwa kufagia viunga vya shule, kufyeka majani, kuokota takataka na kupanda miti. Mazingira safi na yenye hewa safi ni muhimu kwa mwanafunzi ili aweze kujifunza vizuri.

(e) **Kuwahi shuleni:** Mwanafunzi anapowahi shule huepuka kuchelewa masomo. Pia, huweza kujiandaa kikamilifu kwa ajili ya masomo kwa kuandaa nyenzo za kujifunzia kama vile vitabu, madaftari, kalamu na rula.

(f) **Kushirikiana na wenzake:** Mwanafunzi anatakiwa kushirikiana na wenzake kwenye mambo mbalimbali kama vile kujifunza, kutunza mazingira, michezo na uzalishaji mali. Majukumu yote haya huweza kufanyika kwa ufanisi zaidi endapo mwanafunzi atashirikiana vyema na wenzake. Kwa mfano, kufagia maeneo ya shule huhitaji wanafunzi kushirikiana pamoja ili kuokoa muda na kuendelea na shughuli za masomo.

(g) **Kujituma:** Ili mwanafunzi aweze kutimiza majukumu yake ya kupata maarifa shuleni kwa ukamilifu, ni lazima ajitume kwenye shughuli za masomo, uzalishaji mali na kushiriki kutunza mazingira ya shule. Akifanya haya, atakuwa ametimiza wajibu wake vyema. Hali hii humjengea tabia ya kushiriki kwa ufanisi katika shughuli za kijamii na kiuchumi, hivyo kuwa nguzo muhimu kwa jamii yake na Taifa kwa ujumla.

(h) **Kujitambua:** Mwanafunzi anapaswa kujua nafasi yake binafsi, kwa familia, jamii na Taifa kwa ujumla. Mwanafunzi anapojitambua vyema humsaidia kutekeleza malengo aliyojiwekea. Ili mwanafunzi aweze kufikia malengo hayo, ni lazima ajitambue kwa kusoma kwa bidii na kuepuka tabia hatarishi na hatimaye kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali shuleni na nyumbani.

**Zoezi la 3**

1. Eleza kwa kifupi faida za mwanafunzi kuwahi shuleni.



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 114 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Je, tabia ya kujituma imekusaidiaje katika maisha yako ya kila siku?
3. Fafanua umuhimu wa kushirikiana na wenzako katika masomo na shughuli nyingine za shule.

**Kazi ya kufanya namba 3**

Bainisha mambo unayotenda kila siku shuleni na jinsi yanavyokusaidia katika kutimiza majukumu ya kitaaluma, usafi wa mazingira na elimu ya kujitegemea. Yaandike kwenye daftari lako la mazoezi, kisha yawasilishe darasani.

### Kushiriki kwenye uchaguzi shuleni

Ushiriki wa mwanafunzi katika uongozi wa shule, humpa wasaa mzuri wa kuweza kushiriki katika kutekeleza uamuzi wa mambo mbalimbali. Mambo haya yanaweza kuwa yanayohusu masomo, mazingira, michezo na uzalishaji mali. Kupitia uchaguzi wa viongozi wa uongozi wa wanafunzi, wanafunzi hupata wawakilishi wao katika mambo yanayogusa masilahi yao shuleni. Kushiriki katika uchaguzi wa uongozi wa wanafunzi huleta faida mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) **Kujifunza demokrasia kwa vitendo:** Wanafunzi wanaposhiriki katika chaguzi za uongozi wa wanafunzi, hupata nafasi ya kujifunza demokrasia kwa vitendo. Hali hii hujenga ujuzi na uwezo wa kufanya uamuzi. Kupitia chaguzi za shule, wanafunzi hujifunza jinsi ya kushiriki katika chaguzi za ngazi mbalimbali zinazofanyika katika jamii.

(b) **Kupata haki ya kuchaguliwa na kuchagua:** Chaguzi za uongozi wa wanafunzi huwasaidia wanafunzi kupata haki zao kama vile haki ya kuchagua na kuchaguliwa. Wanafunzi wenye sifa hupata nafasi ya kugombea na hatimaye kuchaguliwa kuwa viongozi. Pia, wanafunzi wengine hupata wasaa kupitia uchaguzi huo, kuchagua kiongozi wanayemtaka kutokana na uwezo alionao.

(c) **Kujenga mbinu za uongozi:** Wanafunzi wanaochaguliwa kushika nafasi za uongozi hupata fursa ya kujifunza mbinu mbalimbali za uongozi. Mfano wa mbinu ya uongozi ni kutatua migogoro, matatizo na kufanya uamuzi sahihi. Jambo hili huwasaidia wanafunzi kutimiza majukumu ya kiuongozi katika jamii zao baada ya kuhitimu masomo yao.



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 115 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

1. Fafanua ni kwa namna gani mwanafunzi hujifunza demokrasia kwa vitendo kwa kushiriki uchaguzi shuleni?
2. Eleza kwa kifupi faida tatu za kushiriki uchaguzi shuleni.
3. Ni kwa namna gani mwanafunzi anaweza kujifunza mbinu za uongozi kwa kushiriki katika uchaguzi shuleni?

### Kazi ya kufanya namba 4

Jadiliana na wanafunzi wenzako namna mnavyoshiriki katika uchaguzi wa viongozi wa wanafunzi. Ainisha mambo uliyojifunza kupitia uchaguzi huo kisha yaandike katika daftari lako la mazoezi.

## Zoezi la 5

**A:** Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi.

1. Uaminifu ni nguzo muhimu inayokuwezesha kuishi na kukubalika kwa wenzako katika mazingira ya shule na jamii kwa ujumla. __________
2. Kutii sheria za shule humwezesha mwanafunzi kutokuaminika shuleni na katika jamii yake.__________
3. Kubeza imani na itikadi za watu wengine ni namna ya kuheshimu wengine.__________
4. Faida mojawapo ya uchaguzi shuleni ni kusaidia wanafunzi kujifunza demokrasia kwa vitendo. ___________
5. Mwanafunzi unapojitambua vyema hukusaidia kufikia malengo maalumu unayotaka kuyatimiza katika maisha yako.____________

**B:** Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake kwenye kisanduku.

6. Ni faida gani mwanafunzi hupata anapotimiza jukumu la kuhudhuria shuleni na kujifunza masomo yote darasani?



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 116 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a) kutokuhudhuria baadhi ya vipindi darasani
(b) kushirikiana na wenzake
(c) kujifunza kikamilifu na kushiriki shughuli nyingine kama michezo
(d) kuonesha wenzake njia kimasomo

7. Kujikinga na tabia hatarishi kama utumiaji wa dawa za kulevya na ngono huashiria nini kwa mwanafunzi?
   (a) anajituma
   (b) anawahi shuleni
   (c) ni kiongozi
   (d) anajitambua

8. Ipi ni mojawapo ya ishara ya kuheshimu sheria za shule?
   (a) kuchelewa shule
   (b) kuchonganisha wanafunzi wenzako
   (c) kufuata sheria za shule
   (d) kuheshimu wakubwa tu

9. Ipi kati ya vitendo vifuatavyo kinaonesha umuhimu wa kuheshimu imani na itikadi za wengine?
   (a) kubeza imani za wengine
   (b) kuchonganisha watu kwenye jamii
   (c) kuishi bila kubaguana kwa misingi ya kiimani na kiitikadi
   (d) kuishi kwa raha bila kujali vurugu za kiitikadi

10. Kutunza mali za shule kunamaanisha nini?
   (a) mojawapo ya kitendo cha ujasiri
   (b) mojawapo ya vitendo vinavyoleta kuaminika shuleni na katika jamii
   (c) mojawapo ya vitendo vya umashuhuri shuleni
   (d) mojawapo ya vitendo vya kizalendo kwa familia kwa kila mwanafunzi

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 117 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C:** Oanisha kipengele kutoka **Sehemu A** na maneno yaliyopo **Sehemu B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.

| Sehemu A | Jibu | Sehemu B |
|---|---|---|
| 11. Kuwahi shuleni | | (a) nguzo muhimu isiyokuwezesha kuishi na kukubalika na wenzako katika jamii |
| 12. Uaminifu | | (b) humwezesha mwanafunzi kutimiza azma yake ya kupata maarifa shuleni |
| 13. Kujituma | | (c) humfanya mtu kuwa maarufu sana |
| 14. Kutii sheria za shule | | (d) msingi wa kuwajibika |
| 15. Kujua mbinu za uongozi | | (e) faida za kushiriki katika uchaguzi shuleni |
| | | (f) mojawapo ya vitendo vya uadilifu |
| | | (g) humwezesha mwanafunzi kutimiza majukumu yake shuleni |
| | | (h) humsaidia mwanafunzi kukubalika shuleni na katika jamii |

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Azma | dhamira ya kufanya jambo au shughuli fulani |
| Imani | mapokeo ya maadili ya kidini au kiroho |
| Itikadi | mapokeo ya maadili ya kisiasa ya chama au kundi la wanachama |
| Uaminifu | uadilifu, unyofu wa tabia, ukweli |

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 118 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Tatu

## Kusimamia haki za binadamu

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza juu ya kusimamia haki za binadamu kwa kuainisha mila na desturi zinazokiuka haki hizo, madhara ya rushwa katika kusimamia haki za binadamu na kushirikiana na vikundi vya kijamii kutetea haki za binadamu. Katika sura hii, utajifunza wajibu wa mihimili mitatu ya dola katika kusimamia haki za binadamu, na uhusiano uliopo kati ya mihimili hiyo katika kusimamia haki za binadamu. Pia, utajifunza mambo yanayoweza kusaidia mihimili ya dola katika kusimamia haki za binadamu. Maarifa na ujuzi utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kueleza uhusiano uliopo kati ya mihimili mitatu ya dola katika kusimamia haki za binadamu.*

**Fikiri**

Ni nani mwenye jukumu la kusimamia haki za binadamu nchini Tanzania?

### Wajibu wa mihimili ya dola katika kusimamia haki za binadamu

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, mamlaka yote yenye kutekeleza madaraka ya kutawala, kutunga sheria au utoaji haki yatakuwa mikononi mwa mihimili ya dola. Mihimili ya dola ni Serikali, Bunge, na Mahakama. Vyombo hivi ndivyo vyenye jukumu kubwa la kusimamia haki za binadamu nchini. Kila chombo kina nafasi katika kuhakikisha hakuna dhuluma, uonevu, unyanyasaji na uvunjifu wa sheria miongoni mwa wananchi. Shughuli za mihimili hii mitatu hushabihiana ili kuhakikisha sheria za nchi zinafuatwa kwa manufaa mapana ya Taifa.

**Bunge**

Bunge ni mojawapo ya mihimili ya dola ambao husimamia na kudumisha haki za binadamu. Mhimili huu husimamia haki za binadamu kwa kutunga sheria, kujadili maoni ya mwananchi, kuisimamia Serikali katika utoaji wa huduma muhimu kwa wananchi, kuchunguza ukiukwaji wa haki za binadamu, na



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 119 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuridhia matamko mbalimbali yanayohusu haki za binadamu. Yafuatayo ni majukumu yanayotekelezwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kusimamia haki za binadamu:

(a) **Kutunga sheria:** Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina wajibu mkubwa katika kusimamia haki za binadamu. Ni chombo chenye mamlaka ya kutunga sheria na kupitisha miswada inayoletwa na Serikali inayohusu sheria za haki za binadamu. Sheria zinazohusu haki za binadamu zinazotungwa na Bunge husaidia kudumisha haki za binadamu kwa wananchi. Vilevile, sheria hizi hulinda raia dhidi ya uonevu na kuwawezesha kupata haki stahiki ikiwa ni pamoja na haki ya kuishi, haki sawa mbele ya sheria, uhuru wa kutoa mawazo, kujiunga na chama chochote cha siasa, kuabudu, haki ya kufanya kazi na haki ya kulindwa.

(b) **Kupokea maoni ya wananchi:** Haki za binadamu hutetewa na kujadiliwa na wabunge ambao huwakilisha maoni ya wananchi. Wananchi hutoa maoni au malalamiko yao kwa wabunge wa majimbo yao. Maoni hayo hutolewa katika mikutano mbalimbali ya hadhara na hata wakati mwingine kufika katika Ofisi Ndogo za Wabunge katika jimbo linalohusika. Maoni hayo ya wananchi yanaweza kuhusu kukosekana kwa huduma za msingi za kibinadamu kama vile, huduma za afya, elimu, maji na miundombinu. Wabunge huwasilisha malalamiko hayo bungeni na kufuatilia utekelezwaji wake. Kwa kufanya hivyo hutekeleza wajibu wa Bunge katika kutetea na kudumisha haki za binadamu.

(c) **Kuisimamia Serikali katika utoaji wa huduma muhimu:** Bunge lina jukumu la kuisimamia Serikali katika utoaji wa huduma za kijamii kwa wananchi. Serikali ina wajibu wa kulinda haki za binadamu kwa wananchi wake ili waweze kushiriki vyema katika shughuli za maendeleo. Bunge huisimamia Serikali kufanya utekelezaji wa utoaji wa haki za binadamu. Kupitia vikao na majadiliano mbalimbali, wabunge huwauliza mawaziri maswali mbalimbali yanayohusu wizara zao ambapo mawaziri huwajibika kutoa majibu juu ya utekelezaji wa mambo waliyoulizwa.

(d) **Kuchunguza ukiukwaji wa haki za binadamu:** Majukumu ya Bunge ni pamoja na kuchunguza ukiukwaji wa haki za binadamu nchini. Bunge ambalo hutunga sheria zinazohusu haki za binadamu lina wajibu pia kufuatilia ukiukwaji wa haki za binadamu. Aghalabu, wabunge watawasilisha malalamiko kuhusu ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Bunge linaweza kuunda kamati teule kuchunguza chanzo, sababu na watu waliohusika kukiuka au kuvunja haki za binadamu. Kwa mfano, mwaka 2014 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliunda kamati



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 120 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

teule kuchunguza ukiukwaji wa haki za binadamu wakati wa operesheni ya kupambana na ujangili. Matokeo ya uchunguzi yaliwasilishwa bungeni na maazimio mbalimbali yalifikiwa ikiwa ni pamoja na Bunge kuiagiza Serikali kuchukua hatua za kisheria kwa wale wote waliohusika.

(e) **Kuridhia matamko mbalimbali kuhusu haki za binadamu:** Bunge lina wajibu wa kuridhia matamko mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kuhusu haki za binadamu. Matamko hayo ya haki za binadamu yanaweza kutolewa na taasisi za Serikali au jumuiya za kimataifa kama Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika. Matamko haya yanapotolewa, Bunge lina wajibu wa kuridhia matamko hayo ili yaweze kutumika katika kutetea haki za binadamu kwa kuwa Tanzania ni mwanachama.

**Zoezi la 1**

1. Taja umuhimu wa sheria za haki za binadamu zinazotungwa na Bunge.
2. Elezea kwa kifupi majukumu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutetea haki za binadamu.
3. Fafanua kwanini huduma za afya ni muhimu katika kudumisha haki za binadamu.

**Kazi ya kufanya namba 1**

Jadiliana na wenzako katika kikundi kuhusu dhana ya haki sawa mbele ya sheria kisha wasilisha darasani kwa majadiliano zaidi.

## Mahakama

Mahakama ni mhimili wa dola ambao hutafsiri sheria, kusikiliza kesi na kutoa hukumu, kutoa elimu kuhusu haki za binadamu, na kutoa ushauri wa kisheria kwa wananchi. Mahakama kama ilivyo mihimili mingine ina jukumu la kusimamia na kudumisha haki za binadamu kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. Yafuatayo ni majukumu ya Mahakama katika kutekeleza wajibu wake wa kusimamia na kudumisha haki za binadamu nchini Tanzania:

(a) **Kutafsiri sheria:** Mahakama ina wajibu wa kutafsiri sheria zote zilizotungwa na Bunge zikiwamo zile zinazohusu haki za binadamu. Kazi ya kutafsiri sheria zinazohusu haki za binadamu hufanywa na Mahakama wakati wa usikilizaji wa kesi na utoaji wa hukumu. Hivyo,



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 121 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

tafsiri za mahakama kuhusu sheria mbalimbali zilizopitishwa na Bunge husaidia kusimamia na kudumisha haki za binadamu katika jamii.

(b) **Kutoa hukumu kwa kesi mbalimbali zikiwemo zinazokiuka haki za binadamu:** Ukiukwaji wa haki za binadamu miongoni mwa jamii husababisha kuwapo kwa migogoro katika jamii. Mahakama ni chombo cha kusimamia na kudumisha haki za binadamu. Jambo hili hufanyika kwa kusikiliza kesi na kutoa hukumu kwa wale waliobainika kwa makosa ya ukiukaji wa haki za binadamu. Hivyo, kupitia mashauri na hukumu zinazotolewa na Mahakama, wananchi hupewa haki zao. Pia, jambo hili husaidia jamii kuishi kwa amani na kudumisha utii wa sheria, kanuni na taratibu ambazo ndiyo msingi wa haki za binadamu.

(c) **Kutoa elimu kuhusu haki za binadamu:** Pamoja na kusikiliza mashauri na kutoa hukumu kuhusu masuala ya haki za binadamu, Mahakama pia ina wajibu wa kuelimisha umma katika masuala mbalimbali yanayohusu sheria na haki za binadamu. Mahakama hutoa elimu kwa kutumia vyombo vya mawasiliano kama vile, televisheni, redio, magazeti, makala mbalimbali na mitandao mingine ya mawasiliano. Pia, hutumia makongamano na mihadhara. Hivyo, njia hizi kusaidia kwa kiasi kikubwa kuielimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuheshimu haki za binadamu na madhara ya ukiukwaji wa haki hizo.

(d) **Kutoa ushauri wa kisheria:** Mahakama ina wajibu mwingine wa kutoa ushauri wa kisheria kwa raia kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu haki. Ushauri huo ni pamoja na njia za kufuata ili kutatua au kumaliza mashauri yanayohusu migogoro katika ndoa, ardhi, na masuala mengine yaliyopo katika jamii. Aghalabu, ushauri ambao huwa unatolewa na Mahakama husaidia wahusika kutoendelea na mashauri kwa njia ambayo inaweza kupoteza rasilimali nyingi wakati yanaweza kumalizwa vizuri zaidi kupitia njia za usuluhishi. Hivyo, kupitia njia hii ya ushauri, Mahakama husaidia kuimarisha kuwapo kwa haki za binadamu miongoni mwa wanajamii.

**Zoezi la 2**

1. Eleza kwa kifupi ni kwa namna gani Mahakama inasaidia kuelimisha jamii katika kulinda haki za binadamu.
2. Mahakama ina wajibu gani katika kutetea na kulinda haki za binadamu?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Kwanini Mahakama hutoa hukumu kwa raia wanaokiuka haki za binadamu?

**Kazi ya kufanya namba 2**



Kwa kushirikiana na wenzako kwenye kikundi, andaa igizodhima litakaloonesha namna Mahakama inavyosimamia haki za binadamu. Igizodhima hilo lifanyike wakati wa kipindi darasani.

**Serikali**

Serikali ni mhimili wa dola ambao una jukumu la kutekeleza sheria, kuratibu na kufanya shughuli za kiutawala katika nchi. Yafuatayo ni baadhi ya majukumu yanayofanywa na Serikali katika kusimamia haki za binadamu:

(a) **Kuandaa miswada:** Serikali ina jukumu la kuandaa miswada ambayo hupelekwa bungeni kwa ajili ya kupitishwa na kuwa sheria. Miswada inayohusu haki za binadamu huwasilishwa, hujadiliwa na hupitishwa na Bunge kuwa sheria. Aghalabu, miswada huandaliwa na Serikali baada ya kutokea jambo fulani au kuwapo kwa malalamiko au maoni kutoka kwa wananchi. Hivyo, miswada hiyo inayoandaliwa na Serikali huwasilishwa bungeni ili kutungiwa sheria ambazo zinalinda na kudumisha haki za binadamu nchini.

(b) **Kusimamia sheria:** Rais ambaye ni kiongozi mkuu wa mhimili wa Serikali ndiye anayesaini au kuidhinisha sheria zinazotungwa na Bunge kuanza kutumika. Serikali hufanya kazi ya kuhakikisha kuwa sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa ili kuendesha nchi kwa misingi ya haki na uwajibikaji zinazingatiwa. Kupitia jukumu hili, watu huweza kupata haki kulingana na sheria na taratibu za nchi zilizotungwa na Bunge na kutekelezwa na Serikali. Katika kutekeleza jukumu hili, Serikali huhimiza utawala wa sheria ambapo kila mwananchi hutakiwa kuheshimu sheria ili haki itendeke kwa kila mmoja.

(c) **Kutoa huduma muhimu kwa wananchi:** Ni kazi ya Serikali kuhakikisha upatikanaji wa huduma muhimu za jamii kama vile maji, umeme, afya, elimu, barabara na huduma nyingine. Serikali inapozingatia utoaji wa huduma muhimu za jamii kwa wakati, husaidia kutekeleza haki za binadamu kwa kuwa kila binadamu anastahili kupata huduma hizo.

(d) **Ulinzi wa raia na mali zao:** Serikali ina wajibu wa kusimamia haki za binadamu kwa kulinda raia wake na mali zao. Ulinzi wa raia na mali zao ukiimarishwa vyema, hakutakuwa na migogoro inayosababisha

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 123 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kutoweka kwa amani. Nchi inapokosa amani, husababisha uhalifu, vita, chuki, na mifarakano na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Hata hivyo, wananchi pia wanapaswa kushirikiana na vyombo vya dola kama vile Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika kulinda mali zao na kujilinda wenyewe.

**Zoezi la 3**

1. Ni kwa namna gani ulinzi na usalama unaimarishwa katika eneo unaloishi?
2. Elezea kwa kifupi jinsi Serikali ya mtaa au kijiji inavyohakikisha kuwapo kwa haki za binadamu kwa raia wake.
3. Eleza kwa kifupi namna vyombo vya dola katika eneo unaloishi vinavyohakikisha kuwapo kwa haki za binadamu.

## Uhusiano uliopo kati ya mihimili ya dola katika kusimamia haki za binadamu

Bunge, Mahakama na Serikali hufanya kazi kwa kushirikiana katika kukuza na kudumisha haki za binadamu. Bunge hutunga sheria zinazohusu haki za binadamu na kuiagiza Serikali kufuatilia ukiukwaji wa haki za binadamu. Kuwapo kwa wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi, hutoa fursa sawa ya uwakilishi bungeni na kusaidia Bunge kutekeleza wajibu wake wa kutunga sheria za kusimamia haki za binadamu ipasavyo.

Mahakama hutafsiri sheria, husikiliza kesi na kutoa hukumu na elimu kuhusu haki za binadamu. Kwa kufanya hivi Mahakama hutekeleza sheria zilizotungwa na Bunge kuhusu haki za binadamu.

Serikali husimamia utawala bora katika ngazi zote ili kutekeleza utoaji wa haki za binadamu na kuleta maendeleo kwa wananchi wake. Serikali ina jukumu la kusimamia sheria zilizotungwa na Bunge ili kulinda na kutetea haki za binadamu. Aidha, ina wajibu wa kuunda taasisi au vyombo vya kutetea, kuendeleza na kuzuia ukiukwaji wa haki za binadamu na kuwezesha kila mtu kupata haki yake kwa mujibu wa sheria zilizotungwa na Bunge.

Hivyo, mihimili hii ya dola inashirikiana katika kutetea na kulinda haki za

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 124 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

binadamu ili zisiweze kukiukwa. Kila mhimili unatakiwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo ili kuhakikisha hakuna ukiukwaji wowote wa haki za binadamu. Haki za binadamu zikilindwa na kusimamiwa ipasavyo hakutakuwa na migogoro katika jamii.

## Misingi inayoweza kusaidia mihimili ya dola katika kusimamia haki za binadamu

Ili mihimili ya dola iweze kusimamia haki za binadamu inapaswa kufuata misingi ifuatayo:

**(a)** **Utawala bora:** Mihimili ya dola ina wajibu wa kusimamia utekelezaji wa utawala bora katika kutimiza majukumu yake ya kulinda haki za binadamu. Utekelezaji wa majukumu kwenye mihimili hii hauna budi kuzingatia matumizi sahihi ya vyombo vya dola, na rasilimali za nchi kwa manufaa ya umma. Aidha, kila mhimili unatakiwa kutambua madaraka iliyonayo kulingana na mipaka iliyowekwa kwa mujibu wa Katiba.

**(b)** **Kuthamini utu wa kila mtu:** Kila mhimili wa dola una wajibu wa kuhakikisha utu wa binadamu wote unathaminiwa. Serikali, Bunge na Mahakama vina wajibu wa kuhakikisha na kusimamia haki za binadamu kwa kuhakikisha kwamba raia hawabaguliwi kwa misingi ya jinsi, kabila, rangi au dini zao. Pia, mihimili hii inapaswa kutambua usawa wa kila binadamu mbele ya sheria na kuepuka ubaguzi wa namna yoyote ile.

**(c)** **Kuwapo kwa uwazi na ukweli:** Katika kusimamia haki za binadamu ni lazima uwazi na ukweli viwepo. Uwazi na ukweli katika utekelezaji wa majukumu ya mihimili hii, husaidia wananchi kuwa na uelewa wa haki zao na hatua zinazochukuliwa kuzilinda. Ili kuhakikisha mihimili hii inatekeleza majukumu yake vyema, inawajibika kutoa taarifa juu ya utekelezaji na usimamizi wa haki za binadamu nchini kila wakati kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Ni muhimu panapotokea ukiukwaji wa haki za binadamu nchini, wananchi wapewe taarifa za matokeo ya ufuatiliaji wa matukio hayo. Hali hii itathibitisha utekelezaji wa haki za binadamu unaofanywa na kila mhimili.

**Zoezi la 4**

1. Eleza kwa kifupi jinsi utawala bora unavyoweza kusaidia katika kusimamia haki za binadamu.



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 125 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Ni kwa namna gani mihimili ya dola inavyoweza kushirikiana katika kusimamia haki za binadamu?

3. Ni vitendo gani vinavyofanywa na uongozi wa shule yako vinavyodhihirisha kuwapo kwa uwazi na ukweli katika kusimamia haki za wanafunzi?

### Kazi ya kufanya namba 3

Mkiongozwa na mwalimu wa somo, tembeleeni ofisi za kata au kijiji na kufanya mahojiano na viongozi jinsi wanavyotekeleza wajibu wao wa kulinda haki za binadamu katika jamii unamoishi.

### Zoezi la 5

**A.** Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi.

1. Kazi kuu ya Bunge ni kutekeleza sheria.__________
2. Mihimili ya dola inatambua kila mtu ni sawa mbele ya sheria.__________
3. Mahakama ni mhimili wa dola unaofanya kazi ya kutunga sheria. __________
4. Mihimili ni vyombo maalumu vyenye mamlaka ya kutawala, kuratibu na kufanya uamuzi.__________
5. Ukweli na uwazi husaidia matumizi sahihi ya vyombo vya dola.__________

**B:** Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake kwenye kisanduku.

6. Ipi kati ya yafuatayo si majukumu ya Serikali katika kusimamia haki za binadamu?
   (a) kutoa huduma za kijamii
   (b) kuzuia haki isitendeke kwa wahalifu
   (c) kulinda amani na utulivu
   (d) kulinda rasilimali za nchi

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 126 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

7. Kipi kati ya vyombo vifuatavyo hufanya kazi ya kuhakikisha haki inatolewa kwa wananchi kwa kutoa huduma za kijamii?
   (a) Mahakama
   (b) Serikali
   (c) Bunge
   (d) Jeshi

8. Ni kwa namna gani mhimili wa Mahakama hutumia makongamano na mihadhara katika kusimamia haki za binadamu nchini?
   (a) hutoa elimu kwa wananchi ili kupata haki zao bila kubughudhiwa au kuonewa kwa namna yoyote
   (b) hutoa elimu kwa wananchi juu ya namna ya kuacha watumishi wa mahakama kufanya uamuzi kwa utashi wao tu
   (c) hutoa elimu kwa wananchi juu ya kutokukemea vitendo vya rushwa na ufisadi
   (d) hutoa elimu juu ya namna ya watu kudai haki zao kwa woga

9. Ni jukumu la nani kuimarisha haki za binadamu, ulinzi na usalama nchini?
   (a) Serikali
   (b) vyombo vya dola
   (c) mihimili ya dola
   (d) raia wote

10. Serikali inaposimamia utoaji wa huduma stahiki kwa wananchi hutekeleza jukumu gani?
   (a) haki za raia wake
   (b) haki za binadamu
   (c) mali za nchi
   (d) usalama wa nchi

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 127 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C:** Oanisha kipengele kutoka **Sehemu A** na maneno yaliyopo **Sehemu B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.

| Sehemu A | Jibu | Sehemu B |
|---|---|---|
| 11. Bunge | | (a) kutoa hukumu |
| 12. Mswada | | (b) matamko ya haki za binadamu |
| 13. Haki ya kuishi na uhuru wa kutoa mawazo | | (c) haki za binadamu |
| 14. Umoja wa Afrika | | (d) mapendekezo ya maandishi ambayo huwasilishwa bungeni ili kujadiliwa na kupitishwa kama sheria |
| 15. Mahakama | | (e) kuratibu na kufanya shughuli za kiutawala |
| | | (f) husimamia na kudumisha haki za binadamu |
| | | (g) chombo cha kutunga sheria |
| | | (h) hutoa matamko mbalimbali kudumisha haki za binadamu katika nchi za Afrika |

**Msamiati**

Makala — habari zilizoandikwa kuelezea jambo

Mswada — mapendekezo ya maandishi ambayo huwasilishwa bungeni ili yajadiliwe na kupitishwa kuwa sheria

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Nne

## Kujenga urafiki na mataifa mengine

**Utangulizi**

*Ulipokuwa Darasa la Sita, ulijifunza umuhimu wa kudumisha uhusiano wa kiutamaduni, kibiashara na kimichezo kwa watu wenye asili ya mataifa tofauti. Pia, ulijifunza jinsi ya kuishi na watu wa asili nyingine na mikakati ya kukabiliana na athari ya utandawazi. Katika sura hii, utajifunza maana ya ubalozi, nchi ambazo Tanzania imefungua ofisi za ubalozi, majukumu ya mabalozi wa Tanzania nchi za nje, na umuhimu wa kuwa na ubalozi wa Tanzania katika mataifa mengine. Aidha, utajifunza fursa zinazotokana na uhusiano wa kibalozi na njia za kudumisha uhusiano wa kibalozi kati ya Tanzania na nchi nyingine. Maarifa na ujuzi utakaopata katika sura hii, utakuwezesha kutumia balozi za Tanzania zilizopo katika nchi mbalimbali, na kufahamu fursa za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni zilizo katika nchi hizo na kuzitumia.*

**Fikiri**

Duniani kuna mataifa mengi sana. Kila taifa lina utamaduni wake. Je, tunawezaje kuishi kwa kushirikiana bila kugombana?

### Uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine

Uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine ni jambo la msingi kwa maendeleo ya Taifa na wananchi wake kwa ujumla. Tanzania ina uhusiano na mataifa mbalimbali ulimwenguni ambao husaidia katika kukuza ushirikiano wa kidiplomasia, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kiteknolojia. Uhusiano huu hukuzwa na kuimarishwa kupitia uwakilishi wa nchi katika mataifa mengine kwa kufungua ofisi za ubalozi katika nchi hizo.

### Maana ya ubalozi

Ubalozi ni ofisi ya uwakilishi wa nchi moja katika nchi nyingine. Kidiplomasia, eneo la ubalozi huhesabika kuwa ni ardhi ya nchi anakotoka balozi katika nchi mwenyeji. Balozi ni mwakilishi wa nchi katika nchi mwenyeji. Kazi za ubalozi ni kuwakilisha, kuimarisha uhusiano na ushirikiano, kulinda, kutetea



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 129 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

na kuwakilisha masilahi ya nchi katika nchi inayohusika, kwa mfano, katika masuala ya kisiasa, kiuchumi, uwekezaji, utalii na biashara. Pia, ubalozi huandaa na kutoa viza, hati ya kusafiria na nyaraka nyingine kwa wananchi wa nchi aliyopo balozi kwenda nchi anakotoka balozi. Kwa mfano, Ofisi ya Ubalozi wa Misri nchini Tanzania, hutoa viza kwa wananchi wa Tanzania wanaotaka kwenda nchini Misri.

**Baadhi ya nchi ambazo Tanzania imefungua ofisi za ubalozi**

Katika kujenga urafiki mwema na mataifa mengine, Tanzania imefungua ofisi za ubalozi katika nchi mbalimbali duniani. Zifuatazo ni baadhi ya nchi ambazo Tanzania imefungua ofisi za ubalozi:

(a) Afrika Mashariki – Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi;
(b) Kusini mwa Afrika – Zambia, Zimbabwe, Malawi, Botswana, Afrika Kusini, na Namibia;
(c) Bara la Ulaya – Uingereza, Ufaransa, Swideni, na Ujerumani;
(d) Bara la Asia – Israeli, Saudia Arabia, China, na Korea ya Kusini; na
(e) Bara la Amerika Kaskazini - Marekani na Kanada

## Majukumu ya Ubalozi wa Tanzania nchi za nje

Majukumu ya Ubalozi wa Tanzania nchi za nje yamegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni majukumu ya ofisi ya ubalozi na majukumu ya balozi.

**Majukumu ya ofisi ya ubalozi**

Majukumu ya Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania nchi za nje yamegawanyika katika makundi yafuatayo:

**(a)** **Majukumu ya kisiasa:** Ofisi za Ubalozi wa Tanzania zina majukumu ya kujenga, kudumisha na kuendeleza uhusiano wa kisiasa kati ya Tanzania na nchi inayohusika. Vilevile, zina jukumu la kulinda masilahi ya kisiasa kati ya Tanzania na nchi rafiki.

**(b)** **Majukumu ya kiuchumi:** Ofisi ya Ubalozi ina jukumu la kukuza uchumi wa Tanzania na masilahi mengine kama vile biashara, uwekezaji na utalii. Pia, inawajibika kukuza diplomasia ya uchumi kwa kutangaza vivutio vya utalii na uwekezaji vilivyopo Tanzania.

**(c)** **Majukumu ya kiutamaduni:** Ofisi ya Ubalozi ina jukumu la kudumisha ushirikiano wa kiutamaduni kati ya Tanzania na nchi balozi anakowakilisha. Pia, kulinda haki na masilahi ya Watanzania wanaoishi katika nchi inayohusika ikiwa ni pamoja na kusaidia kupata fursa za kielimu, kiutamaduni na biashara.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**(d) Majukumu ya uwakilishi:** Majukumu ya uwakilishi ni pamoja na kutoa viza, kuzihuisha, kubadilisha, na kutoa hati za dharura za kusafiria kwa wananchi wa Tanzania wanaoishi kwenye nchi inayohusika. Pia, hupokea maombi ya wananchi wa nchi mwenyeji wanaotaka kuwa raia wa Tanzania na kuziwasilisha nchini Tanzania kwa uamuzi. Vilevile, kutoa huduma za ushauri kwa Watanzania wanaoishi katika nchi inayohusika.

**(e) Majukumu mengine:** Majukumu mengine ya Ofisi ya Ubalozi ni pamoja na kuimarisha ushirikiano kati ya mashirika yasiyo ya kiserikali ya Tanzania na yale ya nchi balozi alikotumwa. Ofisi ya Ubalozi ina jukumu la kudumisha ushirikiano kati ya Tanzania na nchi inayohusika, katika nyanja za elimu, sayansi na teknolojia.

**Majukumu ya balozi**

Balozi kama kiongozi mwakilishi wa Tanzania katika nchi mwenyeji kuwa balozi ana majukumu yafuatayo:

(a) Kukutana na viongozi wa nchi mwenyeji na wawakilishi wengine mbalimbali;
(b) Kufanya majadiliano kuhusu makubaliano na mikataba kati ya Tanzania na nchi mwenyeji;
(c) Kufuatilia hali ya uhusiano wa kimataifa ulimwenguni;
(d) Kufuatilia miradi na misaada kutoka nchi mwenyeji; na
(e) Kuratibu ziara za viongozi wa Tanzania katika nchi mwenyeji.

**Zoezi la 1**

1. Nini maana ya neno ubalozi?
2. Taja majukumu matano ya mabalozi wa Tanzania nchi za nje.
3. Fafanua majukumu ya ofisi ya ubalozi katika nchi ambayo Tanzania ina uhusiano wa kibalozi.
4. Taja nchi zingine tano ambazo Tanzania imefungua ofisi za ubalozi tofauti na zilizotajwa hapo juu.

## Umuhimu wa kuwa na Ubalozi wa Tanzania katika mataifa mengine

Ofisi za Ubalozi wa Tanzania zilizopo katika nchi mbalimbali duniani husaidia wananchi wa nchi zote mbili kupata taarifa na fursa mbalimbali. Fursa hizi husaidia Watanzania kufanikisha shughuli zao za maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Umuhimu wa kuwa na Ubalozi wa Tanzania katika mataifa mengine

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 131 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ni kama ifuatavyo:

(a) **Nafasi za ajira:** Balozi hutoa matangazo ya ajira mbalimbali za kimataifa ili Watanzania wenye sifa waweze kuomba nafasi hizo. Nafasi hizo za ajira zinaweza kuwa katika mashirika, asasi au taasisi za kimataifa.

(b) **Vivutio vya uwekezaji katika nchi mbalimbali:** Ubalozi wa Tanzania katika mataifa mengine huisaidia nchi yetu kupata wawekezaji katika sekta mbalimbali kama madini, kilimo na biashara. Kupitia ubalozi wake, Tanzania inaweza kupata fursa ya kutangaza vivutio vilivyomo nchini kama vile, mbuga za wanyama, milima, maporomoko na utamaduni. Vivutio hivi huwezesha nchi kukua kiuchumi kutokana na watalii kuvutiwa kutembelea vivutio hivyo na kuongeza pato la Taifa.

(c) **Mikopo na ufadhili wa huduma za jamii:** Balozi hizi husaidia kupatikana kwa misaada na mikopo kwa ajili ya kuimarisha huduma za jamii. Kwa mfano, mikopo kwa ajili ya ujenzi wa barabara, hospitali na vituo vya afya, miradi ya maji, miradi ya elimu na nafasi za masomo.

(d) **Masoko ya bidhaa na huduma:** Ofisi za Ubalozi hutafuta masoko ya bidhaa zinazopatikana katika nchi ya Tanzania ili kukuza biashara na kutangaza malighafi zilizopo nchini na zile zilizopo kwenye nchi alipo balozi.

(e) **Ujuzi wa sayansi na teknolojia:** Ofisi za Ubalozi huhamasisha nchi kubadilishana uzoefu wa sayansi na teknolojia ili kujenga uchumi imara kwa wananchi wake. Kwa kufanya hivyo, ofisi za ubalozi hukuza ubunifu, huibua vipaji vipya na kuongeza maarifa na ujuzi kwa wataalamu waliopo. Lengo ni kuongeza ufanisi wa matumizi ya teknolojia katika nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Ili uhusiano na fursa mbalimbali ziweze kupatikana kutoka mataifa mengine, ofisi za ubalozi husaidia upatikanaji wa taarifa na fursa zilizopo katika nchi zao kwa kutumia njia mbalimbali. Njia hizo ni kama vile, televisheni na redio, tovuti, mitandao ya kijamii na ziara za maonesho ya biashara. Njia hizi husaidia katika kuimarisha uhusiano kati ya taifa moja na mataifa mengine.

Kielelezo namba 1 na 2 vinaonesha wanafunzi wakipata taarifa kutoka baadhi ya nchi ambazo Tanzania ina uhusiano wa kibalozi. Chunguza vielelezo hivyo kwa makini, kisha jibu maswali yanayofuata.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 1**: *Wanafunzi wakipata taarifa mbalimbali kutoka ofisi ya Ubalozi wa China nchini Tanzania*




**Kielelezo namba 2:** *Wanafunzi wakipata taarifa katika banda la nchi ya Syria katika maonesho ya Saba Saba*



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 133 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2

1. Chunguza Kielelezo namba 1, kisha eleza ulichojifunza kutokana na kielelezo hicho.
2. Je, kitendo kinachooneshwa katika Kielelezo namba 2 kina faida gani kwako?
3. Eleza kwa kifupi njia nne za kupata taarifa na fursa katika ofisi za ubalozi.

### Kazi ya kufanya namba 1

Jadiliana na wanafunzi wenzako namna ofisi za ubalozi wa kigeni zinavyochangia kuleta maendeleo ya kiuchumi na uwekezaji katika nchi ya Tanzania.

### Fursa zinazotokana na uhusiano wa kibalozi

Zifuatazo ni fursa zinazotokana na uhusiano wa kibalozi kati ya Tanzania na nchi nyingine:

(a) **Fursa za biashara:** Moja ya majukumu ya Balozi wa Tanzania nje ya nchi ni kutafuta fursa za kibiashara. Katika kutekeleza wajibu huo, wafanyabiashara wa Tanzania wamekuwa wakipata fursa za kupeleka bidhaa zao nje ya nchi ambako kuna masoko. Kwa mfano, Tanzania ina fursa ya kuuza mazao ya nafaka katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Haya ni matokeo ya uhusiano mwema wa kibalozi kati ya Tanzania na nchi hizi.

(b) **Misaada ya kitaalamu:** Moja ya manufaa ya uhusiano wa kibalozi kati ya Tanzania na nchi nyingine ni kupata misaada ya kitaalamu kutoka katika nchi zilizoendelea na zinazoendelea. Wataalamu wa afya na maeneo mengine ya kiteknolojia wamekuwa wakija Tanzania na wataalamu wa maeneo hayo kutoka Tanzania kwenda kupata utaalamu kutoka katika mataifa haya. Haya yanawezekana kutokana na uhusiano mzuri kati ya Tanzania na mataifa mengine.

(c) **Fursa za masomo:** Kutokana na uhusiano mzuri wa kibalozi kati ya Tanzania na mataifa mengine, Watanzania wengi wamekuwa wakipata fursa za kwenda kusoma katika mataifa hayo na kuongeza ujuzi ambao ni kwa manufaa ya nchi. Baadhi ya mataifa hayo ni: China, Ujerumani, Marekani, Urusi, Kuba na Uturuki.

(d) **Misaada ya kifedha:** Baadhi ya mataifa yenye uhusiano wa kibalozi



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 134 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

na Tanzania yamekuwa yakifanya makubaliano ya moja kwa moja na Tanzania na kutoa misaada ya kifedha kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo, mathalani ujenzi wa barabara na hospitali.

(e) **Teknolojia na uwekezaji:** Uhusiano wa kibalozi husaidia kupata teknolojia mpya na wawekezaji. Mabalozi wana wajibu wa kujua teknolojia mpya na kuwashawishi wawekezaji kutoka nchi hizo kuja kuwekeza Tanzania. Uwekezaji huongeza pato la Taifa kwa kuongeza makusanyo ya kodi, bidhaa za kuuza ndani na nje pamoja na huduma mbalimbali.

## Kudumisha uhusiano wa kibalozi kati ya Tanzania na nchi nyingine

Uhusiano kati ya Tanzania na nchi nyingine unaweza kudumishwa kwa kufanya yafuatayo:

(a) **Dhamira thabiti:** Ili kuboresha na kuendeleza uhusiano wa kibalozi ni muhimu kuwapo kwa dhamira thabiti katika kutekeleza yale ambayo nchi mbili zenye uhusiano zimekubaliana. Uhusiano unajengwa katika misingi ya masuala ya kushirikiana. Uwazi na uwajibikaji utasaidia kudumisha uhusiano mwema.

(b) **Majadiliano:** Majadiliano ya mara kwa mara ni msingi wa uhusiano mwema wa kibalozi. Nchi mbili zenye uhusiano zinahitaji majadiliano yenye kuleta tija kwa mataifa yote mawili. Mathalan, panapotokea kutokuelewana katika baadhi ya mambo, ni vyema nchi hizo kukaa pamoja na kupata ufumbuzi wa changamoto hizo kwa pamoja.

(c) **Kushirikiana katika kutafuta fursa:** Ili kudumisha uhusiano mwema nchi zenye uhusiano wa kibalozi, hazina budi kushirikiana katika kutafuta fursa za kiuchumi na biashara. Ushirikiano huongeza nguvu katika kutafuta fursa mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Fursa hizi zinaweza kutumika kwa manufaa ya pande zote mbili. Uwiano katika manufaa husaidia kuongeza ushirikiano.

(d) **Uaminifu:** Ili kuimarisha uhusiano wa kibalozi kati ya nchi moja na nchi nyingine, ni muhimu kuaminiana wakati wa kupanga, kujadili na kutekeleza masuala mbalimbali. Uaminifu unapokuwapo kati ya nchi na nchi, hujenga uhusiano imara na wenye manufaa.

(e) **Kutumia njia ya kidiplomasia katika kusuluhisha migogoro:** Uhusiano wa kidiplomasia huimarika pale nchi mbili zenye uhusiano zinapotafuta njia nzuri za kusuluhisha migogoro. Njia nzuri ni zile zinazotanguliza masilahi ya wananchi wa nchi zote mbili.

(f) **Kuimarisha mawasiliano:** Mawasiliano bora kati ya pande mbili yatakuzwa na kuendelezwa kwa viongozi kutembeleana, kubadilishana



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 135 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

uzoefu na ziara za mafunzo ya viongozi na watendaji wa nchi hizo.

## Zoezi la 3

1. Kwa namna gani balozi anaweza kudumisha uhusiano mzuri kati ya Tanzania na nchi anayoiwakilisha?
2. Eleza namna ofisi za ubalozi zinavyoweza kutumika kukuza biashara na uwekezaji katika nchi yetu.
3. Eleza ni kwa jinsi gani uhusiano wa kibalozi unaweza kurahisisha mawasiliano kati ya Tanzania na nchi inazohusiana nazo.

## Kazi ya kufanya namba 2

Jadiliana na wanafunzi wenzako jinsi gani mwananchi wa kawaida anavyoweza kudumisha uhusiano mwema kati ya Tanzania na nchi nyingine. Andika majibu mliyopata katika daftari lako la mazoezi.

## Zoezi la 4

**A:** Andika **Kweli** kwa sentensi iliyo sahihi na **Si Kweli** kwa sentensi isiyo sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi.

1. Tanzania ni nchi isiyohitaji kuwa na uhusiano na nchi nyingine.
   ____________
2. Serikali inapojenga mazingira mazuri ya uwekezaji wa ndani na nje huzuia kukua kwa uchumi. ____________
3. Sayansi na teknolojia si nyenzo muhimu katika kutatua changamoto za uhusiano kati ya Tanzania na nchi nyingine.____________
4. Kazi kuu ya balozi ni kuwakilisha nchi mwenyeji. ____________
5. Kutangaza vivutio vya utalii na uwekezaji kwa mataifa mengine ni jukumu la kila Mtanzania.___________



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 136 30/07/2021 20:42
FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B:** Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake kwenye kisanduku.

6. Ipi ni kazi kubwa ya mabalozi wa Tanzania katika nchi za nje?
   (a) kukuza ushirikiano wa kidiplomasia, kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiteknolojia na mataifa mengine
   (b) kufanya biashara za kimataifa
   (c) kuandaa ziara za viongozi nje ya nchi
   (d) kuunda umoja wa mataifa ya kigeni

7. Ipi kati ya zifuatazo ni njia za haraka za kutangaza fursa zilizopo Tanzania katika nchi za kigeni?
   (a) tovuti, mitandao ya kijamii, majarida, na vipeperushi
   (b) simu za mkononi
   (c) mikutano ya kisiasa
   (d) redio

8. Ipi kati ya njia zifuatazo hukuza uhusiano zaidi miongoni mwa mataifa?
   (a) usafirishaji wa bidhaa
   (b) uwekezaji
   (c) utalii
   (d) utandawazi

9. Nani mwenye mamlaka ya kufanya uteuzi wa mabalozi wa kuiwakilisha Tanzania nchi za nje?
   (a) Baraza la Mawaziri
   (b) Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Tanzania
   (c) Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
   (d) Waziri Mkuu

FOR ONLINE USE ONLY



URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 137 30/07/2021 20:42

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C:** Oanisha kipengele kutoka **Sehemu A** na maneno yaliyopo **Sehemu B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.

| Sehemu A | Jibu | Sehemu B |
|---|---|---|
| 10. Diplomasia | | (a) jukumu la kila Mtanzania |
| 11. Kulinda heshima na usalama ya nchi yetu | | (b) hali ya nchi moja kutokuelewana na nchi nyingine |
| 12. Biashara na ajira | | (c) utatuzi wa changamoto zinazotokana na uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine |
| 13. Jukumu la Watanzania kutangaza nchi yao | | (d) maarifa na ustadi wa kuendesha na kusimamia uhusiano wa kimataifa |
| 14. Kuwakilisha nchi kimataifa | | (e) mojawapo ya majukumu ya balozi wa Tanzania kwa mataifa mengine |
| | | (f) hupunguzia nchi mapato na fursa za ajira |
| | | (g) athari za Watanzania kutokutii sheria za nchi nyingine |
| | | (h) fursa zilizopo kutokana na uhusiano wa Tanzania na nchi za nje |
| | | (i) kukuza uhusiano mwema na raia wa nchi nyingine |

## Msamiati

Diplomasia — maarifa na stadi za kuendesha na kusimamia uhusiano wa kimataifa

Fursa — nafasi iliyopo ya kufanya jambo fulani


FOR ONLINE USE ONLY





URAIA DARASA LA 7 FINAL.indd 138 30/07/2021 20:42


## Taasisi ya Elimu Tanzania


## Vitabu vingine vya Darasa la Saba









ISBN 978-9987-09-142-3

Uraia na Maadili 7 Cover Mwanafunzi FOR SALE.indd 1